Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page i

# Historia na Sira za Viongozi Waongofu

## Sehemu ya Kwanza

Kimeandikwa na:
**Jopo la waandishi wa Vitabu vya Kiada**

Kimetarjumiwa na:
**Hemedi Lubumba Selemani**

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**

**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 512 - 38 - 6**

Kimeandikwa na:
**Jopo la waandishi wa vitabu vya kiada**

Kimetarjumiwa na:
**Hemedi Lubumba Selemani**

Kupangwa katika Kompyuta na:
**Hajat Pili Rajab.**

Toleo la kwanza: Mei, 2010
**Nakala: 1000**

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page iii

**ترجمة**

تاريخ وسيرةُ القادةٍ الهداة

تأليف

لجنة تأ ليف الكتب الدراسية

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

# YALIYOMO


**Somo la kwanza**

Hatu ya kwanza kuelekea kwenye masomo ya sira na historia ya Uislamu............................................................................2

**Somo la Pili**

Muhammad bin Abdullah (s.a.w.w) ni utabiri wa Manabiii (a.s)..............................................................................11

**Somo la Tatu**

Mazingira safi............................................................17

**Somo la Nne**

Maisha ya Nabii wa mwisho....................................................25

Maisha ya Mtume na Historia ya Uislamu ndani ya mstari....31

**Somo la Tano**

Tabia na mwonekanoo wa hitimisho la Manabii (s.a.w.w)......37

**Somo la Sita**

Tabia na mwonekano wa hitimisho la manabii (s.a.w.w)................46

**Somo la Saba**

Tabia na mwonekano wa hitimisho la manabii ................................55

**Somo la Nane**

Urithi wa mbora wa Mitume....................................................62

**Somo la Tisa**

Dondoo za Maisha ya mbora wa Manabii...............................68

Kukua kwa Imam Ali bin Abu Talib na hatua za maisha yake.69

**Somo la Kumi**

Mwonekano wa utu wa Imam Ali bin Abu Talib (a.s).............77

**Somo la Kumi na moja**

Sifa za Imam Ali (a.s) na mwonekano wake...........................83

**Somo la Kumi na mbili**

Sifa za Imam Ali (a.s) na mwonekano wake...........................92

**Somo la Kumi na Tatu**

Urithi wa Imam Ali (a.s)........................................................101

**Somo la Kumi na nne**

Urithi wa Imam Ali (a.s)........................................................107

**Somo la Kumi na tano**

Fatma Az-Zahrau mama wa Maimam watakasifu..................116

**Somo la Kumi na Sita**

Mwonekano wa utu wa Fatma Az-Zahrau..............................124

**Somo la Kumi na Saba**

Fadhila na mwonekano wa Az-Zahrau (a.s)...........................131

**Somo la Kumi na Nane**

Fadhila na mwonekano wa Az-Zahrau (a.s)...........................141

**Somo la Kumi na Tisa**

Urithi wa Az-Zahrau..............................................................148

بسم الله الرحمن الرحيم

## NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho *Tarikh wa Sirati 'l-Qadati 'l- Hudaah.* Sisi tumekiita, *Historia na Sira za Viongozi Waongofu.*

Kitabu hiki ni matokea ya kazi ya kielimu iliyofanywa na wanavyuoni wa Kiislamu waliomo kwenye Jopo la Waandishi wa Vtabu vya Kiada katika Taasisi ya Kimataifa ya Hawza na Madrasa. Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Hemedi Lubumba Selemani kwa kukubali kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

**Mchapishaji:**

Al-Itrah Foundation

S. L. P. 19701

Dar es salaam, Tanzania.

# UTANGULIZI

Hamna shaka kuwa historia ya mwanadamu ndio chemchemu na chanzo cha maarifa, chanzo ambacho mataifa yanakihitaji katika safari yake yenye kuendelea. Na ndio chanzo pekee chenye uwezo wa kuhuisha na kulisukuma taifa mbele na kulipa sifa na hadhi maalum huku kikilifunganisha taifa hilo na mizizi yake ya ustaarabu ambayo hulizuwia taifa dhidi ya mmong'onyoko.

Qur'ani imemhimiza kila mwanadamu ikamtaka azame ndani ya historia ya mwanadamu na azingatie yaliyomo ili awaidhike na kuongoka, hivyo Mwenyezi Mungu akasema: "Je, hawatembei katika ardhi ili wapate nyoyo za kufahamia au masikio ya kusikilizia?"[1] Baada ya Mwenyezi Mungu kutoa historia ya Adi, Thamudi, Firauni, watu wa miji iliyopinduliwa na watu wa Nuh akasema: "Ili tuifanye ukumbusho kwenu na sikio lisikialo lisikie."[2]

Historia ya ujumbe mbalimbali wa Mwenyezi Mungu imejaa masomo na mazingatio, masomo ambayo yameonyesha jinsi manabii watukufu walivyojali mataifa yao ili kuyaokoa toka kwenye matatizo mbalimbali. Pia ujumbe huo umeonyesha lengo na mwelekeo wake wenye kujaa nuru na manufaa. Kwa ajili hiyo sira ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kizazi chake huwa ni tafsiri ya kivitendo ya misingi na sheria za kiislamu.

Hivyo kusoma sira yao na historia ya maisha yao ni chanzo muhimu cha kuifahamu Qur'ani na Sunna, na ni chemchemu ya maarifa ya wanadamu wote, kwa sababu ni ujumbe wa Mwenyezi Mungu alioutuma kwa wanadamu huku Nabii wa mwisho na mawasii wake

---

1 *Al-Hajj*: 46.

2 *Al-Haaqah*: 12.

wateule wakiwa ni viongozi wa wanadamu wote bila kubagua.

Tumeona ni vizuri tuweke silabasi kwa ajili ya kusoma historia ya kiislamu kwa kufuata hatua moja baada ya nyingine, kwani masomo ya historia ya nukuu hutangulia kabla ya masomo ya uchambuzi**.**

Na kwa kuwa umma wote umekongamana juu ya wema na utakaso wa viongozi wa ujumbe wa Mwenyezi Mungu basi inafaa tuingize historia ya maisha yao ndani ya maisha ya wanafunzi, kwani Qur'ani imetamka wazi kuhusu umaasumu na utakaso wao ili wawe ni kiigizo chema kwa yule anayetarajia fadhila za Mwenyezi Mungu na malipo mema ya Siku ya Kiyama.

**Lengo la silabasi ya kitabu hiki**

Kitabu "Masomo ya utangulizi katika historia na sira ya viongozi wema" kimetungwa ili kiwe hatua ya mwanzo ya kuelekea kwenye masomo mbalimbali ya lengo la kina zaidi, huku kikitegemea kufikia lengo hilo kwa kutumia wepesi wa ibara, usalama wa nukuu na vyanzo vyenye kukubalika ili kitoe picha ya wazi isiyokuwa na utata, shaka au hisia ambazo huenda zikamchanganya msomaji wa sira na historia mwanzoni tu mwa safari yake hii**.**

Masomo haya sitini yataanza kuzungumzia historia na sira kwa mtazamo wa Qur'ani, kisha yatatoa maisha binafsi na ya kijamii ya kila mmoja kati ya maasumina kumi na wanne (a.s.), na mwisho yataishia kwenye uwanja kati ya viwanja vya urithi wao wenye kunukia manukato. Mwisho kabisa tutatoa faida ya maisha yao ya ujumbe huku tukionyesha mavuno ambayo yamepatikana ndani ya karne tatu bali ni zaidi ya karne kumi na nne za mapambano yenye kuendelea kwa ajili ya kuuokoa umma wa kiislamu na jamii ya wanadamu toka kwenye yale yaliyowapata na waliyonasa ndani yake.

Na ili yawe maandalizi mema yenye kuunea na mapinduzi ya kiulimwengu ambayo yanamsubiri kiongozi wake wa kiroho, Imam angojewaye Al-Mahdi (a.s.) ambaye Mwenyezi Mungu aliwaahidi watu wa mataifa yote, ili aje kuunganisha nguvu na kuzifanya vizuri hali zao huku akiwaokoa wanadamu toka kwenye upotevu na kutimiza matarajio ya manabii na akitimiza wema wa ubinadamu, wema ambao bado binadamu anaendelea kuutolea juhudi zake usiku na mchana.

Hivyo mafunzo ya historia yamegawanywa katika sira binafsi na sira ya kijamii, huku yakiwa hayana uchambuzi wa matukio ya kihistoria wala kuzama sana ndani ya matukio makuu ya kihistoria, hiyo ni ili baadaye yafuatiwe na masomo mapana zaidi kuliko mafunzo haya. Pia tumejiepusha na urudiaji huku tukikomea kwenye historia ya ujumbe wenyewe na yale yaliyopita katika mzunguko na vipindi vya ujumbe na kwenye matokeo yaliyopatikana ndani ya karne zilizopita ambazo ziliupitia Uislamu na waislamu.

Mada hizi zimetimia kwa kufuata uchambuzi wa kielimu dhidi ya matukio yaliyosajiliwa ndani ya vitabu vya historia au yaliyogunduliwa na watafiti. Katika hali zote mbili tumejaribu kutegemea juhudi za wale waliotutangulia, ambazo ni masomo ya waandishi na watafiti ili kupata matunda ya juhudi zao na kuunganisha kati ya watu wa zamani na kizazi cha sasa. Pia ili tuwafunze vijana dharura ya kupitia rejea za kutegemewa za zamani na za sasa bila kudhulumu haki za waliyotangulia bali ili zionekane juhudi zao na jinsi walivyochangia katika uwanja wa elimu na maarifa ya jamii, na ili kuijua nafasi waliyonayo katika kunukuu urithi na kuvipelekea vizazi vyenye kufuata.

Waandishi wa zama hizi tutakaowataja ni Sheikh Baqir Sharifu Al-Qarashiy, Sayyid Murtaza Al-Askariy, marehemu Sheikh Asad Haydar, mashahidi wawili: Sayyid Muhammad Baqir As-Sadri na

Sayyid Muhamad Baqir Al-Hakim. Kisha Sayyid Jafar Murtaza Al-Amiliy, Sheikh Muhammad Had Al-Yusufiy Al-Gharawiy na wengine ambao tumegusia vitabu vyao mwishoni mwa kila mada ambayo tumenukuu toka kwao.

Ni wajibu wetu kusema: Kitabu hiki ni mjumuisho wa mada mbalimbali na utunzi unaolenga mafunzo ambayo yamezagaa ndani ya vitabu maalumu vilivyoteuliwa kufundisha sira ya kizazi cha Mtume (s.a.w.w.) ili iwe ni mali kwa mtafiti, mwanafunzi, mhutubu, mubalihghiina, mlezi na mlelewa ili ajiandae na masomo ya juu zaidi katika historia ya Uislamu kwa ajili ya kupambana mapambano ya kielimu dhidi ya matukio ya kihistoria na kijamii, na ili tuzame ndani huku tukipata mafunzo toka humo ili yawe ni mazingatio kwa msomaji na mawaidha kwa mwenye mazingatio, insha'allah.

Kutokana na maelezo yaliyopita, kwa muhtasari tunatoa matokeo yafuatayo:

**Kwanza:** Katika hatua hii mwalimu anapofundisha historia asitegemee kukutana na mafunzo ya kihistoria yenye mtiririko wa kuungana na kufuatana kwa maana iliyozoeleka. Kwa kuanzia jografia na historia ya Bara la Uarabu, kisha utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na dola yake, kisha dola ya makhalifa ambao walitawala kwa utaratibu maalumu. Hiyo ni kwa sababu sisi hatukusudii isipokuwa kusoma sira ya viongozi wema maasumina ambao ni lazima kuwaiga ili mwanafunzi afuate nyayo zao, awafuate na kuongoka kwa uongozi wao na sira yao katika maisha yake binafsi na ya kijamii.

**Pili:** Mwanafunzi anaweza kupata mafunzo muhimu ya kihistoria kupitia njia ya kutoa hatua za maisha ya kila mmoja kati ya maasumina kumi na wanne kwa kiwango kinachonasibiana na hatua ya mwanzo ya utangulizi ambayo imeishia kugusia nafasi na sehemu ya

kizazi cha Mtume katika historia na harakati za Uislamu, kwa kuanzia nafasi yao maalumu ya kipekee aliyowapa Mwenyezi Mungu na kumalizia hali halisi ya kihistoria ambayo imetoa harakati zao na mwenendo wao muda wa karne tatu na zaidi.

**Tatu:** Kwanza hakika mafunzo ya historia ya Bara la Uarabu hayaingii yote katika historia ya Uislamu isipokuwa huwa kama utangulizi tu. Pili hutumiwa katika sehemu ya uchambuzi, jambo ambalo hatulikusudii katika hatua hii ya masomo haya. Zaidi ya hapo ni kuwa maelezo ya kizazi cha Mtume (s.a.w.w.) kama vile kauli za Imam Ali (a.s.) toka kwa Mtume (s.a.w.w.) na maelezo ya Zahra (a.s.) ndani ya hotuba yake mashuhuri aliyoitoa baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.) yameelezea vizuri hali ya waarabu kabla ya Uislamu. Na pia imeunganisha kati ya yaliyopita na yaliyopo ambayo aliyatimiza Mtume (s.a.w.w.), na majukumu makubwa yaliyofuatia yaliyopo juu ya waislamu ambao walitolewa na Uislamu toka kwenye shimo la ujinga mpaka kwenye nuru ya mwanga wa Uislamu.

**Nne:** Hakika anayemaliza kusoma kitabu hiki inampasa azalishe mafunzo ambayo yatampa njia ya kufikia malengo yanayokusudiwa katika kusoma historia ndani ya hatua zote mbili, na wala asitosheke na haya yaliyopo kwenye masomo ya hatua ya utangulizi.

Hatutaki kurudia mafunzo mara juu juu au mara nyingine kwa upana na undani zaidi, kwa ajili hiyo tunategemea waheshimiwa walimu wetu watazingatia malengo ya masomo kabla ya kuhoji silabasi ya kitabu. Na watatilia maanani silabasi ya kitabu kabla ya kuzama ndani ya vipengele vidogo vidogo vya historia ambavyo tumeviteua kwa ajili ya hatua hii. Pia watazingatia kikomo cha wakati na dharura ya kupangilia mafunzo kulingana na ubora ambao ni lazima kuzingatiwa katika silabasi ya mafunzo. Na kwa kuwa hiki si kitabu cha ziada bali kimeandaliwa kama kitabu cha kiada basi walimu watafundisha

kulingana na silabasi ya mafunzo iliyopangwa.

Hatuna budi kusema kuwa kitabu hiki kilichapishwa mwanzo kwa jina la: '**Dondoo za sira za viongozi wema**'. Lakini baada ya kupitia upya mafunzo ya kitabu, kilibadilishwa jina na kuitwa: **'Masomo ya utangulizi katika historia na sira ya viongozi wema'.**

Mwisho tunatoa shukurani za dhati kwa ndugu zetu kamati ya elimu katika taasisi ya kimataifa inayosimamia vituo vya elimu na shule za kiislamu kwa msaada na juhudi walizozitoa.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe uongofu na nguvu, hakika Yeye ndiye kiongozi bora na Mwenye kunusuru. Pia tunatoa shukuranu za dhati kwa mwandishi wa kitabu hiki Ustadh Sayyid Mundhir Al-Hakim (heshima yake idumu).

**Jopo la kamati ya waandishi wa vitabu vya kiada.**
**1425 A.H.**

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 1

بسم الله الرحمن الرحيم

# Somo la Kwanza

## Hatua ya mwanzo kuelekea kwenye masomo ya sira na historia ya Uislamu

Kwanza: Sira na lengo la kuisoma.

### 1- **Sira kiistilahi:**

Sira ya mwanadamu ni njia yake na mwenendo wake katika maisha, hivyo sira ya Mtume na kizazi chake ni njia na mwenendo wao katika maisha. Sira hii inaonekana katika kauli zao, matendo yao na misimamo yao dhidi ya matukio na mambo mbalimbali ambayo yalitokea katika zama zao na wakaishi nayo kipindi cha karne tatu na miongo minne. Yaani tangu uanze utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mpaka mwisho wa ghaiba ndogo ya Imam wa kumi na mbili Muhammad bin Hasan Al-Askariy, Al-Mahdi hoja mwenye kungojewa.

### 2- **Jinsi Qur'ani ilivyotilia umuhimu sira:**

Hakika Qur'ani imetilia umuhimu sira kwa kubainisha sira ya manabii na watu wema. Ikataka tufuate sira yao na kujifunza kupitia sira ya wale waliopita huku tukiwaidhika na sira yao. Pia imetuhimiza kujali sira ya hitimisho la manabii na bwana wa mitume, Muhammad bin Abdullah (s.a.w.w.) ikataka tumuige[3] baada ya kumwambia: **"Na kwa hakika wewe unaongoza kwenye njia iliyonyooka."[4]**

3 **Al-Ahzab: 21**.
4 **As-Shura: 52.**

Kisha akawaamrisha waislamu wote kukazania yote yanayotoka kwa yule asiyetamka la matamanio yake akasema: **"Na anachokupeni Mtume basi kipokeeni, na anachokukatazeni basi jiepusheni."**[5] Kisha akatuelekeza kwa kizazi cha Mtume, ambao Mwenyezi Mungu kawaondolea uchafu na kuwatakasa kabisa[6]. Akahimiza kushikamana na wakweli na kufuata mwenendo wao, hivyo Mwenyezi Mungu akasema: **"Enyi mlioamini, mcheni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli."**[7]

## 3 - Lengo la kusoma sira:

Hakika kumfuata Mtume wa Mwenyezi Mungu na kizazi chake kitakasifu ni kufuata njia iliyonyooka inayofikisha kwenye wema na ushindi kwa sababu ni njia inayokuepusha na upotovu na ghadhabu za Mwenyezi Mungu. Na ndio njia ya manabii ambao Mwenyezi Mungu aliwaneemesha kwa neema ya uongofu wake unaowapeleka kwenye haki[8]. Ndiyo maana akaamrisha kuwafuata, Mwenyezi Mungu akasema: **"Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewaongoza, basi fuata mwongozo wao."**[9]

Pia kwa ajili hiyo ndiyo maana sira ya yule hitimisho la manabii na sira ya mawasii wake watakasifu imekuwa ni chanzo kati ya vyanzo vya sheria ya kiislamu, na ni chemchemu ya maarifa na elimu ya kiislamu na ni sawa na Kitabu cha Mwenyezi Mungu cha milele, kama ilivyoelezea kuhusu hilo Hadithi ya vizito viwili iliyo *mutawatir*.[10]

---

5 **Al-Hashri: 7.**
6 **Al-Ahzab: 33.**
7 **At-Tawba: 119.**
8 **Al-Fatiha: 5 – 7.**
9 **Al-An'aam: 90.**
10 Rejea Hadithi hiyo kwenye somo la saba.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 4



Zaidi ya hapo ni kuwa sira yao - Amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote kwa ujumla - ina faida kubwa katika kufahamu makusudio ya Kitabu kitakatifu na tafsiri ya Aya zake tukufu. Pia sira yao hutubainishia jinsi ya kutekeleza mafunzo ya juu ya kiislamu katika maisha ya mwanadamu anayeishi katika maisha haya. Kwa hiyo tunafahamu kuwa kusoma sira yao kwa namna sahihi kutatupa silabasi muhimu katika malezi ya kiislamu na njia sahihi ya kujifunza mwenendo sahihi katika maisha.

## Pili: Mahusiano kati ya historia ya Uislamu na sira

**Historia:**

Historia ni mkusanyiko wa matukio na uzoefu wa wanadamu waliopita ukilinganisha na zama tunazoishi hivi sasa.

**Historia ya Uislamu:**

Hakika historia ya Uislamu ni historia ya dini ya milele ya kiislamu, tangu ulipodhihiri, kuenea kwake na harakati zake katika maisha. Pia inakusanya historia ya walioibeba dini na kuihami ambao walikesha wakihudumia na kulinda dini dhidi ya vitimbi vya maadui wake. Hivyo hakika sira ya bwana wa mitume na sira ya kizazi chake kitakasifu ambacho kilipewa jukumu la kufikisha dini, kutekeleza na kuilinda, inakuwa ni sehemu isiyogawika ndani ya historia yenyewe ya Uislamu (yaani ndio historia yenyewe ya Uislamu).

Kwa sababu wao walizama ndani ya Uislamu na wakaihami sheria, wakatoa nafsi zao na maisha yao kwa ajili ya Uislamu. Hivyo misimamo yao ya kidini ndio Uislamu wenyewe na harakati zao ndio harakati za Uislamu wenyewe. Wao hudhihirisha kimatendo mafunzo halisi ya Uislamu na huyaelezea maelezo halisi. Hivyo historia yao

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 5



ndio historia ya Uislamu katika hatua zake zote na mambo yake yote, wala siyo historia ya mtu fulani kati ya waislamu.

## Vyavzo vya historia ya Uislamu na sira ya Mtume (s.a.w.w.)

Hakika chanzo muhimu cha historia ya Uislamu na historia na sira ya manabii hasa historia na sira ya nabii wa mwisho (s.a.w.w.) ni Kitabu cha milele cha Mwenyezi Mungu, Qur'ani yake ya muujiza ambayo: **"Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake, kimeteremshwa na Mwenye hekima, Mwenye kuhimidiwa."[11]**

Ama vitabu vya sira, historia, tafsiri na Hadithi ambavyo viliandikwa baada ya kupita karne moja au zaidi tangu kufariki kwa Mtume (s.a.w.w.) vyenyewe ni vyanzo vya daraja la pili. Hakika vyanzo hivi vilivyokuja nyuma vimejumuisha ukweli huku pembeni yake vikiwa vimejaza visa vya uongo, Hadithi na habari za uzushi zilizowekwa kupitia ndimi za maswahaba au wanafunzi wa maswahaba.

Kwa ajili hiyo vyanzo hivi vinahitajia kipimo makini ili kupembua habari sahihi na kuzitenganisha na habari zilizochomekwa. Pia inatakiwa kuzipima na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna sahihi ya Mtume na akili salama ili ziwe ni mwongozo kwa watafuta ukweli.

## Zama za historia ya Uislamu

Historia ya Uislamu inaanzia pale alipopewa utume Mtukufu Mtume, tarehe ishirini na saba mfungo kumi (Rajabu) miaka kumi na tatu kabla ya hijra ya Mtume (s.a.w.w.), muda ambao maisha ya Uislamu wa kudumu yalianza na yakaendelea kuchanja mbuga ndani ya jamii

11 **Fusilat: 42.**

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 6



ya kiarabu na mwanadamu chini ya mkono wa Mtukufu Mtume Muhammad bin Abdullah.

Uislamu ulikuwa ni mapinduzi ya Mwenyezi Mungu yenye mabadiliko katika kila kitu, hivyo yalianzia Makka tukufu na kuishia kwenye kuasisi dola ya kiislamu iliyobarikiwa huko Madina na Bara la Arabu. Baada ya jihadi kubwa chini ya uongozi wa Mwenyezi Mungu Mwenye busara matunda yake yalionekana ndani ya muda mfupi, kinyume na historia nyingi za wito wa mabadiliko. Zama hizi ambazo Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alianzisha mapinduzi haya yaliyobarikiwa tunaweza kuziita ni zama za Mtume Muhammad (s.a.w.w.), nazo ni zama za kufikisha Uislamu.

Ama zama zilizofuatia zenyewe ni zama za mawasii waliousiwa mapinduzi na dola ya Mtume. Hizi tunaweza kuziita zama za Maimam maasumina au zama za Maimam viongozi wema. Zama zote mbili zinagawanyika katika vipindi na nyakati mbili.

a) **Zama za Mtume (s.a.w.w.)**

Zama za Nabii zina vipindi viwili tofauti navyo ni: Kipindi cha Makka na kipindi cha Madina. Kipindi cha kwanza kinaanzia pale aliporuhusiwa kutangaza utume huko Makka na kinakomea pale alipohama toka Makka kuelekea Madina (Yathirib) katika usiku wa mwanzo wa mfunguo sita mwaka wa kumi na tatu tangu kupewa utume.

Kipindi cha pili kinaanzia pale alipofika Madina tarehe kumi na mbili ya mfungo sita ndani ya mwaka huo huo, na kinakomea pale alipofariki Mtume (s.a.w.w.) tarehe ishirini na nane mfunguo tano mwaka wa kumi na moja tangu kuhamia Madina.

Katika kipindi cha Makka Mtume alitengeneza nguvu kali, alijenga

Uislamu kiimani na kisheria kwa ajili ya maisha, hivyo ni kipindi cha kutengeneza umma wa kiislamu na kuanzisha kundi la waumini wenye kuamini Uislamu.

Ama kipindi cha Madina kinajitofautisha kwa kuasisiwa dola ya kiislamu, nayo ndiyo jengo la kwanza la kisiasa lenye sura ya dola ya kiislamu iliyojengeka katika kutekeleza sheria ya kiislamu ndani ya maisha. Katika vipindi vyote viwili wahyi wa Mwenyezi Mungu ndiyo uliokuwa ukimuelekeza yeye Mtume kama kiongozi wa umma wa kiislamu kupitia Aya za Qur'ani ambayo iliteremka ndani ya muda wa miaka ishirina na tatu. Qur'ani imetuhifadhia matukio ya vipindi vyote viwili kupitia Aya zake. Hivyo tunaweza kuijua historia ya zama hizi iwapo tu tutajua kwa usahihi utaratibu wa kushuka Aya za Qur'ani tukufu. Hivyo tunaweza kugawa kipindi cha Makka katika vipindi viwili vifuatavyo:
Kipindi cha kuwalingania watu mahsusi na kuandaa mbegu za mwanzo za kundi la waumini. Muda wa kipindi hiki unakadiriwa ni miaka mitatu mpaka mitano.

Kipindi cha kuwalingania watu wote au kipindi cha kutangaza na kuanza mapambano dhidi ya shirki na ukafiri. Muda wa kipindi hiki unakadiriwa ni miaka mitatu mpaka minne.

Kipindi cha uhamishoni, nacho ni kipindi cha kuendeleza mkondo wa Uislamu. Kipindi hiki kimekusanya hijra tatu zenye kufuatana nazo ni: Kuhama kuelekea Uhabeshi (Ethiopia ya sasa), kisha kuelekea Taif na kisha kuelekea Madina.

Pia tunaweza kugawa kipindi cha Madina katika vipindi viwili tofauti navyo ni:
Kipindi cha kuasisiwa dola ya kiislamu na kuihami ndani ya nusu ya kwanza ya kipindi cha Madina kuanzia hijra na kumalizikia vita vya

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 8



Handaki au Ahzab.

Kipindi cha ufunguzi na kuendeleza mapinduzi ya kiislamu na kupanua wigo wa dola ya kiislamu. Hii ni kuanzia suluhu ya Hudaybiya mpaka mwaka wa Hijja ya mwisho ya kuaga, nayo ni nusu ya pili ya kipindi cha Madina.

b): **Zama za Maimam wema**

Hakika harakati za mageuzi ziliienea jamii ya kijahiliya hivyo kutokana na zilivyokuwa fikra, mafunzo, mila, na desturi za kijahiliya ni kuwa mapinduzi ya kiislamu na dola mpya ya Mtume (s.a.w.w.) vilikuwa vinahitajia usia wa kiitikadi. Hiyo ni kwa sababu njia mbele ya harakati ilikuwa bado ndefu huku ikiendela kipindi chote cha vita nzito vya kiroho kati ya Uislamu na ujahiliya.

Kipindi kilichochukuliwa na mapinduzi, kisha dola ya Mtume hakikuwa kinatosha kung'oa mizizi yote ya ujahiliya na athari zake. Na hilo ni kama ilivyothibitisha historia ya matukio ambayo yalitokea baada tu ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.). Kwani baada ya Mtume (s.a.w.w.) utawala wa kiislamu ulibakia ni mpira unaochezewa na watoto wa kizazi cha Umayya ambao kabla ya hapo walikuwa wamesimama kidete dhidi ya Uislamu kuanzia mwanzo mpaka sekunde ya mwisho.[12]

Kuanzia hapo Mtume kiongozi aliainisha Maimam kumi na wawili maasumina kwa amri toka kwa Mwenyezi Mungu. Ambao ni mawasii wenye uwezo watakaoshika nafasi yake ili kulinda mapinduzi yake,

12 -Kwa ufafanuzi zaidi rejea kitabu *Nash'atutashayyu wa Shia* cha Shahid Sayyid Muhammad Baqir As-Sadri, uhakiki wa Dr. Abdul-Jabar Shararah, Uk. 51 – 57 na 58 – 61.

ujumbe wake, umma wake, na dola yake baada yake. Hivyo baada yake walisimamia jukumu la kutetea sheria ya Mwenyezi Mungu na dola ya bwana wa mitume na umma wa hitimisho la manabii.

Zama zao zimegawanyika katika vipindi viwili tofauti navyo ni: Kipindi cha kuonekana na kipindi cha ghaibu. Kipindi cha kuonekana kinaanzia pale alipofariki Mtume (s.a.w.w.) na kinakomea mwaka 260 A.H. Pale alipofariki Imam wa kumi na moja kati yao naye ni Hasan Al-Askariy.

Ama kipindi cha ghaibu ni kipindi cha kutoonekana Imam wa kumi na mbili kati yao naye ni maasumu wa kumi na wane. Hujja bin Al-Hasan Al-Mahdi (a.s.) mwenye kungojewa. Ambaye uimamu wake umefungana na ghaibu yake.

Kipindi cha Ghaibu nacho kina vipindi viwili:

Cha kwanza: Kipindi cha ghaibu fupi ambacho kilifikia muda wa miongo saba. Yaani kuanzia mwaka 260 mpaka 329 A.H.

Cha pili: Kipindi cha ghaibu ndefu ambacho kilifuata baada ya fupi ikiwa ni mwishoni mwa muongo wa tatu karne ya nne baada ya kufariki balozi wake wa nne mwaka 329 A.H. Nacho kinaendelea mpaka leo.

**Muhtasari:**

Sira ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na sira ya kizazi chake kitakasifu ni chanzo muhimu kati ya vyanzo vya maarifa na sheria ya kiislamu. Huzingatiwa pia kuwa ni nyenzo kati ya nyenzo za kufikia wema na mafanikio, kwa sababu kuwafuata wao ni mfano halisi wa kufuata njia ya Mwenyezi Mungu iliyonyooka.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 10



Historia ya kiislamu ndio historia ya Uislamu na ndio historia ya watetezi ambao walizama ndani na kujitoa muhanga kila dakika ya maisha yao katika njia ya Uislamu. Nao ni Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kizazi chake kitakasifu kilichotakasika dhidi ya kila aina ya uchafu na kila aina ya dosari.

Qur'ani ndio chanzo muhimu cha historia na sira ya Mtume (s.a.w.w.) na historia ya kiislamu. Kwa ajili hiyo vyanzo vyote vingine vya sira na historia vinapimwa kwa Qur'ani, kwa sababu vyanzo vingine vimekosa sifa ya "kumdiriki Mtume (s.a.w.w.)", "kudiriki yote, umakini, na kutoegemea" kwenye maslahi ya makundi na madhehebu ambayo yalizuka baada ya zama za Mtume (s.a.w.w.). Zama za Mtume wa mwisho (s.a.w.w.) huchukuliwa kama mwanzo wa zama za historia ya kiislamu kisha hufuatiwa na zama za Maimam wema (a.s.).

**Maswali:**

1. Elezea maana ya sira ya Mtume na sira ya kizazi chake kitakasifu.
2. Bainisha msimamo wa Qur'ani kuhusu sira na kujifunza kwake.
3. Elezea malengo na faida itokanayo na kujifunza sira ya Mtume (s.a.w.w.) na kizazi
   chake.
4. Ni upi uhusiano uliyopo kati ya sira ya Mtume (s.a.w.w.) na historia ya kiislamu?
5 . Ni vipi vyanzo vya sira na historia ya kiislamu?
6. Ni zipi sifa za kipekee za Qur'ani zinazoifanya iwe ni chanzo cha sira na historia ya Uislamu?
7: Orodhesha zama za historia ya kiislamu?

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 11



# Somo la Pili

## Muhammad bin Abdullah (s.a.w.w.) ni utabiri wa manabii (a.s.)

### Mwenendo wa utabiri:

Ni mwenendo wa Mwenyezi Mungu na ni rehema na amani kutoka Kwake kuwapa habari waja Wake za kuja kwa Mtume atakayemtuma kwao muda ujao. Hivyo manabii waliotangulia walikuwa wakimbashiri Nabii atakayekuja baada yao.

Qur'ani imeashiria jinsi Yahya alivyobashiri unabii wa Isa (**Al Imran: 39**). Pia imeashiria jinsi Isa alivyobashiri unabii wa Muhammad (**As-Swaf: 6**). Hivyo manabii wote msitari wao ni mmoja kwani aliyetangulia humbashiri atakayemfuata, na huyu aliyefuata humwamini aliyetangulia**.** Mwenendo huu wa kubashiri umetamkwa na Qur'ani katika Sura ya tatu Aya ya themanini na moja. Zaidi ya hapo ni ushahidi na mifano halisi utakayoiona hapa mbele:

1**.** Qur'ani imeelezea utabiri wa Ibrahim kipenzi juu ya utume wa Nabii wa mwisho kwa ulimi wa dua akisema:

﴿ رَبَّنَا وَٱبۡعَثۡ فِيهِمۡ رَسُولاً مِّنۡهُمۡ يَتۡلُواْ عَلَيۡهِمۡ ءَايَـٰتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلۡكِتَـٰبَ
وَٱلۡحِكۡمَةَ وَيُزَكِّيهِمۡ ۚ إِنَّكَ أَنتَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾ ﴾

**"Ewe Mola wetu, wapelekee mtume katika wao awasomee Aya zako na kuwafunza kitabu na hekima na kuwatakasa. Hakika wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima." (Al-Baqarah: 129)**
Qur'ani imeeleza wazi kuwa utabiri wa Nabii Muhammad ulikuwe-

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 12



mo ndani ya vitabu viwili: Taurati na Injili, na laiti kama utabiri huo usingekuwemo ndani ya vitabu hivyo basi watu wa vitabu hivyo wangeupinga waziwazi, Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِىَّ ٱلْأُمِّىَّ ٱلَّذِى يَجِدُونَهُۥ مَكْتُوبًا عِندَهُمْ
فِى ٱلتَّوْرَىٰةِ وَٱلْإِنجِيلِ يَأْمُرُهُم بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَىٰهُمْ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَيُحِلُّ
لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ ٱلْخَبَٰٓئِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَٱلْأَغْلَٰلَ
ٱلَّتِى كَانَتْ عَلَيْهِمْ ۚ ﴿١٥٧﴾ ﴾

**"Ambao wanamfuata mtume, nabii aliyeko Makka ambaye wanamuona ameandikwa kwao katika Taurati na Injili, ambaye anawaamrisha mema na anawakataza yaliyo mabaya, na kuwahalalishia vizuri na kuwaharamishia maovu, na kuwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao." (Al-A'araf: 157)**

Aya ya sita ya Surat Swaffu imeelezea waziwazi kuwa Isa (a.s.) alisadikisha Taurati na akambashiri Mtume atakayekuja baada yake jina lake Ahmad. Kama inavyoashiria kauli ya Mwenyezi Mungu:

﴿ وَإِذْ قَالَ عِيسَى ٱبْنُ مَرْيَمَ يَٰبَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ إِنِّى رَسُولُ ٱللَّهِ إِلَيْكُم مُّصَدِّقًا
لِّمَا بَيْنَ يَدَىَّ مِنَ ٱلتَّوْرَىٰةِ وَمُبَشِّرًۢا بِرَسُولٍ يَأْتِى مِنۢ بَعْدِى ٱسْمُهُۥٓ أَحْمَدُ ۖ
فَلَمَّا جَآءَهُم بِٱلْبَيِّنَٰتِ قَالُوا۟ هَٰذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٦﴾ ﴾

**"Na aliposema Isa bin Mariam: Enyi wana wa Israeli, hakika mimi ni mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu. Nimethibitisha yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na ni mwenye kutoa habari njema ya mtume atakayekuja baada yangu, jina lake ni**

**Ahmad, lakini alipowaletea hoja zilizo wazi, walisema: Huu ni uchawi ulio dhahiri”** (**As-Swaff: 6**).

## Ahlul-Kitab wamngojea Nabii wa mwisho:

Manabii waliyotangulia hawakuishia tu kutoa sifa kuu za nabii aliyetabiriwa, bali zaidi ya hapo walitaja baadhi ya alama ambazo wale wanaopewa utabiri wanaweza kumjua vizuri. Alama hizo ni kama vile sehemu atakayozaliwa, atakayohamia na sifa mahsusi za wakati atakaopewa utume. Pia alama za kipekee alizonazo mwilini, tabia na sheria zake za kipekee. Bali Qur’ani imeeleza kuwa walikuwa wanamjua kama wanavyowajua watoto zao (**Al-An’am: 20**).

Kutokana na utabiri huo wakafuatilia kivitendo na mwisho wakagundua sehemu atakayohamia na kusimamisha dola yake. Hapo wakafanya makazi yao na kuanza kuiombea nusra dini yake dhidi ya makafiri (**Al-Baqarah: 89**), na kuomba ushindi kupitia Mtume wa Mwenyezi Mungu dhidi ya Ausi na Khazraji.

Hivyo habari hizi zikaenea kwa wengine kupitia mapadri na wasomi wao, zikazagaa Madina zikafika hadi Makka. Wakampa habari Abdul Muttalib[13] na Abu Talib[14] huku wakiwahadharisha na vitimbi vya mayahudi. Hivyo baada ya Mtume kutangaza utume wake, ujumbe wa makuraishi ulikwenda kwa mayahudi wa Madina kwa lengo la kuthibitisha ukweli wa madai ya unabii waliousikia toka kwa Muhammad, wakachukua baadhi ya mambo waliyomtahini nayo Mtume,[15] na hatimaye ukabainika ukweli wa madai yake.

13 *Tarikh Al-Yaaqubiy*, Juz. 2, uk. 12.

14 *Siiratu Ibnu Hisham*, Juz. 1, uk. 181, na *Ilamul-Waraa*, uk. 26.

15 Rejea sababu ya kuteremka **Surat Kahfi**.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 14



Baadhi ya Ahlul-Kitabi na wengineo walimwamini Nabii Muhammad kwa kufuata alama hizi ambazo walizifahamu hata bila ya kumuomba muujiza wowote mahsusi (**Al-Maidah: 83**). Mpaka leo baadhi ya nakala za Taurati na Injili zimehifadhi baadhi ya utabiri huo.[16] Na hivyo ndivyo ulivyofuatana utabiri wa unabii wa nabii wa mwisho Muhammad kabla ya kuzaliwa kwake**.** Kisha ukanukuliwa wakati wa uhai wake kabla ya kukabidhiwa unabii. Ulienea utabiri aliouelezea padri Buhayra kisha ushahidi wa Waraqa bin Nawfal juu ya utume wa Muhammad, ushahidi uliotokana na utabiri.[17]

Imam Ali (a.s.) ameelezea hali hiyo kwa kusema: "Mwenyezi Mungu hajawaacha viumbe wake bila ya nabii aliyetumwa au kitabu kilichoteremshwa, au hoja ya lazima, au njia ya wazi iliyonyooka. Mitume ambao uchache wa idadi yao au wingi wa wapingaji havikumzuwia aliyetangulia kumtaja atakayekuja baada yake, au aliyepita kutambulishwa na aliye kabla yake.

Kwa mwenendo huo karne zikapita……… Mpaka Mwenyezi Mungu alipomleta Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu ili kutekeleza utaratibu Wake na kutimiza unabii wake, huku ahadi yake ikiwa imechukuliwa kwa manabii waliyotangulia na alama zake zikiwa ni mashuhuri……..”[6]

---

16 *Ashia'tul-Baytun-Nabawiyyi*, Juz. 1, uk. 70, humo amenukuu kutoka kwenye Taurati. Pia rejea *Siratur-Rasulu wa Ahlul-Baytihi*, Juz. 1, uk. 39 humo amenukuu baadhi ya tabiri kutoka kwenye Injili ya Yohana.

17 Katika vitabu vikubwa vya Siira.

6 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya kwanza.

### Sifa za Nabii Muhammad (s.a.w.w.):

Ibnu Saad amepokea toka kwa Sahlu mtumwa wa Utayba ambaye alikuwa mkiristo wa Mar'yasi na alikuwa ni yatima aliyelelewa na mama yake mzazi na ami yake, pia alikuwa msomaji wa Injili, alisema kuwa: "Nikachukua kitabu cha ami yangu nikawa nakisoma mpaka iliponipita karatasi, hivyo nikataka kujua ni kipi kilichoandikwa katika karatasi iliyonipita. Nikaigusa kwa mkono wangu na pindi nilipoangalia nikakuta vitini vya karatasi vimeshikana hapo nikaviachanisha nikakuta ndani yake sifa za Muhammad:

"Yeye si mfupi, si mrefu, mweupe, kati ya mabega yake kuna muhuri, mara nyingi hukaa mkao wa ihtibau, hapokei sadaka, anapanda punda na ngamia, anakamua mbuzi, anavaa kanzu chakavu, na atakayefanya hivyo basi kajiepusha na kiburi na yeye hufanya hivyo, na yeye anatokana na kizazi cha Ismail na jina lake ni Ahmad."

Sahlu akasema: "Nilipofika hapa katika kumtaja Muhammad ami yangu akaja na alipoiona karatasi alinipiga na kusema: "Kwa nini umefungua karatasi hii na kusoma?" Nikasema: Humu mna sifa za nabii Ahmad. Akasema: "Yeye bado hajakuja."[18]

## Muhtasari:

Matukio ya kihistoria yanaonyesha kuwa mwenendo wa manabii ni wa kiukamilifu wenye lengo moja na njia moja. Pia mwenendo wa Mwenyezi Mungu ni manabii waliyopo kuwabashiri watakaochukua nafasi zao katika unabii. Ikiwa ni huruma toka kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya mzigo walio nao wanadamu katika kuamini na kukubali na ni kumrahisishia nabii anayefuata kazi ya uhubiri na ulinganio.

18 *At-Tabaqatu Al-Kubra,* Juz. 1, uk. 363.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 16



Na kwa kuwa Uislamu na Mtume Muhammad vina umuhimu mkubwa katika historia ya binadamu, na ukizingatia kuwa Uislamu ni dini inayohusu kila kitu na ndiyo dini ya mwisho huku Mtume (s.a.w.w.) akiwa ndiyo mtume wa mwisho, basi Uislamu huo ulibashiriwa tangu zamani na hilo limeelezwa na Qur'ani tukufu.

Kuna habari zilizoenea kabla ya Mtume kukabidhiwa utume ambazo zilikuwa zimebeba wasifu kamili wa Mtume Muhammadin (s.a.w.w.) na mazingira yake, zikiwataka watu wamwamini na wajiepushe na upotovu kwa kumfuata yeye.

Habari hizi zilisaidia baadhi ya Ahlul-Kitabu na wengineo kuamini dini ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) bila ya kuomba muujiza wowote mahsusi.

## Maswali:

1: Ni upi umuhimu wa bishara za manabii?

2: Je, kuna utabiri mahsusi toka kwa manabii waliyotangulia unaomhusu nabii Muhammad?

3: Toa Aya kuthibitisha utabiri huo?

4: Ni kitu gani walichokifahamu Ahlul-Kitabi kuhusu Nabii (s.a.w.w.) kabla ya utume wake?

5: Ni upi ulikuwa msimamo wa Ahlul-Kitabu dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) baada ya kupewa utume?

# Somo la Tatu

## Mazingira safi

Mazingira yana mchango mkubwa katika malezi ya mwanadamu, humfanya awe mwema au humharibu. Mazingira tunayokusudia hapa ni wale watu wanaomzunguka mwanadamu ambao mwanadamu huyu hupokea kutoka kwao misingi ya maarifa yake na lugha yake. Wanadamu ambao kupitia kwao hujifunza elimu na maarifa mbalimbali na huongoka kupitia kwao, kwani huathirika kulingana na wanadamu wanaomzunguka, hivyo yeye huwaathiri na wao humwathiri.

Familia ndio mazingira ya mwanzo ambayo wanadamu hukulia ndani yake wakiwemo manabii na walinganiaji wa tawhidi ambao walisimama kidete kupiga vita shirki, maadili machafu na mila potovu. Hakika Mwenyezi Mungu aliwaumba na kuwalea katika familia za tauhidi zenye kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu. Baba wa manabii Adam (a.s.) ndiye aliyefundishwa majina yote na Mwenyezi Mungu kabla hajaletwa aridhini. Na yeye ndiye wa kwanza kumtakasa Mwenyezi Mungu na ndiye wa kwanza aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu katika tauhidi. Hivyo kwa mwenendo huo wakafuata manabii wote, manabii ambao wamehitimishwa na Muhammad (s.a.w.w.).

### Mazingira ya Mtume (s.a.w.w.) kwa mujibu wa maelezo ya Ahlul-Bayt

Imam Ali (a.s.) ameelezea mazingira ya tauhidi ambayo Mtume (s.a.w.w.) alitokana nayo akasema: “Akamteua kutokana na mti wa manabii, shubaka yenye mwanga, nywele za utosi wa watukufu na

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 18



kitovu cha Makka"[19] "….Mahala pake alipoishi (Mfuko wa uzazi) ndiyo mahala bora, na chimbuko lake ndio chimbuko bora katika machimbuko ya madini ya utukufu na busati la amani."[20]

"Hivyo akamleta toka ndani ya madini yenye chimbuko bora na asili tukufu, toka ndani ya mti ambao alikusudia kuwatoa ndani yake manabii na kuteua waaminifu wake kutoka humo."[21] "Kila Mwenyezi Mungu alipokiongeza kizazi kwa kugawa makundi mawili basi alikiweka kizazi chake katika kundi bora, kundi ambalo mzinifu hakuchangia chochote wala hakupata fungu lolote."[22]

Pindi Qur'ani ilipotaja kuteuliwa kwa ajili ya ulimwengu wote Adam, Nuh, kizazi cha Ibrahim na kizazi cha Imran Mwenyezi Mungu aliendelea kwa kusema:

﴿ ذُرِّيَّةً بَعْضُهَا مِنْ بَعْضٍ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٣٤﴾ ﴾

"**Kizazi cha wao kwa wao na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua"** (**Al Imrani: 34**).

Akamtaja kipekee mtume wake wa mwisho kwa kusema:

﴿ وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ﴿٢١٧﴾ الَّذِي يَرَاكَ حِينَ تَقُومُ ﴿٢١٨﴾
وَتَقَلُّبَكَ فِي السَّاجِدِينَ ﴿٢١٩﴾ ﴾

**"Na umtegemee Mwenye nguvu, Mwenye rehema. Ambaye anakuona unaposimama. Na mageuko yako katika wale wanaosujudu** (**Shu'araa: 217-219**)."

19 *Nahjul-Balagha*h, hotuba ya 161.
20 *Nahjul-Balaghah* hotuba ya 98.
21 *Nahjul-Balaghah* hotuba ya 94.
22 *Nahjul-Balaghah* hotuba ya 214.

Hivyo wote waliomtangulia Muhammad walikuwa wakisujudu na kunyenyekea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na wala hawajamshirikisha na chochote hata sekunde moja. Imam Jafar As-Swadiq (a.s.) amefafanua geuko hili kwa kusema: "Ndani ya mifupa ya migongo ya manabii kulikuwa na nabii baada ya nabii mpaka akamleta toka mifupa ya mgongo wa baba yake kutokana na ndoa na wala si kwa uzinzi, hali hii ni tokea kwa Adam."[23]

Nabii mwenyewe (s.a.w.w.) kaelezea hali hiyo waziwazi kwa kusema: "Nilihamishwa toka ndani ya mifupa ya migongo mitakasifu mpaka kwenye kizazi kitakasifu katika hali ya ndoa wala si hali ya uzinzi."[24]

Pia akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu alimteua Ibrahim toka kizazi cha Adam akamfanya kipenzi. Akamteua Isma'il toka kizazi cha Ibrahim. Kisha akamteua Nazari toka kizazi cha Isma'il. Kisha akamteua Mudhira toka kizazi cha Nazari. Kisha akamteua Kinana toka kizazi cha Mudhar. Kisha akamteua Qurayshi toka kizazi cha Kinana. Kisha akateua kizazi cha Hashim toka kizazi cha Qurayshi. Kisha akateua kizazi cha Abdul Muttalib toka kizazi cha Hashim. Kisha akaniteua mimi toka kizazi cha Abdul Muttalib."[25]

## Mazingira ya Mtume (s.a.w.w.) kwa mujibu wa maelezo ya wanahistoria.

Wanahistoria wameeleza wazi kuwa Abdul Muttalib alikataa kuabudu masanamu. Akampwekesha Mwenyezi Mungu, akatekeleza nadhiri. Akaanzisha mienendo ambayo mingi kati ya hiyo imetajwa na Qur'ani huku ikiridhiwa na Mtume (s.a.w.w.) kupitia sunna yake.

23 *Fadhailul-Khamsa mina Sahihi Sita*, Juz. 1, uk. 9.
24 *Fadhailul-khamsa mina Sahihi sita*, Juz. 1, uk. 9.
25 *Dhakhairul-U'quba*, uk. 10, na *Sahih Muslim*, Juz. 4, uk. 461.

Kati ya mienendo hiyo ni kutimiza nadhiri, fidia ya ngamia mia moja, kutooa maharimu na kutoyaendea majumba kwa nyuma. Pia kukata mkono wa mwizi, kukataza kuwauwa watoto wa kike, maapizano, kuharamisha pombe, kuharamisha zinaa na kutoa adhabu kwa mzinifu. Kuteua kwa bahati, kukataza kutufu uchi, kumkirimu mgeni, kutokutoa kitu wanapohiji isipokuwa toka kwenye mali waipendayo na kutukuza miezi mitukufu.

Walipokuja watu wa tembo maquraishi waliikimbia *Haram*, Abdul Muttalib akawaambia: **"**Naapa kwa Mwenyezi Mungu sitoki haramu natafuta ushindi kupitia njia nyingine." Maquraishi wakawa wakisema: "Abdul Muttalib ni Ibrahim wa pili.

Al-Masuudiy amesema: "Abdul Muttalib alikuwa akiwausia wanawe kuunga undugu, kulisha chakula na akiwatamanisha na kuwahofisha kufanya na kuaacha kitendo cha mtu anayetaraji siku ya Kiyama na ufufuo."[26]

Al-Shahrastaniy amesema: "Alikuwa akiwaamrisha wanawe waache dhuluma na ujeuri. Akiwahimiza juu ya maadili mema. Akiwakataza mambo duni. Katika usia wake alikuwa akisema: Hakika dhalimu hatotoka ndani ya dunia hii isipokuwa baada ya malipo ya kisasi na kufikiwa na adhabu." Hivyo alipofariki mtu mmoja dhalimu ambaye hakufikiwa na adhabu, watu wakaanza kumuuliza Abdul Muttalib kuhusu hilo. Akafikiri na kusema: Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika nyuma ya nyumba hii kuna nyumba nyingine ambayo ndani ya nyumba hiyo mwema hulipwa wema wake na muovu ataadhibiwa kwa uovu wake."[27]

26 *Muruju Dhahabi*, Juz. 2 uk. 103-108.
27 *Mausuatu Ta'rikh Al-Islamiyi* Juz. 1, uk., 244.

## Mtoto wa vichinjwa viwili:

Imam Ali Ridha (a.s.) aliulizwa kuhusu maana ya kauli ya Mtume : "Mimi ni mtoto wa vichinjwa viwili." Akajibu: "Hakika Abdul Muttalib alijining'iniza katika mlango wa Kaaba akamuomba Mwenyezi Mungu amruzuku watoto kumi. Akaweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu kuwa atamchinja mmoja kati ya hao iwapo tu Mwenyezi Mungu atajibu dua yake. Hivyo walipofika watoto kumi akasema: Hakika Mwenyezi Mungu kanitekelezea ombi langu, basi ni lazima nitekeleze nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Akawaingiza wanawe Kaaba na kuanza mchakato kati yao, na hatimaye mchakato huo ukaangukia kwa Abdullah baba wa Mtume (s.a.w.w.) na ndiye aliyekuwa kipenzi chake sana.

Akarudia mara ya pili mchakato huo ukaangukia tena kwa Abdullah. Akarudia kwa mara ya tatu mchakato ukaangukia kwa Abdullah. Ndipo alipomchukua na kuazimia kumchinja. Wakakusanyika maquraishi na kumkataza asifanye hivyo."[28]

Imam Al-Baqir (a.s.) amesema: "Mchakato ukaangukia kwa Abdullah. Akazidisha majina kumi lakini bado mchakato ukamwangukia Abdullah. Akaendelea kuzidisha majina kumi kumi mpaka yakafika mia moja ndipo mchakato ulipoangukia kwa ngamia. Hapo Abdul-Muttalib akasema: 'Sikumtendea haki Mola wangu,' hivyo akarudia mara tatu na mara zote ukaangukia kwa ngamia. Akasema: 'Sasa nimejua kuwa Mola Wangu kaniridhia.' Ndipo alipochinja ngamia.'"[29]

28 *Uyunu Akhbari Ridha* Juz. 1, uk. 212.
29 Al-Khisal, uk. 156.

## Amina binti Wahab:

Baada ya miaka kumi tangu kuchimbwa Zamzamu na baada ya mwaka mmoja[30] tangu Abdullah kufidiwa kwa ngamia Abdul Muttalib alitoka na mwanae Abdullah na kuenda nae katika nyumba ya Wahab bin Abdul Manafi bin Zahrat (wakati huo alikuwa ndio bwana wa kizazi cha Zahrah kinasaba na kisharaf). Hapo akamposa binti wa Wahabi, Amina kwa ajili ya Abdullah.

Amina alikuwa ndiye mwanamke bora kinasaba na kimaadili kwa maquraishi, hivyo Abdul Muttalib akamuozesha na kummilikisha Abdullah, Amina. Ndani ya nyumba ya Abdul Muttalib ndimo Abdullah alimomuingilia Amina na kupata ujauzito wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).[31]

Imam Ali (a.s.) amesema: "Amina binti Wahabi aliona usingizini kuwa anaambiwa: Hakika aliyomo tumboni mwako ni bwana, hivyo ukimzaa mwite Muhammad." Kisha Ali (a.s.) akasema: "Hivyo Mwenyezi Mungu alimpa jina kutoka ndani ya jina lake, kwani hakika Mwenyezi Mungu ni Mahmudu na huyu ni Muhammad."[32]

Hakika Abdullah alipata umashuhuri mkubwa akawa ni mtu muhimu kwa watu, akawa ndiyo mazungumzo yao na kipenzi chao. Baada ya tukio la kisa cha fidia yake, kisa ambacho kilifanana na kisa cha babu yake Isma'il…… Mwenyezi Mungu akamjalia kukutana na binti bora kati ya mabinti wa kiquraishi……lakini hakumjalia kuishi nae muda mrefu. Kwani utafutaji ulimpeleka Sham akiwa na maquraishi kwa ajili ya biashara. Alielekea Gaza huku akiwa amemuacha mke wake

30 *Tarikh Yaaqubiy*: Juz. 2 Uk. 9.

31 *Siratun-Nabawiyyah* ya Ibnu Hisham, Juz. 1, uk. 165.

32 *Al-Ihtijaj*, Juz. 1, uk. 321.

mja mzito, na alipokuwa akirudi alielekea Madina kwa lengo la kuwazuru wajomba zake na kuzidisha undugu, lakini mipango ya Mwenyezi Mungu haikumpa muda, hivyo akaugua huko na rafiki zake kulazimika kumwacha na kurudi huku wakiwa wamebeba habari za ugonjwa wake na kufikisha kwa baba yake Abdul Muttalib.

Abdul Muttalib akamtuma Al-Harithi ambaye ni mwanae mkubwa ili akamuuguze ndugu yake mpaka apone kisha arudi nae Makka. Isipokuwa mipango ya Mwenyezi Mungu ilikuwa ikimuharakisha Abdullah, hivyo Al-Harithi hakufika Madina isipokuwa baada ya siku nyingi tangu kufariki kwa ndugu yake.[33] Hivyo akarudi kwa baba yake akiwa na moyo wa huzuni, mwenye kutetemeka huku akibeba habari za kifo cha mtoto kipenzi kati ya watoto wa baba yake. Hakika ni habari nzito kwa Abdul Muttalib lakini hazikuteteresha subira yake wala hazikudhoofisha uvumilivu wake.

## Muhtasari:

Hakika Mwenyezi Mungu aliweka umuhimu maalumu kwa manabii wake, hivyo akawezesha wazaliwe toka ndani ya familia takasifu ili wawe na uwezo wa kuwasafisha watu dhidi ya shirki. Hivyo ndivyo alivyomteua nabii Muhammad (s.a.w.w.). Hakika alihama toka mifupa ya migongo mitakasifu yenye imani na toka mapaja ya utawa mpaka dunia ilipopata sharafu kwa kuzaliwa kwake.

Familia ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ilikuwa ni familia na damu yenye kuheshimika, kwani yeye ametokana na nabii Ibrahim (a.s.). Pia ilikuwa ikijihusisha na kulinda Haram ya Makka na kuitetea dhidi ya maadui.

33 *Biharul-Anwar*, Juz. 15 uk. 124. Tazama tafsiri ya **Surat Dhuha** kwenye kitabu *Majma'ul-Bayan* na *Al-Mizan Fidhilalil-Qur'ani.*

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 24



Babu wa Mtume Abdul Muttalib aliishi zama ambazo ujumbe wa Mwenyezi Mungu ulikuwa umetoweka huku nguvu za shirki zikiwa zimedhihiri na ufisadi na dhuluma vikishamiri, lakini pamoja na hayo yote alikuwa ni mwenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu huku akilingania maadili mema, na njia hiyo ndiyo waliyopita watoto wake.

Abdul Muttalib alimjali sana mwanae Abdullah, hivyo akamwozesha mwanamke bora toka familia na damu yenye heshima. Lakini matakwa ya Mwenyezi Mungu yalitaka Abdullah afariki kabla ya kuzaliwa mwanae Muhammad (s.a.w.w.).

## Maswali:

1. Elezea nafasi ya mazingira katika malezi ya mwanadamu?

2. Taja dalili inayothibitisha imani ya utohara wa wazazi wawili wa manabii?

3.Taja mifano halisi ya imani na tauhidi ya Abdul Muttalib babu wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.)?

4. Inamaanisha nini kauli ya Mtume (s.a.w.w.): “Mimi ni mtoto wa vichinjwa viwili”?

5. Kwa nini Mwenyezi Mungu huwateua manabii wake toka kwenye vizazi vitakasifu?

6. Kwa nini Abdul Muttalib aliazimia kumchinja mwanae Abdullah?

7. Elezea jinsi Abdullah alivyosalimika kuchinjwa?

# Somo la Nne

## Maisha ya Nabii wa mwisho

Hakika Mwenyezi Mungu alipenda asimamie malezi ya Muhammad (s.a.w.w.) amtoe mikononi mwa familia yake ili awe chini ya ulinzi wake ikiwa ni maandalizi ya kupata familia kubwa ambayo kiongozi wake atakuwa ni Muhammad. Familia ambayo haitopendelea taifa wala lugha au rangi bali mbora wao ndani ya familia hiyo ni yule tu mwenye uchamungu. Hivyo Qur'ani imeelekeza maana hii kwa kusema: **"Je hakukukuta ni yatima akakuhifadhi?" (Dhuha: 6).** Mtume akaelezea kwa kusema: "Hakika Mola wangu alinilea akaboresha maadili yangu."[34]

Hakika busara za Mwenyezi Mungu zilimnyima Muhammad (s.a.w.w.) mapenzi na huruma ya muda mfupi huku Mwenyezi Mungu akimpangia huruma na mapenzi ya muda mrefu usio na kikomo, kwani alimuhifadhi kwa babu yake kisha kwa ami yake, hivyo hao wawili wakawa wakimpendelea zaidi ya nafsi zao na zaidi ya watoto wao wa kuzaa. Katika njia hiyo ya malezi wakatoa kila aina ya mapenzi na huruma kwa kiwango ambacho wazazi hawawezi kujitolea kwa watoto wao wa kuzaa.

Hilo ni miongoni mwa fadhila za Mwenyezi Mungu kwa Mtume (s.a.w.w.) bali hakika alimfanyia umuhimu maalumu pindi alipojitolea mwenyewe kumlinda na kumuhami kwa huruma yake, na hakika hakuna neema kubwa kama hii ambayo kaielezea Mwenyezi Mungu kwa kusema: **"Na hakika fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yako ni kubwa."[35]**

34 *Mizanul-Hikma*, ameipokea kutoka kwenye kitabu *Nuru Thaqalayni* Juz. 5, Uk. 389.

35 An-Nisai: 133.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 26



## Kuzaliwa kwake: Zama, sehemu na namna:

Alizaliwa (s.a.w.w.) katika mji wa Makka ndani ya mwaka wa ndovu (tembo) mwezi wa mfungo sita. Kwa Shia Imamiya ni mashuhuri kuwa alizaliwa alfajiri ya siku ya ijumaa ya terehe kumi na saba. Kwa wengine mashuhuri ni kuwa alizaliwa siku ya jumatatu terehe kumi na mbili wakati wa kuchomoza alfajiri au jua au wakati wa kukengeuka jua.

Lililo mashuhuri toka kwa Amina binti Wahabi kama alivyoelezea Ibnu Is'haqa ni kuwa: "Wakati Amina alipokuwa akielezea siku za mimba ya Mtume (s.a.w.w.) alisema: Hakika Amina aliona nuru ikitoka mpaka akaona makasiri ya Basra kutokea ardhi ya Sham. Akaambiwa hakika wewe umembeba bwana wa umma huu, hivyo atakapotua aridhini sema: Namkinga kwa Mwenyezi Mungu mmoja dhidi ya shari ya kila hasidi, kisha mwite Muhammad."[36]

Halima binti Dhuaybu As-Saadiyyah ameongeza kuwa: "Amina alisema: 'Kisha naapa kwa Mwenyezi Mungu hakuna mimba niliyoona ni nyepesi kwangu na rahisi kama yake.'"[37]

Al-Yaaqubiy amesema: "Alipozaliwa Muhammad (s.a.w.w.) mashetani yalilaaniwa na nyota ziliporomoka, watu wakasema: Hakika hii ni alama ya Kiyama, watu wakapatwa na tetemeko la ardhi ambalo lilienea dunia nzima mpaka makanisa na mahekalu yakabomoka, na kikatoka sehemu yake kila kilichokuwa kikiabudiwa kinyume na Mwenyezi Mumgu. Mambo ya kichawi yakaharibika na mashetani wao wakafungwa, kasri la Kisra likatetemeka hivyo yakaporomoka masharafu kumi na tatu na moto wa Farsi ukazimika.

36 *As-Siratu An-Nabawiyyah* cha Ibnu Hisham, Juz. 1, Uk. 166.

37 *Mawsuuatut-Tarikh Al-Islamiyyah*, Juz 1, Uk 250, kutoka kwa Ibnu Saad.

Kabla ya hapo ulikuwa na muda wa miaka elfu bila kuzimika….

Mtu kati ya Ahlul-kitabi alikwenda kwa maquraishi akiwemo Hisham bin Al-Mughirah, Al-Walid bin Al-Mughirah na Al-Utba bin Rabia akasema: "Usiku huu kazaliwa mtoto kwa ajili yenu[38]……..ndani ya usiku huu kazaliwa nabii wa umma huu naye ni Ahmad wa mwisho……Kisha akatoa alama zinazomtambulisha."[39]

## Kunyonya kwake:

Maziwa ya mwanzo aliyonyonya baada ya maziwa ya mama yake mzazi yalikuwa ni ya Thuwaybah mjakazi wa Abu Lahabi bin Abdul Muttalib. Hiyo ilikuwa ni kabla hajanyonyeshwa na Halima binti Abu Dhuaybu As-Saadiyyah,[40] kwani watu wa Makka walikuwa waki-wanyonyesha watoto wao kwa wanawake wa vijijini kwa lengo la kutaka ufasaha.

Ushahidi juu ya hilo ni kauli yake mwenyewe (s.a.w.w.): "Mimi ndiye mfasaha kuliko wote wanaotamka kiarabu, zaidi ya hapo mimi ni mkurayshi na nimenyonyeshwa na watoto wa Saad."

Alibakia (s.a.w.w.) mikononi mwa Halima muda wa miaka miwili mpaka alipoacha kunyonya, ndipo Halima akamkabidhi kwa mama yake na kumpa habari za baraka zote alizoziona, hapo Amina akam-rudisha kwa Halima kisha baadae Halima akamrudisha kwa mama yake huku Mtume (s.a.w.w.) akiwa na umri wa miaka mitano.[41]

38 *Tarikh Yaaqubiy*, Juz. 2, Uk. 8 – 9.

39 *Tabaqat* ya Ibnu Saad, Juz. 1, Uk. 106. *As-Siratun-Nabawiyyah*, Juz. 1, Uk. 226. *Al-Iswabah*: 1/ 3, Uk. 181.

40 *Tarikh Yaaqubiy*, Juz. 2, Uk. 9.

41 *Aayanus-Shia*, Juz. 1, Uk. 218.

## Majina yake na majina yake ya heshima:

Muhammad bin Jubayri bin Mut'im amepokea toka kwa baba yake kuwa alimsikia Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Hakika mimi nina majina kadhaa: Mimi ni Muhammad, Ahmad na mfutaji, Mwenyezi Mungu atafuta ukafiri kupitia mimi. Na mimi ni mkusanyaji, Mwenyezi Mungu atakusanya watu chini ya nyayo zangu. Na mimi ndiye niliyefuata baadae hakuna mwingine yeyote baada yangu."[42]

Jina lake la heshima lililo maarufu ni: Abu Qaasim. Imepokewa kutoka kwake kuwa alisema: "Jiiteni kwa jina langu lakini msijipe heshima kwa jina langu la heshima."[43] Pia inasemekana kuwa jina lake la heshima ndani ya Taurati ni: Baba wa wajane, na jina lake ni: Swahibul-Malhama.[44]

Al-Halbiy amesema: "Ni wazi kuwa majina yake yote yametokana na sifa za vitendo alivyotenda ambavyo vinalazimu sifa na ukamilifu, hivyo ndani ya kila sifa ana jina."[45]

## Vipindi vya maisha yake:

Maisha ya Mtume (s.a.w.w.) mwanzo yamegawanyika katika vipindi viwili tofauti:
Kipindi cha kwanza: Ni kuanzia alipozaliwa mpaka alipokabidhiwa unabii, nacho ni kipindi cha miaka arubaini.

Kipindi cha pili: Ni kuanzia alipokabidhiwa unabii mpaka alipofariki,

42 *Sahih Bukhar*, Juz. 4 Uk. 225. *Tabaqat Ibnu Saad*, Juz. 1, Uk. 104.
43 *Tabaqat Ibnu Saad*, Juz. 1, Uk. 104.
44 *Al-Manaqib*, Juz. 1, Uk. 13. *Iilamul-Waraa*, Juz. 1, Uk. 51.
45 *As-Siratun-Nabawiyyah* cha Al-Halbiy, Juz. 1, Uk. 78 – 82.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 29



nao ni muda wa miaka ishirini na tatu.

Katika vipindi vyote vya maisha yake, Muhammad bin Abdullah (s.a.w.w.) alijulikana kwa maadili mema, kujitenga na vitendo vya shirki, kujitenga na unywaji pombe, kutokuhudhuria vikao vya upuuzi, kamari na zaidi ya hayo ambayo vijana wa zama hizo walikuwa wakivutiwa nayo. Kutokana na maadili yake mema alijulikana kwa jina la **mwaminifu,** hivyo maquraishi walipozozana kuhusu mtu atakayeweka jiwe jeusi waliangukia kwenye uamuzi wa Muhammad (s.a.w.w.) huku wakikiri kuwa yeye ni mwaminifu asiyeyumba.

Wanahistoria wote wamekiri kuwa Muhammad (s.a.w.w.) hakuwahi kuabudu sanamu na alikuwa akichukizwa na masanamu hayo. Alikuwa akihamia pango la Hira kila mwaka muda wa mwezi mzima……Pia alikuwa mbali na sifa za kijahiliya ambazo walikuwa nazo vijana wa kiarabu wa zama hizo. Bali alikuwa akikataza ibada ya masanamu pale anapopata fursa ya kufanya hivyo.

Kila kipindi kati ya vipindi vya maisha yake kimegawanyika sehemu nyingi, hivyo kipindi cha kwanza unaweza kukigawa sehemu tatu:

Sehemu ya kwanza: Ni kuanzia alipozaliwa mpaka aliposafiri safari yake ya kwanza ya Sham akiwa na ami yake Abu Talib. Kipindi hicho alikuwa na umri wa miaka kumi na miwili.

Sehemu ya pili: Ni kuanzia pale aliporudi kutoka Sham mpaka alipomuoa Khadija. Kipindi hicho alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano.

Sehemu ya tatu: Ni kuanzia alipooa mpaka alipokabidhiwa unabii akiwa na umri wa miaka arubaini.

Kipindi cha pili kimegawanyika zama mbili tofauti:
Zama za kwanza: Nazo ni zama za Makka ambazo zilichukua muda wa miaka kumi na tatu.

Zama za pili: Nazo ni zama za Madina[46] ambazo zilichukua muda wa miaka kumi.

**Muhtsari:**

Ni maarufu kuwa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alizaliwa yatima. Na mama yake Amina binti Wahabi aliona baadhi ya alama zilizojulisha kuwa mwanae atakuwa na jambo kubwa na cheo cha juu.

Hakukuwa na kalenda maarufu ya kuhifadhi kumbukumbu za matukio, hivyo historia ya kuzaliwa Mtume (s.a.w.w.) imehifadhiwa na tukio la kuhujumiwa kwa Kaaba, tukio ambalo hujulikana kwa jina la tukio la tembo. Qur'ani imeashiria tukio hili la kihistoria ndani ya *Sura Al-Fiylu*.

Ukoo wa Abdul Muttalib ulimjali sana Muhammad bin Abdullah (s.a.w.w.). Hilo lilidhihirika pale walipompeleka kunyonya kwa Bani Saad kwani baada ya maziwa ya mama yake walimpeleka kijijini ili akanyonye katika mazingira ya afya na ufasaha wa lugha.

Mtume ana majina mazuri, sifa nzuri na majina mazuri ya heshima.

Maisha ya Mtume (s.a.w.w.) yalichukua miaka sitini na tatu huku yakigawanyika vipindi viwili vikuu: Cha kwanza: Kuanzia alipozaliwa mpaka alipokabidhiwa unabii. Muda wake ni miaka arubaini. Cha pili: Kuanzia alipokabidhiwa unabii mpaka alipofariki. Muda wake ni

46 Rejea zama za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwishoni mwa somo la kwanza.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 31



miaka ishirini na tatu.

## Maswali:

1. Weka kikomo cha mwaka aliozaliwa Mtume Muhammadi (s.a.w.w.).

2. Mlezi wa kwanza wa Mtume (s.a.w.w.) ni nani?

3. Ni zipi zilizokuwa dalili za huruma ya Mwenyezi Mungu kwa Mtume (s.a.w.w.) kabla hajazaliwa na baada ya kuzaliwa?

4. Ni mambo gani yalitokea siku ya kuzaliwa Mtume (s.a.w.w.)?

5. Wapi aliponyonya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na ni kwa nini?
6. Taja majina yake na majina yake ya heshima?

7. Ni upi uhusiano uliyopo kati ya majina yake na sifa zake?

# Kujisomea

## Maisha ya Mtume na historia ya Uislamu ndani ya mistari

I. Alizaliwa mwaka wa tembo (Ndovu) huko kwenye mji mtukufu wa Makka.

II. Alinyonyeshwa na Bani Saad.

III. Alirudishwa kwa mama yake na babu yake akiwa na umri wa miaka minne au mitano na ndani ya muda huu ilionekana karama ya kuomba mvua kupitia kwake.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 32



IV. Mama yake alifariki Mtume (s.a.w.w.) akiwa na umri wa miaka sita.

V. Aliishi pamoja na babu yake na mama yake muda wa miaka miwili, kisha babu yake akafariki huku Mtume (s.a.w.w.) akiwa na umri wa miaka minane.

VI. Babu yake aliacha majukumu ya kumlea mikononi mwa ami yake, hivyo akabaki mikononi mwak**e** mpaka alipooa.

VII. Alisafiri na ami yake kwenda Sham akiwa na umri wa miaka kumi na nane.

VIII. Njiani alikutana na padri Buhayra ambaye alimhadharisha ami yake Abu Talib dhidi ya vitimbi vya mayahudi.

IX. Alihudhuria kiapo cha damu baada ya miaka ishirini tangu kuzaliwa.

X. Baada ya kujengwa upya jengo la Al-Kaaba aliweka jiwe jeusi huku akishirikisha makabila yote katika hilo.

XI. Alisafiri kwenda Sham akiwa mtumishi wa mali ya Khadija.

XII. Alimuoa Khadija akiwa na umri wa miaka ishirini na tano.

XIII. Alikabidhiwa utume akiwa na umri wa miaka arobaini.

XIV. Ulinganio maalumu ulichukua muda wa miaka mitatu.

XV. Ndani ya mwaka wa nne tangu kukabidhiwa utume aliamrishwa kuwaonya jamaa zake wa karibu.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 33



XVI. Siku aliyowaonya jamaa zake wa karibu pia alitoa maelezo ya usia wa Ali (a.s.) kwa kumteua kuwa khalifa wake baada yake.

XVII. Kisha aliamrishwa kutangaza utume wake kwa watu wote.

XVIII. Baada ya mbinyo kuzidi toka kwa maquraishi aliwapa ruhusa waislamu wahame kuelekea Ethiopia ikiwa ni mwaka wa tano tangu kuwa Mtume.

XIX. Mwaka wa saba hadi wa kumi tangu kuwa Mtume aliwekewa vikwazo yeye na Bani Hashim wote wakiwa sehemu ijulikanayo kama bonde la Abu Talib.

XX. Baada ya vikwazo kuisha Abu Talib na Khadija walifariki, hivyo akauita mwaka huo kuwa ni mwaka wa huzuni.

XXI. Israi na Miraji ilikuwa ndani ya mwaka huu au kabla ya mwaka huu au baada ya mwaka huu kulingana na kauli tofauti.

XXII. Alikuwa akitangaza utume wake kwa makabila mbalimbali ifikapo msimu wa Hijja, hiyo ni baada ya kuondolewa vikwazo.

XXIII. Kisha akahamia Taifa akiwa na mtoto wa ami yake Ali (a.s.).

XXIV. Kwa mara ya kwanza yeye kukutana na watu wa Madina ilikuwa mwaka wa kumi na moja kisha akaendelea kukutana nao mpaka alipofanikiwa kuhamia Madina.

XXV. Maquraishi walijikusanya kwa lengo la kumuua hivyo akamwamuru Ali (a.s.) alale kitandani kwake wakati wa

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 34



kuhama kwenda Madina.

XXVI. Alifika Qubaa mfunguo sita. Na kuhama huko kukawa ndiyo mwanzo wa kalenda ya kiislamu kwa amri ya Mtume mwenyewe (s.a.w.w.).

XXVII. Ndani ya mwaka huu aliweka misingi ya mwanzo ya dola ya kiislamu kwa kuanza kujenga msikiti kisha kuunga undugu, kisha kwa kutoa waraka maalumu uliyoelekeza mpangilio wa shughuli za dola mpya, kisha akaweka mikataba na mayahudi. Ujumbe wa kwanza wa kijeshi uliongozwa na ami yake Hamza ikiwa ni mwezi wa saba tangu kuhamia Madina, hivyo kuanzia alipohama mpaka mwishoni mwa mwaka wa kwanza alituma ujumbe wa kijeshi mara tatu. Na ndani ya mwaka huo huo alianza maisha ya ndoa na Aisha baada ya kufunga naye ndoa huko Makka.

XXVIII. Ndani ya mwaka wa kwanza baada ya kuhama Aya nyingi katika Sura Baqarah ziliteremka, hivyo zikawafedhehesha wanafiki na kufichua mbinu za mayahudi huku zikileta baadhi ya hukumu.

XXIX. Mayahudi na maquraishi walikusudia kuiangusha dola changa ya Mtume (s.a.w.w.), isipokuwa Mtume (s.a.w.w.) aliweza kuzuwia harakati zao hivyo ndani ya mwaka wa pili kulitokea vita mara nane na ujumbe wa kijeshi mara mbili, vikiwemo vita vya Badr ambavyo vilikuwa ndani ya mwezi wa Ramadhani tarehe kumi na saba. Ndani ya mwaka huo huo funga ilifaradhishwa na Qibla kikabadilishwa, pia Ali (a.s.) alimuoa Fatima (a.s.).

Ndani ya mwaka huu kulishuhudiwa ushindi mbalimbali na sheria mbalimbali za kisiasa na kijamii, na ndiyo mwaka ambao maquraishi walipata pigo la kwanza la uchungu katika vita vya Badri. Ndani ya

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 35



mwaka huu liling'olewa kundi la kwanza la kiyahudi (Bani Qaynuqaa) baada ya kuvunja mkataba uliokuwepo kati yao na Mtume (s.a.w.w.), hiyo ilikuwa ni baada ya ushindi wa vita vya Badri.

XXX. Yaliendelea mashambulizi toka kwa mayahudi na maquraishi dhidi ya waislamu muda wa miaka mitatu: Mwaka wa tatu, wanne na watano. Kisha vikafuata vita vya Uhudi, kisha vya Bani Nadhiri, kisha vya Ahzab, kisha vya Bani Quraydha, kisha vya Bani Mustalaqi. Kwa ujumla mwaka wa tano ulikuwa ndio mwaka mgumu sana kwa Mtume (s.a.w.w.) na waislam ukilinganisha na miaka mingine.

XXXI. Baada ya hapo Mwenyezi Mungu alizuwia vitimbi vya mayahudi, hivyo suluhu ya Hudaibiya ikawa ndiyo mwanzo wa ukombozi kwa waislam, kwani Mtume (s.a.w.w.) alianza kuwekeana mikataba ya ushirikiano na makabila mbalimbali, hivyo nguvu ya mayahudi na maquraishi ikaanza kudhoofika. Kisha vikafuata vita vya Khaybar, Muuta, Ukombozi wa Makka, Hunayni na Tabuk.

XXXII. Mwaka wa tisa ulikuwa ni mwaka wa kupokea ujumbe toka sehemu mbalimbali, kisha ikafuata Hijja ya kuaga ndani ya mwaka wa kumi. Ndipo akafariki Mtume (s.a.w.w.) tarehe ishirini na nane mfunguo tano (Safar) mwaka wa kumi na moja tangu kuhamia Madina. Ikiwa ni baada ya nguzo za dola ya kiislamu kukomaa huku akiwa kaiwekea viongozi wenye uwezo wakiwakilishwa na Imam Ali bin Abu Talib (a.s.), mtu ambaye alilelewa na mikono miwili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kumlea malezi bora kamilifu huku akimuandaa maandalizi bora chini ya msaada wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuongoza umati wake.

XXXIII. Matokeo ya ulinganio wa zama za Makka ni kuanzisha

umma wa kiislamu kupitia mafunzo na malezi yake kiakili, kisaikolojia hadi kimantiki. Pia kuandaa nguvu ya kijeshi ndani ya muda huo huku akifanikiwa kuweka mipango kwa amri ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya mustakbali wa Uislamu, hivyo akalea kundi la wachamungu kisha akalitangaza hatua kwa hatua, huku akijiandaa kwa uhamisho mkubwa ikiwa ni baada ya kuikomboa Madina kupitia Uislamu wa watu wema wa zama hizo.

XXXIV. Matokeo ya ulinganio wa Mtume (s.a.w.w.) zama za Madina yalionekana pale ilipoanzishwa ndani ya Bara la uarabu dola ya kwanza ya kisiasa ya kiislamu, na kuanzishwa sheria ya kijamii ambayo ilijenga heshima itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na kufungua mifereji ya nguvu za kiakili katika jamii ya kibinadamu kupitia mapinduzi ya kielimu ambayo yalianzishwa na Uislamu kwa baraka za Qur'ani ambayo ilikuwa ikiwaandaa waislam kwa ajili ya kuondoa vikwazo wakati wa kueneza Uislamu nje ya Bara la uarabu kwa ajili ya kutangaza jina la Mwenyezi Mungu katika ardhi hii.

Siku ya Ghadiri baada ya hija ya kuaga Mtume (s.a.w.w.) alimtangaza rasmi kiongozi aliyestahiki kisheria kuchukua nafasi yake. Kwa ajili hiyo Mtume (s.a.w.w.) alichukua dhamana ya kuendeleza mapinduzi ya kiroho kupitia mikono ya kizazi chake ambacho Mwenyezi Mungu amekiondolea uchafu na kukitakasa kabisa.

XXXV. Hivyo matokeo ya zama za Mtume (s.a.w.w.) yalikuwa: Kwanza, kupatikana Uislamu uliyokamilika na wa kudumu kwa ajili ya kutoa mpangilio wa maisha ya mwanadamu.

Pili: Kupatikana umma wa kiislamu uliobeba bendera ya kiislamu huku ukiamini itikadi na nidhamu za maisha kwa mujibu wa Uislamu. Tatu: Kupatikana dola ya kiislamu ambayo inaelekeza Uislamu na kupambana na vikwazo ambavyo vinajitokeza kwa lengo la kuzuia maendeleo ya Uislamu.

Nne: Kuandaa viongozi wema wa umma wa kiislamu wenye uwezo kwa lengo la kuendeleza malezi ya kiroho ya kimapinduzi kwa misingi na mafunzo ya Mwenyezi Mungu, na kwa ajili ya kufungua vipaji vya wanadamu kwa lengo la kumwendeleza na kumpeleka mwanadamu katika ukamilifu.

# Somo la tano

## Tabia na mwonekano wa hitimisho la manabii (s.a.w.w.)

**Ndani ya Qur'ani Tukufu:**

Hakika Muhammad bin Abdullah alisifika kwa sifa nzuri na maadili bora ambayo yalimtofautisha na kila aliyeishi katika zama zake au kabla yake au aliyekuja baada yake, hivyo ndio maana akawa ni mbora wa manabii. Hakika ukamilifu wake umeelezwa wazi na Qur'ani kupitia maelezo yake matukufu. Qur'ani imeelea ukamilifu wa akili yake na ubora wa maadili yake kwa kusema: **"Kwa neema ya Mola wako wewe si mwenda wazimu.* Na kwa hakika una malipo yasiyokatika.* Na bila shaka una tabia njema tukufu."**[47]

47 - Al-Qalam: 2 -4.

Utumwa wake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu umeonyeshwa na kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Utukufu ni wake ambaye alimpeleka mja wake usiku kutoka msikiti mtukufu mpaka msikiti wa mbali."[48]**

Ama ukunjufu wa kifua chake umeashiriwa na Aya: **"Je hatukukupanulia kifua chako?"[49]** Ama kumfuata kwake Mwenyezi Mungu katika kila kitu huku akimwogopa na kumnyenyekea yeye tu kumeelezwa na Aya: **"Sifuati ila ninayofunuliwa kwa wahyi. Hakika mimi naogopa nikimwasi Mola wangu adhabu ya siku iliyo kuu."[50]** Ushahidi mwingine ni Aya: **"Wale wanaofikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kumwogopa yeye wala hawamwogopi yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye atoshaye kuhesabu."[51]**

Ama huruma yake na upole wake kwa walimwengu huku akiwahangaikia watu ili kuwaongoza waelekee kwa Mwenyezi Mungu kumeelezwa na Aya: **"Nasi hatukukutuma ila uwe rehema kwa walimwengu."[52]**Na akasema: **"Bila shaka amekufikieni Mtume kutoka miongoni mwenu, yanamhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni, kwa waumini ni mpole, mwenye kuwaonea huruma.**"**[53]** Na Aya isemayo: **"Enyi watu wa kitabu, hakika amekwisha kufikieni mtume wetu, anayekubainishieni mengi mliyokuwa mkiyaficha katika kitabu, na kusamehe mengi"[54]** inaonyesha msamaha wake.

[48] - Al-Israi: 1.
[49] - Al-Inshirah: 1.
[50] - Yunus: 15.
[51] - Al-Ahzabi: 39.
[52] Al-Anbiyai: 107.
[53] At-Tawba: 128.
[54] Maidah: 15.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 39



Ama Aya isemayo: "Sema: Hii ndiyo njia yangu ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa ujuzi, mimi na wanaonifuata, na Mwenyezi Mungu ametakasika na kila upungufu wala mimi simo miongoni mwa washirikina"[55] inaonyesha ufahamu wake na kudumu kwake katika njia ya uongofu wa Mola wake. Pia hali hiyo inathibitishwa na Aya isemayo: "Sema: Na uite kwa Mola wako, bila shaka wewe uko juu ya mwongozo ulio sawa".[56] Na ile isemayo: "Basi tegemea kwa Mwenyezi Mungu hakika wewe uko juu ya haki iliyo wazi."[57] Pia ile isemayo: **"Yeye ndiye aliyemtuma mtume wake kwa mwongozo na kwa dini ya haki ili ishinde dini zote, ingawa washirikina watachukia."**[58] Zote hizo zinathibitisha hali hiyo.

Aya ifuatayo: **"Ambao wanamfuata mtume, nabii aliyoko Makka, ambaye wanamwona ameandikwa kwao katika Taurati na Injili, ambaye anawaamrisha mema na anawakataza yaliyo mabaya na kuwahalalishia vizuri na kuwaharamishia maovu, na kuwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao."**[59] inathibitisha kutojifunza kwake toka kwa mtu yeyote huku akimkomboa mwanadamu dhidi ya kila aina minyororo.

Ama uadilifu na usawa wake katika maadili na mwenendo wake umeashiriwa na Aya isemayo: **"Na hivyo tumekufanyeni umati bora ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe shahidi juu yenu."**[60]

---

55 Yusuf: 108.

56 Al-Hajj: 67.

57 An-Namlu: 79.

58 At-Tawba: 33.

59 Al-Aa'raaf: 157.

60 Al-Baqarah: 43.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 40



Aya ifuatayo: "Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kumwogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana."[61] Imethibitisha kuwa yeye ndiye mfano wa kuigwa katika ukamilifu wa mwanadamu. Ama utawala wake juu ya viumbe na cheo chake juu yao umethibitishwa na Aya isemayo: **"Hakika kiongozi wenu hasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake."**[62]

Aya ifuatayo: **"Muhammad mtume wa mwenyezi Mungu na walio pamoja naye ni imara mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao"**[63] inathibitisha jinsi alivyo mkali dhidi ya wapinzani na makafiri.

Ama Aya ifuatayo**: "Ewe Nabii, kwa hakika sisi tumekutuma shahidi na mtoaji wa habari nzuri na muonyaji. Na muhitaji kwa Mwenyezi Mungu kwa idhini yake na taa itoayo nuru."**[64] inathibitisha ufasaha wake, kuhusika kwake katika kila jukumu na kuwaongoza watu.

**Ndani ya maelezo ya bwana wa mawasii (a.s.):**

Imam Ali (a.s.) amesema: " ……Mpaka Mwenyezi Mungu alipomtuma Muhammad shahidi, mtoaji wa habari njema, mwonyaji, mbora wa viumbe kati ya watoto wote, na mbora wa viumbe watakasifu kati ya wakongwe wote, mtakasifu wa maadili kati ya watakasifu wote, na mbora wa ukarimu kati ya wakarimu wote."[65]

---

61 Al-Ahzabi: 21.

62 Al-Maidah: 55.

63 - Al-Fat'hu: 29.

64 Al-Mulk: 26.

65 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 105.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 41



"Akamteua kutokana na mti wa manabii, shubaku yenye mwanga, nywele za utosi wa watukufu…… na chemchemu ya hekima, tabibu maarufu kwa tiba yake, yuko tayari kwa dawa yake huku akifuatilia kwa hiyo dawa yake kila sehemu yenye mghafiliko na sehemu za shaka."[66]

"Nakiri kuwa Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake aliyemteua kati ya viumbe Wake, aliyeteuliwa kwa ajili ya kubainisha ukweli halisi, aliyeteuliwa mahsusi kwa ajili ya miujiza mitukufu na ujumbe mtakatifu, mwenye kubainisha alama za uongofu kupitia ujumbe huo, hivyo mwenye kujitenga naye yumo katika upotevu mkubwa."[67]

"Hakika Mwenyezi Mungu alimtuma Muhammad huku ndani ya waarabu hakuna anayejua kusoma kitabu wala anayedai unabii, hivyo akawapeleka watu mpaka akawafikisha sehemu yao, huku akiwafikisha eneo la uokovu wao, hivyo njia yao ikanyooka na sifa zao zikatulia."[68]

"Hivyo akavuka kiwango katika kutoa nasaha, akafuata njia sahihi na kulingania hekima na mawaidha mazuri."[69]

"Mwenye kutangaza haki kupitia haki, mwenye kuondoa mchemko wa batili, na mwenye kuangamiza ukali wa upotovu. Kama alivyobebeshwa ndivyo alivyoinuka huku akisimama kwa nguvu zote kupitia amri yake. Mwenye kuharakisha katika kupata ridhaa Zako huku akiwa haogopi kwenda vitani wala si dhaifu katika nia. Mwenye kuhifadhi ufunuo Wako, mwenye kulinda ahadi Yako huku akiende-

66 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 108.
67 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 178.
68 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 33.
69 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 95.

lea kutekeleza maamrisho Yako……..Hivyo yeye ni mwaminifu mwenye kuaminika na muhazini wa elimu Yako ya siri."[70]

"Imam wa atakayemcha Mwenyezi Mungu na jicho la atakayeongoka."[71]

"Hivyo akapambana katika njia ya Mwenyezi Mungu dhidi ya wale waliyomkimbia na dhidi ya wale waliyojitenga Naye……..[72] kwa ajili ya kutetea dini Yake, huku haumzuwii kufanya hivyo mkusanyiko wa wote wenye kumpinga na ule wa wenye kutaka kuzima nuru yake."[73]

"Ilikuwa tukizidiwa na ukali wa vita tunajikinga kwa mtume, hivyo hakuna yeyote kati yetu aliyekuwa karibu na adui zaidi yake."[74]

"Hivyo muige Mtume wako mbora wa watakasifu. Hakika katika kumuiga kuna kigezo chema kwa atakayeiga. Aliidokoa dunia na wala hakuitamani kabisa, hivyo yeye ndiye aliyeiacha dunia bila kuijali, na ndiye aliyeliacha tumbo tupu bila dunia…… Alipewa dunia yote akakataa kuipokea………..Alikuwa akila huku kakaa aridhini, alikaa mkao wa mtumwa huku akishona viatu vyake kwa mkono wake……..Alitoka duniani bila kustarehe na nayo, na alifika akhera akiwa salama, hivyo hakulimbikiza kitu mpaka alipofariki."[75]

70 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 72.
71 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 116.
72 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 133.
73 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 190.
74 *Kashful-Ghummah*, Juz. 1, Uk. 9.
75 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 160.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 43



## Ndani ya dondoo za sira yake binafsi:

Imepokewa kutoka kwa Hasan bin Ali (a.s.) kuwa Hindu bin Abi Halati alitoa wasifu wa Mtume (s.a.w.w.) kwa kusema: "Huanza kumtolea salamu yule aliyekutana naye……..Daima alikuwa na huzuni, mwingi wa tafakuri muda wote, mwimgi wa ukimya, hazungumzi pasipo na haja ya kuzungumza, huzungumza yenye kutosheleza, hazungumzi yasiyo na maana wala yaliyo pungufu, si mwenye kunyanyapaa wala si mwenye kudharau."

Hivyo neema ndogo kwake ilikuwa kubwa, haikashifu neema yoyote. Wala dunia na kichache alichokipata havimkasirishi. Anapopewa haki hakuna anayefahamu, wala hakutenda jambo kwa ghadhabu mpaka atakapoimiliki……..Anapoghadhibika huacha na kuondoka, na anapofurahi hubana sauti yake bali alama ya kucheka kwake ni tabasamu lake.

## Ndani ya dondoo za sira yake kijamii:

Husein bin Ali (a.s.) amepokea Hadithi kutoka kwa baba yake Imam Ali (a.s.) inayozungumzia sira ya Mtume (s.a.w.w.) kijamii:

"Anapokuwa nyumbani kwake hugawa muda wake mafungu matatu: Fungu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Fungu kwa ajili ya wakeze na fungu kwa ajili ya nafsi yake. Kisha fungu lake huligawa kwa ajili yake na kwa ajili ya kuhudumia jamii. Mwenendo wake katika kuhudumia umma ulikuwa ni kuwatanguliza wale wenye ubora huku akigawa ubora wao kulingana na ubora wao katika dini.

Alikuwa akizuia ulimi wake isipokuwa katika yale yanayomuhusu huku akiwaunganisha pamoja bila kuwasambaratisha. Humheshimu mheshimiwa wa kila kundi huku akimtawalisha juu yao. Hujihadhari

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 44



na kujilinda dhidi ya watu bila ya kupunguza bashasha yake wala tabia yake. Huwatafuta maswahaba zake wasipoonekana huku akiulizia matatizo ya watu.

Hulisifia jema na kulipa nguvu, na hulisifu kwa ubaya lile lililo baya huku akilishusha thamani. Jambo lake huwa wastani wala haghafiliki na kitu….Hapunguzi wala hazidishi huku aliye mbora mbele yake ni yule mwenye kuwanasihi sana waislam. Na mwenye hadhi kubwa sana mbele yake ni yule mwenye kuwasaidia na kuwanusuru watu. Hakai wala hasimami ila akimtaja Mwenyezi Mungu. Humpa kila aliyekaa naye fungu lake, hivyo anapokaa na mtu humvumilia mpaka mtu yule aondoke mwenyewe.

Amwombaye haja yoyote humjibu kwa kumtekelezea haja yake na kwa kauli tamu. Kikao chake ni kikao cha heshima, ukweli na uaminifu. Muda wote alikuwa ni mwenye bashasha, mwenye tabia nyepesi, mpole, asiye mkali wala si mkavu wa tabia. Hakuwa mchekaji ovyo wala mtukanaji, hakuwa mwaibishaji au mwongeza chumvi katika kusifia. Hujighafilisha na yale asiyoyapenda, hivyo alikuwa akinyamaza kwa sababu ya mambo manne: Kwa sababu ya busara, tahadhari, ridhaa, na tafakari."[76]

## Muhtasari:

Mwenyezi Mungu katoa wasifu wa Mtume Wake Muhammad (s.a.w.w.) kwa kueleza sifa zake za ukamilifu wa kibinadamu, hivyo akamfanya mbora wa mitume, hitimisho lao, na kigezo chema ambacho watakiiga wanadamu ili wanadamu hao wafikie kilele cha ukamilifu. Mwenyezi Mungu kawafafanulia waigaji sifa zake na maadili yake mazuri mema.

76 Tazama kitabu *Sunanun-Nabiyyi*, Uk. 14 na 17.

Kizazi chake ambacho ndio kijuacho zaidi yale yaliyomo nyumbani kimetoa wasifu wa mbora wao na mjumbe mwaminifu kupitia maneno yaliyo timilifu yaliyokusanya sifa zote. Huku maneno hayo yakitoa taswira ya ukamilifu na sifa ambazo zimemfanya awe ni kiigizo chema kwa wanaomfuata na bendera kwa wenye kuongoka.

Maelezo hayo yaliyonukuliwa kutoka kwa kizazi chake yametoa taswira ya adabu ya hali ya juu ya Mtume (s.a.w.w.) na sira yake binafsi na ya kijamii ya hali ya juu.

## Maswali:

1. Andika Aya inayoonyesha kuwa Mtume (s.a.w.w.) kapambika na sifa ya utumwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu?

2. Elezea jinsi Qur'ani ilivyotoa taswira ya shakhsia ya Mtume wa mwisho (s.a.w.w.)?

3. Ni sifa zipi muhimu za Mtume (s.a.w.w.) ambazo zimetajwa ndani ya *Nahjul-Balaghah*?

4. Linganisha sifa za Mtume (s.a.w.w.) zilizoelezwa na Qur'ani na zile zilizoelezwa na *Nahjul-Balaghah*?

5. Ni mambo gani unayoyapata katika sira ya Mtume (s.a.w.w.) kupitia maelezo ya Maimam Hasan na Husein (a.s.)?

# Somo la sita

## Tabia na mwonekano wa hitimisho la manabii (s.a.w.w.)

### Msomi asiyewahi kusoma wala kuandika:

Kati ya sifa za kipekee alizonazo Mtume wa mwisho (s.a.w.w.) ni kuwa yeye hakujifunza kusoma wala kuandika kutoka kwa mwalimu yeyote yule wa kibinadamu,[77] wala hakukulia katika mazingira ya kielimu bali alikuwa ndani ya jamii ya wajinga. Hakuna yeyote aliyepinga ukweli huu uliyoelezwa na Qur'ani tukufu, bali alikuwa ndani ya jamii ambayo watu wake walikuwa ni wajinga sana kuliko watu wa jamii nyingine yoyote ile, lakini pamoja na hali hiyo alileta Kitabu kinacholingania elimu na maarifa, kikiamsha fikra na akili huku kikiwa kimekusanya aina zote za maarifa.

Hakika Mtume (s.a.w.w.) alianza kuwafunza watu Kitabu na hekima[78] kwa silabasi nzuri sana mpaka akaibua ustaarabu wa kipekee ambao ulizamisha Magharibi na Mashariki kupitia elimu na maarifa yake, na bado mpaka leo nuru yake inang'aa, hivyo yeye Mtume (s.a.w.w.) ni mtu asiyewahi kusoma wala kuandika lakini alikuwa aking'oa ujinga, ujahili na ibada za masanamu huku akiwa amewaletea wanadamu dini ya hadhi ya juu na sheria ya kimataifa ambayo itawafaa wanadamu muda wote wa maisha yao.

Hivyo kupitia elimu, maarifa yake, maneno yake timilifu, ubora wa akili yake, mafunzo yake na silabasi yake ya malezi yeye mwenyewe

77 Al-Ankabuti: 48. Na An-Nahli: 103.
78 Al-Jum'ah: 2.

huwa ni muujiza, kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu akasema: **"Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake nabii asiyewahi kuandika wala kusoma, ambaye anamwamini Mwenyezi Mungu na maneno yake, na mfuateni ili mpate kuongoka."**[79]

Hakika Mwenyezi Mungu alimfundisha yale aliyokuwa hayajui na akamfunza kitabu na hekima mpaka akawa nuru, taa yenye kuangaza, dalili, shahidi, mtume wa wazi, mshauri nasaha mwaminifu, mkumbushaji, mwenye kutoa habari njema na mwenye kuonya.[80] Yeye ndiye aliyemkunjua kifua kwa ajili yake, akamwandaa kupokea ufunuo na kutekeleza jukumu la kuongoza katika jamii ambayo ilikuwa imetawaliwa na ubaguzi, chuki na majivuno ya kijahiliya. Hivyo akawa ni kiongozi bora wa hali ya juu aliyetambuliwa na wanadamu katika uhubiri, malezi na mafunzo.

## Mwislamu wa kwanza na mbora wa wanaibada:

Hakika kilele cha mwanzo ambacho ni lazima kwa kila mwanadamu akifikie ili ajiandae kuteuliwa na kuchaguliwa na Mwenyezi Mungu ni unyenyekevu kamili kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Muumba wa ulimwengu. Pia kujisalimisha kiukamilifu mbele ya nguvu Zake tukufu na hekima zake kamilifu. Pia utumwa wa hiari uliotimia mbele ya Mwenyezi Mungu mmoja wa pekee aliye tegemeo.

Hakika Qur'ani tukufu imemtolea ushahidi nabii huyu aliyewapita manabii wote katika kila kitu, ikasema: **"Na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha."**[81] Hakika hicho ni kilele cha ukamilifu ambacho

79 Al-A'araf: 158.

80 Al-Maidah: 15. Al-Ahzab: 46. An-Nisai: 174. Al-Fat'hu: 8. Az-Zukhruf: 29. Al-Aaraf: 68. Al-Ghashiyah: 21. Al-Israi: 105. Al-Maidah: 19.

81 Al-An'am: 163.

alikifikia mja huyu mkweli katika ibada zake, na akawa kawapita watu wote kwa ujumla. Hakika unyenyekevu wake wa kweli ulidhihirika katika matendo na kauli zake, hivyo akasema: "Kitulizo cha macho yangu ni Swala."[82]

Hakika Swala ilipendezeshwa kwake kama yalivyopendezeshwa maji kwa mtu mwenye kiu, hivyo anywapo maji hukata kiu, lakini Mtume (s.a.w.w.) hakukatwa kiu na Swala, kwani daima aliusubiri kwa hamu muda wa Swala huku shauku ya kusimama mbele ya Mola wake ikiongezeka. Alikuwa akimwambia mwadhini wake: "Tupe raha ewe Bilal".[83]

Imepokewa kuwa alikuwa akizungumza na familia yake na wao wakimzungumzisha lakini unapoingia wakati wa Swala huwa kama vile hawajui na hawamjui.[84] Kipindi anaposali kifua chake hutoa sauti ya kutetemeka kama sauti ya mchemko wa chungu huku akilia kutokana na kumwogopa Mwenyezi Mungu mtukufu hadi msala wake unalowana.[85]

Hivyo alikuwa akisali mpaka nyayo zake zinatoa harufu. Watu humwambia unafanya hivyo ilihali Mwenyezi Mungu ameshakusamehe madhambi yako yaliyotangulia na yaliyofuatia. Hujibu: "Hivi haifai nikawa mja mwenye kushukuru?"[86]

Alikuwa akifunga mwezi wa Shabani na Ranadhani na siku tatu ndani ya kila mwezi,[87] huku akibadilika rangi uingiapo mwezi wa

82 *Amali Twusiy*, Juz. 2, Uk. 141.
83 *Biharul-An'war*, Juz. 83 Uk. 16.
84 *Akhlaqin-Nabiyyi Waadabihi*, Uk. 251 na 201.
85 *Akhlaqin-Nabiyyi Waadabihi*, Uk. 251 na 201.
86 *Sunan-Nabiyyi*, Uk. 32.
87 *Akhlaqin-Nabiyyi*, Uk. 199. *Sahih Bukhar*, Juz. 1, Uk. 381, hadithi ya 1078.

Ramadhani, Swala zake huongezeka huku akinyenyekea katika dua.[88] Linapoingia kumi la mwisho la Ramadhani hujitenga na kuwahama wakeze huku akiupitisha usiku akiwa faragha kwa ajili ya ibada.[89]

Alikuwa akisema: "Dua ndiyo roho ya ibada, silaha ya muumini, nguzo ya dini na nuru ya mbingu na ardhi."[90] Daima alikuwa katika mawasiliano na Mwenyezi Mungu, akijifunga kwake kwa unyenyekevu na dua katika kazi yoyote ile kubwa au ndogo, bali alikuwa akimwomba Mwenyezi Mungu msamaha na kutubu kila siku mara sabini bila ya kuwa na dhambi yoyote.[91]

Hakuamka usingizini ila ni mnyenyekevu mwenye kusujudu.[92]

Alikuwa akimhimidi Mwenyezi Mungu kila siku mara mia tatu sitini akisema: "Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu wote, na ni nyingi katika kila hali."[93] Daima alikuwa akisoma Qur'ani huku akiwa ni mwenye kushughulishwa sana na usomaji huo.

**Imani isiyo na mipaka kwa Mwenyezi Mungu:**

Mwenyezi Mungu amemhimiza Mtume Wake (s.a.w.w.) awe na imani isiyo na mipaka na Mola Wake kwa kusema: **"Je, Mwenyezi Mungu hamtoshei mja wake?"**[94] Pia alisema: **"Na umtegemee Mwenye nguvu, Mwenye rehema.* Ambaye anakuona unaposimama.* Na mageuko yako katika wale wanaosujudu."**[95]

88 *Wasailus-Shia*, Juz. 4 Uk. 309.
89 *Sunan-Nabiyyi*, Uk. 300.
90 *Al-Kafiy,* Juz. 4 Uk. 155.
91 *Al-Mahijjatul-Baydhau*, Juz. 2, Uk. 281 – 284.
92 *Biharul-An'war*, Juz. 16, Uk. 217 na 253.
93 *Biharul-An'war*, Juz. 16, Uk. 217 na 253.
94 Az-Zumar: 36.
95 Shuaraa: 217 – 219.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 50



Imepokewa kutoka kwa Jabir (r.a.) kuwa: "Tulikuwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) tukafika kwenye mti wenye kivuli tukamwachia mti huo. Ghafla akatokea mtu kati ya mushrikina huku upanga wa Mtume (s.a.w.w.) ukiwa umetungikwa kwenye mti, ndipo mushrik yule alipouchukua upanga ule na kumwambia Mtume (s.a.w.w.): "Je unaniogopa? " Mtume akajibu: "Hapana." Mushriku akasema: "Nani atakuzuwia dhidi yangu?" Mtume akajibu: "Mwenyezi Mungu." Hapo upanga ukadondoka toka mikononi mwa mushriku.

Ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu alipouchukua na kusema: "Na wewe ni nani atakayekuzuwia dhidi yangu?" Akajibu: 'Mbora wa wachukuaji." Mtume akasema: "Je unakiri kuwa hapana mola wa haki isipokuwa Allah na kwamba hakika mimi ni Mtume wa Allah?" Mushriku akajibu: "Hapana, isipokuwa ninakuahidi kuwa sitokupiga vita, wala sitokuwa pamoja na watu wanaokupiga vita.

Hapo Mtume akamwachia, na mushriku akaenda kwa jamaa zake na kuwaambia: "Nimewajia toka kwa mbora wa watu."[96]

## Ushujaa wa hali ya juu:

Mwenyezi Mungu ameeleza sifa za Mtume Wake (s.a.w.w.) kwa kusema: **"Wale wanaofikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kumwogopa Yeye wala hawamwogopi yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye atoshaye kuhesabu."[97]**

96 *Riyadhu As-Swalihina* ya An-Nawawiy Uk. 5. *Sahihi Muslim*, Juz . 4, Uk. 465.
97 Al-Ahzab:39.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 51



Imam Ali (a.s.) ambaye mashujaa wa kiarabu waliinamisha vichwa mbele yake ametupa wasifu makini kuhusu ushujaa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akasema: "Pindi vita vinapokuwa vikali na kundi moja likalizidi kundi lingine basi tulikuwa tukijikinga kwa Mtume, hivyo hakuna yeyote anayekuwa karibu sana na maadui kuliko yeye."[98]

Mikidad ameelezea msimamo wa Mtume (s.a.w.w.) siku ya Uhud baada ya watu kutawanyika huku wakimwacha Mtume (s.a.w.w.) peke yake, Mikidad amesema: "Naapa kwa yule aliyemtuma kwa haki, ukimwona Mtume (s.a.w.w.) kainua mguu wake shibri moja basi ujue yuko mbele ya adui huku kundi la jamaa wa adui likiwa limemvamia na muda huo huo likitawanyika kwa kumkimbia, utamwona kasimama akirusha upinde au akirusha jiwe mpaka mawe yawaenee."[99]

## Utawa usiyokuwa na mfano:

Mwenyezi Mungu amesema kumwambia Mtume Wake (s.a.w.w.) kuwa: "Wala usivikodolee macho yako tulivyowastarehesha watu wengi miongoni mwao, ni mapambo ya maisha ya dunia, ili tuwajaribu kwa hayo, na riziki ya Mola Wako ni bora mno na iendeleayo." [100]

Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa mkweli katika kuiacha dunia na mapambo yake. Aliiacha dunia mpaka ikapokewa toka kwa Abu Umamah toka kwa Mtume (s.a.w.w.) kuwa alisema: "Mola Wangu alinitunukia akataka aifanye Makka yote iwe dhahabu kwa

98 *Fadhailul-khamsa mina Sahihi sitta*, Juz. 1, Uk. 138.
99 Al-*Maghaziy Al-Waqidiy*, Juz. 1, Uk. 239-240.
100 Taha:131.

ajili yangu, nikasema: Hapana Mola Wangu! lakini napenda niwe nashiba siku moja na kushinda na njaa siku nyingine……..Kwani nitakapokuwa na njaa nitakunyenyekea na kukukumbuka, na nitakaposhiba nitakushukuru na kukuhimidi”.[101]

Akalala juu ya changarawe na alipoamka zilikuwa zimeathiri ubavu wake. Akaambiwa: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu tungekuwekea kizuwizi.” Akajibu: “Mimi nina nini na hii dunia, kwani mimi si chochote ndani ya dunia hii isipokuwa ni kama msafiri aliyejipumzisha chini ya mti wa kivuli na baada ya mapumziko ataondoka na kuuacha ule mti.”

Ibnu Abbas amesema: “Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akilala njaa siku zenye kufuatana, huku familia yake ikiwa haipati chakula cha usiku. Mara nyingi mkate wao ulikuwa ni mkate wa shairi.”

Aisha amesema: “Familia ya Muhammad haikula milo miwili ndani ya siku moja isipokuwa mlo mmoja ulikuwa ni tende tu.”[102] Akamwambia mtoto wa dada yake Urwah: “Hakika sisi tulikuwa tukiutazama mwezi mwandamo, kisha mwezi mwandamo mwingine hadi miezi miandamo mitatu katika miezi miwili huku ndani ya muda wote huo haujawashwa moto katika nyumba za Mtume (s.a.w.w.).”

Urwah akamuuliza: “Ewe mama mdogo; alikuwa akiwalisha nini usiku?” Akajibu: “Vyeusi viwili: Tende na maji. Isipokuwa Mtume alikuwa na jirani yake wa kianswari aliyekuwa na mifugo, hivyo alikuwa akimpa Mtume wa Mwenyezi Mungu maziwa yake na Mtume anatupa sisi.”[103]

101 *Sunani Tirmidhiy*, Juz. 4 Uk. 1518 na 508, hadithi ya 2377 na 2360.
102 *Sahih Bukhari* Juz. 5 Uk. 2371, hadithi ya 6090.
103 *Sahih Bukhari* Juz. 2 Uk. 907, hadithi ya 2428.

Pia amesema: "Mtume (s.a.w.w.) alifariki huku ngao yake ikiwa imewekwa rehani kwa yahudi kwa thamani ya vibaba thelathini vya shairi."[104]

Imepokewa toka kwa Anas bin Malik kuwa: "Fatima (a.s.) alimpelekea Mtume (s.a.w.w.) kipande cha mkate. Mtume akasema: "Ewe Fatima, kipande hiki cha nini? "Akajibu: "Ni kipande cha mkate kwani roho yangu haijaridhika mpaka nikuletee kipande hiki." Mtume akasema: "Hakika hiki ni chakula cha kwanza kilichoingia ndani ya kinywa cha baba yako tangu siku tatu zilizopita."[105]

Hii ni sura fupi na halisi ya utawa wa Mtume (s.a.w.w.) na jinsi alivyoipa mgongo dunia mpaka akafariki.

## Muhtasari:

Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammad bin Abdullah hakujifunza mikononi mwa mwanadamu yeyote, lakini alikuja na Kitabu cha kielimu na kimaarifa cha kimataifa ambacho kimewataka wanadamu wote katika zama zote walete mfano wake.

Kupitia Kitabu hicho Mtume (s.a.w.w.) aliweza kumtoa mwanadamu toka jamii ya kijinga mpaka jamii ya kielimu iliyokamilika yenye kustaarabika, huku akihimiza usiku na mchana juu ya utafutaji wa elimu na maarifa mbalimbali. Hivyo kupitia Kitabu hicho aliasisi dola kubwa na kujenga ustaarabu wa pekee ambao mfano wake haujashuhudiwa na mwanadamu.

104 *Sahih Bukhari* Juz. 3 Uk. 1068, hadithi ya 2759.
105 *Tabaqati* ya Ibnu Saad, Juz. 1, Uk. 400.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 54



Mtume (s.a.w.w.) alibeba maana kamili ya ibada kwa Mwenyezi Mungu Muumba, hivyo alikuwa na mahusiano ya karibu sana na Mola Wake Mtukufu, mahusiano ambayo yalitokana na ujuzi, mapenzi, utashi, na moyo mkunjufu, hivyo akawa ni kiigizo chema katika swala yake, funga, dua na uombaji msamaha, kiigizo ambacho kinamchorea mwanadamu njia ya ukamilifu kuelekea kwa Muumba, Mjuzi.

Mtume (s.a.w.w.) alianza harakati akiwa amebeba jukumu kubwa huku akimtegemea Mwenyezi Mungu katika kila harakati na kila jambo, hivyo akawa ni shujaa, jasiri na mkakamavu katika kulingania njia ya Mwenyezi Mungu.

Mtume (s.a.w.w.) aliishi mbali na ladha za dunia na starehe zake, hivyo alikuwa ni sehemu ya mafakiri na masikini, akishirikiana nao katika taabu zao huku akitarajia rehema za Mola Wake, mnyenyekevu Kwake, mwenye kujitenga na kila ujeuri utokanao na starehe za dunia na furaha za mapambo yake.

## Maswali:

1. Ni nani nabii mwarabu asiyewahi kusoma wala kuandika. Na nini makusudio ya kutowahi kusoma wala kuandika?
2. Je, Qur'ani ni kitabu cha elimu na maarifa? Kwa nini?
3. Elezea ibada ya Mtume (s.a.w.w.) na jinsi alivyojielekeza kwa Mwenyezi Mumgu?
4. Toa sura halisi ya utegemezi na imani kubwa ya Mtume kwa Mwenyezi Mungu?
5. Elezea jinsi Mikidad alivyoelezea msimamo wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na ushujaa wake siku ya Uhudi?
6. Elezea utawa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu?

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:11 AM Page 55



# Somo la saba

## Tabia na mwonekano wa hitimisho la manabii (s.a.w.w.)

**Ukarimu:**

Ibnu Abbas amesema: "Mtume (s.a.w.w.) alikuwa mkarimu sana katika mambo ya kheri, ukarimu wake ulikuwa ukiongezeka zaidi ndani ya mwezi wa Ramadhani……Alikuwa akikutana na Jibril ndani ya kila mwezi wa Ramadhani kila mwaka, hivyo akikutana na Jibril huwa mkarimu sana kuliko upepo uvumao."[106]

Jaabir amesema: "Mtume (s.a.w.w.) hakuombwa chochote akajibu hapana."[107]

Imepokewa kuwa Mtume (s.a.w.w.) alikwenda kwa muuza nguo akanunua kanzu kwa dirhamu nne akatoka huku kaivaa. Ghafla akatokea mtu kati ya answari na kusema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nivishe kanzu, hakika Mwenyezi Mungu atakuvisha nguo kati ya nguo za Peponi." Hapo Mtume (s.a.w.w.) akavua kanzu na kumvisha. Kisha Mtume (s.a.w.w.) akarudi dukani na kununua tena kanzu kwa dirhamu nne huku akibakiwa na dirhamu mbili. Ghafla akatokea kijakazi njiani huku akilia. Mtume akamuuliza: "Kitu gani kinakuliza?" Akjajibu: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu mabwana zangu wamenipa dirhamu mbili nikanunulie unga lakini zimepotea." Basi hapo Mtume (s.a.w.w. ) akatoa dirhamu mbili na kumpa.

106 *Sahih Muslim*, Juz. 4, Uk. 481, hadithi ya 3308. *Musnadi Ahmad*, Juz. 1, Uk. 598, hadithi ya 3415.

107 *Sunanud-Daramii*, Juz. 1, Uk. 34.

Kijakazi yule akasema: "Nahofia watanipiga."

Mtume (s.a.w.w.) akaenda naye kwa mabwana zake, kisha Mtume (s.a.w.w.) akawatolea salamu. Wakaijua sauti yake, kisha akatoa mara ya pili, kisha mara ya tatu. Ndipo walipomjibu salamu yake. Mtume akasema: "Je mlisikia salamu yangu ya mwanzo?" Wakajibu: "Ndio, lakini tulipenda utusalimie zaidi, je ni jambo gani lililokusumbua?" Mtume (s.a.w.w.) akajibu: "Nilimuonea huruma kijakazi huyu msije mkampiga." Hapo bwana wake akasema: "Yeye yuko huru katika njia ya Mwenyezi Mungu, hivyo utaondoka naye."

Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu akawabashiria heri na pepo kwa kusema: "Hakika Mwenyezi Mungu ametia baraka katika dirhamu kumi, kamvisha kanzu Mtume wake na mtu kati ya answari, na akampa uhuru mtumwa, ninamhimidi Mwenyezi Mungu, hakika Yeye ndiye aliyeturuzuku haya kwa uwezo Wake."[108]

Alikuwa akiwaachia watumwa wote huru uingiapo mwezi wa Ramadhani huku akimpa kila mwombaji.[109]

## Upole na Usamehevu:

Zaid bin Aslam amesema: "Tulipata habari kuwa Abdullah bin Salama alikuwa akisema: "Hakika sifa za Mtume wa Mwenyezi Mungu ndani ya Taurati ni: Ewe nabii hakika tumekutuma uwe shahidi, mbashiri, mwonyaji na kinga kwa wasiojua kusoma na kuandika. Wewe ni mja Wangu na Mtume Wangu, nimekuita jina la Al-Mutawakkil (Mwenye kunitegemea). Si mkali wala si mshupavu wa moyo. Si mpiga kelele masokoni wala halipi ubaya kwa ubaya lakini

108 Al-*Mu'ujam Al-Kabir* cha Tabaraniy, Juz. 12 Uk. 337, hadithi ya 13607.
109 *Hayatun-Nabii wa Siratuhu*, Juz. 3 Uk. 311 na 303 na 306 na 307.

husamehe. Sitomfisha mpaka ninyooshe dini iliyopinda na watu waseme: Hapana Mola wa haki isipokuwa Allah, hivyo kupitia yeye Mwenyezi Mungu afungue macho yasiyoona, masikio yasiyosikia na nyoyo zilizoziba." Maneno hayo yalipomfikia Kaaby akasema: "Amesema kweli Abdullah bin Salama."

Imepokewa toka kwa Aisha kuwa: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) hakulipiza kisasi dhidi ya jambo lolote alilotendewa binafsi isipokuwa linapovunja utukufu wa Mwenyezi Mungu. Hivyo hakukipiga kitu chochote kwa mkono wake isipokuwa akipige katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hakuna chochote alichoombwa akanyima isipokuwa aombwe jambo la dhambi. Hakika alikuwa mbali na jambo lolote la dhambi."[110]

Ubaydu bin Umayr amesema: "Hakuna jambo lolote alilofanyiwa Mtume (s.a.w.w.) lisilolazimu adhabu kisheria isipokuwa alisamehe."[111]

Anas amesema: "Nilimhudumia Mtume wa Mwenyezi Mungu muda wa miaka kumi, ndani ya muda wote huo hakuwahi kunifyonza na nilipofanya jambo lolote hakuniambia: Kwa nini umefanya hivi? Na nilipoacha jambo lolote hakuwahi kuniuliza: Kwa nini umeacha?"[112]

Alikuja bedui na kuvuta nguo ya Mtume (s.a.w.w.) kwa nguvu mpaka upinde wa nguo ukamuumiza Mtume shingoni, kisha bedui yule akasema: "Ewe Muhammad amrisha nipewe sehemu ya mali ya Mwenyezi Mungu iliyopo kwako." Mtume (s.a.w.w.) akamgeukia huku akitabasamu, kisha akaamrisha apewe.

110 *Hayatun-Nabii wa Siratuhu*, Juz. 3, Uk. 311 na 303 na 306 na 307.
111 *Sahihi Bukhari*, Juz. 5 Uk. 2260, hadithi ya 5738.
112 Tazama: *Muhammad fil-Qur'ani*, Uk. 60-65.

Hakika Mtume alifahamika kwa usamehevu na upole muda wote wa maisha yake…….Hivyo alimsamehe Wahshiyu muuaji wa ami yake Hamza……Alimsamehe mwanamke wa kiyahudi aliyempa nyama ya mbuzi yenye sumu. Pia alimsamehe Abu Suf'yani huku akifanya kitendo cha kuingia nyumbani mwa Abu Suf'yani ni usalama dhidi ya kuuawa. Aliwasamehe maquraishi ambao walimpiga vita kwa kila aina ya nyenzo waliyokuwa nayo……huku akiwa katika kilele cha uwezo na nguvu lakini anawaombea heri kwa kusema: "Ewe Mola Wangu! waongoze jamaa zangu, hakika wao hawajui…….Nendeni hakika nyinyi ni watu mlioachiwa huru."

Qur'ani imeweka bayana usamehevu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ikaelezea hilo kwa kusema: **"Basi kwa sababu ya rehema ya Mwenyezi Mungu umekuwa mpole kwao na kama ungekuwa mkali mshupavu wa moyo wangekukimbia. Basi wasamehe na uwaombee msamaha na ushauriane nao katika mambo."**[113] Na ikasema tena: **"Bila shaka amekufikieni Mtume kutoka miongoni mwenu, yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni, kwa waumini ni mpole, mwenye kurehemu."**[114]

Kwa usamehevu huu mkubwa Mtume (s.a.w.w.) aliweza kukonga nyoyo ngumu kakamavu na kuzifanya zimzunguke na kuamini utume wake wa kudumu.

## Haya:

Imepokewa kutoka kwa Abu Saad Al-Khidriy kuwa: "Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na haya sana kuliko mtawa katika utawa wake, hivyo iwapo akichukizwa na jambo hufahamika kupitia uso

113 Al Imrani: 159.

114 At-Tawba:128.

wake."[115]

Imepokewa kutoka kwa Ali (a.s.) kuwa: "Iwapo Mtume (s.a.w.w.) kaombwa kutenda jambo na akataka kulitenda basi husema: Ndio. Na iwapo hataki kulitenda hunyamaza kimya, wala hakuwa anasema hapana akataapo kutenda jambo."[116]

## Unyenyekevu:

Imepokewa kutoka kwa Yahya bin Abi Kathiri kuwa Mtume (s.a.w.w) alisema: "Ninakula kama alavyo mtumwa, nakaa kama akaavyo mtumwa, hakika mimi ni mtumwa."[117]

Siku moja Mtume (s.a.w.w.) alimsemesha mtu, basi mtu huyo akatetemeka, hapo Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Tulia, hakika mimi si malaika isipokuwa mimi ni mtoto wa mwanamke wa kikurayshi ambaye alikuwa akila nyama kavu tu."[118]

Imepokewa kutoka kwa Abu Amamah kuwa: "Mtume alitujia huku anatembelea fimbo basi tukasimama, hapo Mtume (s.a.w.w.) akasema: Msisimame kama wanavyosimama waajemi kwani baadhi yao huwatukuza wengine."[119] Alikuwa akiwatania maswahaba zake isipokuwa hatamki ila la kweli.[120] Pia alikuwa akiwatolea watoto salamu.[121] Alishirikiana na swahaba zake katika kujenga msikiti.[122]

115 *Sahihi Bukhari*, Juz. 3 Uk. 1306, hadithi ya 23369.

116 *Majmauz-Zawaid*, Juz. 9, Uk. 13.

117 *Tabaqat ya Ibnu Saadi*, Juz. 1, Uk. 37. *Majmauz-Zawaid*, Juz. 9, Uk. 19.

118 *Sunanu Ibnu Majah*, Juz. 2, Uk. 1101, hadithi ya 3312.

119 *Sunanu Abi Daudi*, Juz. 4, Uk. 358, hadithi ya 5330.

120 *Sunanut-Tirmidhiy*, Juz. 4, Uk. 304, hadithi ya 1990.

121 *Hayatun-Nabii wasiratuhu*, Juz. 3, Uk. 313, kutoka kwa Ibnu Saad.

122 *Musnad Ahmad*, Juz. 3, Uk. 80.

Akachimba handaki,[123] na mara nyingi alikuwa akiomba ushauri toka kwa maswahaba zake, japokuwa yeye ndiye aliyekuwa na akili bora kuliko watu wote.[124]

Mara nyingi alikuwa akisema: "Ewe Mola Wangu nipe uhai katika hali ya umaskini na unifishe nikiwa masikini. Hakika muovu wa kutupa ni yule anayekusanyikiwa na ufakiri wa dunia na adhabu ya Akhera."[125]

Hii ni sura fupi sana kuhusu sifa za shakhsia ya Mtume (s.a.w.w.), na hizi ni baadhi tu ya tabia zake binafsi na za kijamii. Pia kuna sura nyingi nzuri kuhusu mwenendo wake na sira yake kiutawala, kisiasa, kijeshi, kiuchumi na kifamilia, mwenendo ambao unahitaji masomo ya ndani zaidi ili kufuata na kuuiga, hivyo masomo hayo tunayaacha kwa ajili ya muhula ujao.

Hivyo ndivyo zilivyotubainikia sifa za pekee za Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ambazo tunaweza kuzifupisha katika maneno yafuatayo:

Usafi wa familia, ulinzi wa Mwenyezi Mungu daima, tabia za hali ya juu, nafasi ya juu ya kijamii, maadili mema, ufasaha wa lugha, maisha mepesi, kujiepusha na kila aina ya shirki na kila aina ya mila potovu, kufikia kilele katika ibada ya Mwenyezi Mungu na unyenyekevu kwa ajili ya haki katika hali yoyote ile.

---

123 *Tabaqat cha Ibnu Saad*, Juz. 1, Uk. 240.

124 *Durul-Manthur*, Juz. 2, Uk. 359. *Al-Mawahibu Ad-Daniyyah*, Juz. 2, Uk. 331.

125 *Sunanut-Tirmidhiy*, Juz. 4, Uk. 499, hadithi ya 2352.

## Muhtasari:

Hakika Mtume (s.a.w.w.) alikuwa mkarimu sana, hivyo alikuwa akieneza upendo, ukarimu, wema na mali kwa watu wote, huku akitoa msamaha, huruma na ulaini kwao. Ili awaokoe toka kwenye ujinga wao na apate kuwaunganisha pamoja wawe kitu kimoja.

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anaishi na waislam kama mmoja wao huku haya zikimtukuza kwa kumpa haiba na heshima, huku unyenyekevu ukimzidishia heshima na utukufu. Hivyo alikuwa akiwahurumia wadogo na kuwaheshimu wakubwa. Alikuwa akisikia ushauri wa mnasihi ilihali yeye ni mwenye akili zitokazo mbinguni kwa njia ya ufunuo.

## Maswali:

1. Elezea jinsi Mtume (s.a.w.w.) alivyoshirikiana na ombaomba?
2. Thibitisha ukarimu wa Mtume (s.a.w.w.) kwa makafiri kwa kuonyesha matukio mbalimbali?
3. Ni sehemu gani Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akipiga au akiacha?
4. Ni wakati gani Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akiwasamehe wanaomkosea. Thibitisha hilo kwa kutoa visa viwili?
5. Elezea tunavyoweza kufaidika na sifa ya kutoa msamaha tunapolingania katika njia ya Mwenyezi Mungu?
6. Kwa nini Mwenyezi Mungu alimwamuru Mtume wake atoe msamaha na kuwaombea maghfira watu wake?
7. Elezea jinsi Mtume (s.a.w.w.) alivyopambana na yule aliyesimama kidete kuzuia dini ya Mwenyezi Mungu baada ya kuenea?

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 62



# Somo la nane

## Urithi wa mbora wa mitume

**Akili na ukamilifu wa mwanadamu:**

Mtume (s.a.w.w.) alielezea kuhusu akili, majukumu yake na nafasi yake katika maamrisho na majukumu ya mwanadamu, nafasi yake katika matendo na malipo, hivyo akabainisha sababu za kukua na kukamilika kwa akili akasema: "Hakika akili ni kitanzi dhidi ya ujinga na nafsi ni sawa na mnyama mbaya, hivyo iwapo hakufungwa kitanzi hucharuka, basi akili ni kitanzi kuliko ujinga.

"Mwenyezi Mungu aliumba akili kisha akaiambia nenda mbele ikaenda mbele. Rudi nyuma, ikarudi nyuma. Hapo Mwenyezi Mungu akaiambia: Naapa kwa nguvu Zangu na utukufu Wangu, sikuumba kiumbe muhimu kuliko wewe, wala kitiifu kuliko wewe. Kupitia wewe nitaumba na nitarudisha, na kwa ajili yako nitalipa thawabu na nitaadhibu, hivyo uvumilivu ukatokana na akili, na elimu ikatokana na uvumilivu, na uongofu ukatokana na elimu. Utawa ukatokana na uongofu, na kujimiliki kukatokana na utawa, na aibu ikatokana na kujimiliki na heshima hutokana na haya.

"Heshima husababisha kudumu ndani ya heri na kuchukizwa na shari, hivyo kumtii mshauri kunatokana na kuchukizwa na shari. Haya ni makundi kumi katika aina za kheri na katika kila kundi kuna aina kumi za kheri…."[126]

126 *Tuhfatul-Uqul*, mlango wa mawaidha ya Nabii na hekima zake.

## Elimu ni uhai wa nyoyo:

Mtume (s.a.w.w.) alijali sana elimu na maarifa akabainisha nafasi ya elimu na jukumu lake katika maisha akasema: "Kutafuta elimu ni faradhi kwa kila mwisilamu. Fuateni elimu toka kila sehemu mnayodhani mtaipata. Jifunzeni toka kwa wenyenayo hakika kujifunza kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni wema na kuitafuta ni ibada, kujikumbusha elimu hiyo ni tasbihi na kuitumia ni jihadi, kumfunza yule asiyejua ni sadaka na kuieneza kwa wahusika ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa sababu elimu ndio alama ya halali na haramu, na minara ya watu wa peponi na ndio mfariji wakati wa upweke na rafiki wakati wa ugeni na upweke, na ndio msemeshaji wakati wa siri na upekee. Ni alama ijulishayo mambo ya siri na ya kudhuru, ni silaha dhidi ya maadui, na ni pambo kwa vipenzi.

Mwenyezi Mungu huwainua watu kupitia elimu, hivyo huwafanya viongozi bora ambao athari zao hunufaisha na vitendo vyao hufuatwa, mawazo yao hutegemewa huku malaika wakipenda urafiki wao, huwapangusa kwa mbawa zao na huwabariki katika Swala zao. Kila kibichi na kikavu huwaombea msamaha. Pia viumbe vya baharini na nchi kavu, kuanzia vidogo hadi vikubwa navyo huwaombea msamaha.

Hakika elimu ni uhai wa moyo dhidi ya ujinga na ni nuru ya macho dhidi ya kiza na ni nguvu ya mwili dhidi ya udhaifu. Humfikisha mja nafasi ya wenye heri na vikao vya watu wema na daraja la juu hapa duniani na huko Akhera. Kuitaja tu huwa sawa na kufunga, na kuisoma ni sawa na kusali Swala za usiku. Kupitia elimu Mola hutiiwa na undugu huunganishwa na haramu na halali hujulikana. Elimu huwa mbele ya vitendo na vitendo hufuata elimu. Mwenyezi Mungu huwa-

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 64



pa watu wema na huwanyima waovu, hivyo ni jambo zuri sana kwa yule ambaye hajanyimwa na Mwenyezi Mungu fungu lolote la elimu. Sifa ya mwenye akili ni kumvumilia asiyejua na kumsamehe aliyemdhulumu, kumnyenyekea aliye chini yake na kushindana katika kutafuta wema dhidi ya yule aliye juu yake.

Anapotaka kuzungumza, kwanza hufikiri hivyo kama ni la heri huzungumza na kufaidika, na kama ni la shari hunyamaza na kusalimika. Iwapo utamfika mtihani hushikamana na Mwenyezi Mungu na huzuia mkono na ulimi wake. Aonapo jambo bora hulichangamkia na hapo aibu haimzuii wala tamaa haimpeleki pupa. Basi hizo ndio sifa kumi hujulikana kwazo mtu mwenye akili.

Sifa ya mjinga ni kumdhulumu anayechanganyikana naye, kumdhulumu aliye chini yake, kumfanyia kiburi aliye juu yake. Huongea bila kufikiri, na akiongea hutenda dhambi na akinyamaza husahau. Iwapo utamfika mtihani basi huuendea pupa na kumcharua. Huwa mzito aonapo jambo la heri huku akijitenga nalo, hana khofu dhidi ya dhambi zake za mwanzo wala hatetemeki dhidi ya umri wake uliyobaki na dhambi alizonazo. Huwa mzito na mwenye kuchelewa dhidi ya jambo la heri. Hasikitikii heri yoyote iliyompita au aliyoipoteza. Hizo ni sifa kumi za mjinga ambazo akili imenyimwa."[127]

## Vizito viwili: Kitabu na Kizazi (Ahlul-Bayt):

Mtume (s.a.w.w.) aliwachorea watu njia ya wema wa kweli akawapa dhamana ya kuufikia wema huo iwapo tu watashikamana kwa ukamilifu na mafunzo aliyoyabainisha, hivyo akawapa ufupi wa njia

127 Ameipokea ndani ya kitabu Maniyyatul-Murid kutoka kwa Imam Ridhaa (a.s.) kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Tazama hadithi hii kwa urefu ndani ya kitabu *Tuhful-Uqul*.

ya wema ambayo inawakilishwa na kitendo cha kushikamana na asili na misingi miwili ambayo hutegemeana nayo ni: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi chake, Akasema:

"Enyi watu, hakika mimi nawatangulia nanyi mtanikuta katika hodhi. Fahamuni kuwa mimi nitawauliza kuhusu vizito viwili, hivyo angalieni jinsi gani mtahusika navyo baada yangu. Hakika Mpole mtoa habari amenipa habari kuwa: Hakika hivyo viwili havitoachana mpaka vinikute. Nilimwomba Mola Wangu hivyo na akanipa. Fahamuni hakika mimi nimewaachieni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu Ahlul-Bayt, hivyo msiwatangulie mtafarikiana, wala msiwaache mtaangamia na wala msiwafunze hakika wao ni wajuzi zaidi yenu. Enyi watu! Msiwe makafiri baada yangu ikawa baadhi yenu wanawauwa wengine hivyo mkanikuta huku mkiwa kundi dogo kama mfereji wa maji uliyoacha njia. Fahamuni kuwa Ali bin Abu Talib ni ndugu yangu na wasii wangu, atapigania tafsiri ya Qur'ani baada yangu kama nilivyopigania uteremkaji wake."[128]

## Mawaidha fasaha:

Mtume (s.a.w.w.) ambaye mwenendo wake ni fasaha tupu ana semi fupifupi ambazo ni alama ya ufasaha wake, hivyo miongoni mwa mawaidha yake ni:

"Enyi watu, mazungumzo ya kweli kabisa ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na shikio imara ni neno la uchamungu, na mila bora kabisa ni mila ya Ibrahim, na mwenendo bora kabisa ni mwenendo wa Muhammad, na mazungumzo matukufu kabisa ni kumtaja Mwenyezi Mungu.

128 *Nasikhut-Tawarikh*, Juz. 3. Rejea ufafanuzi wa hotuba hii ndani ya kitabu *Tarikh Yaaqubiy*, Juz. 2 Uk. 109.

“Visa vizuri sana ni visa vya Qur’ani, mambo bora ni maamrisho na mambo mabaya ni bidaa. Uongofu bora kabisa ni uongofu wa manabii, kifo bora ni kifo cha mashahidi, upofu zaidi ni kupotea baada ya kuongoka. Kazi bora ni ile yenye kunufaisha, na uongofu bora ni ule wenye kufuatwa. Upofu mbaya ni upofu wa moyo, na mkono wa juu ni bora kuliko mkono wa chini. Kichache kinachotosheleza ni bora kuliko kingi kisichofaa.

“Msamaha mbaya ni ule uombwao wakati kifo kimefika na majuto mabaya ni majuto ya siku ya Kiyama. Kati ya makosa makubwa ya ulimi ni uongo. Utajiri bora ni utajiri wa nafsi na maandalizi bora ya safari ni uchamungu. Msingi wa busara ni kumwogopa Mwenyezi Mungu na jambo bora uliyopewa moyo ni yakini. Kilevi husababisha moto, na pombe ni mkusanyiko wa mikasa yote. Wanawake ni kamba za ibilisi na ujana ni tawi la uwendawazimu.

“Chumo baya zaidi ni riba, na chakula kibaya zaidi ni kula mali ya yatima. Mwema ni yule anayewaidhika kupitia mwenzake. Hakika kila mmoja wenu atawekwa ndani ya dhiraa nne (Kaburini). Kipimo cha vitendo ni mwisho wake na kila lijalo basi liko karibu. Kumtukana muumini ni ufasiki na kumuua ni ukafiri. Kumla nyama yake (kumsengenya) ni maasi na mali yake imeharamishwa kama ilivyoharamishwa damu yake.

“Atakayemuomba Mwenyezi Mungu msamaha basi Mwenyezi Mungu atamsamehe. Atakayesamehe basi Mwenyezi Mungu atamsamehe na atakayevumilia katika msiba basi Mwenyezi Mungu atampa badala.”[129]

129 *Al-Bidayatu Wan-Nihayah*, Juz. 5 Uk. 13, chapa ya Darul-fikri

## Muhtasari:

Mtume (s.a.w.w.) ni mfano hai wa ukamilifu wa mwanadamu. Pia urithi wake ndio wenye thamani baada ya Qur'ani. Hakika yeye alikunywa toka chemchemu ya ufunuo mpaka akabubujisha ukamilifu wake kwa wanadamu kwa kiwango kinachotosheleza kuwapeleka wanadamu mbele upande wa ukamilifu na kuwafikisha kileleni mwa ukamilifu.

Tumechagua mifano ya ufasaha wake na semi zake fasihi kuhusu akili, elimu na njia ya kufikia wema na ukamilifu. Tumechagua kwa kiwango ambacho kitawaangazia wenye kufuata njia yake, hivyo wale watafuta ukweli hawatojizuia kutumia madhumuni ya semi hizo.

## Maswali:

1. Akili ni nini? Na ina nafasi gani katika maisha ya mwanadamu?

2. Ni kipi kinachotokana na akili. Taja sifa ambazo haziachani na akili?

3. Tunatafuta elimu kutoka wapi? Na ni zipi hatua za utafutaji elimu?

4. Ni ipi nafasi ya elimu katika maisha ya mwanadamu?

5. Ni vipi hivyo vizito viwili? Na kila kimoja kina mahusiano gani na kingine?

6. Ni zipi sifa mahsusi za Qur'ani?

7. Ni ipi nafasi ya kizazi cha Mtume kwa Mtume (s.a.w.w.)?

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 68



# Somo la tisa

## Dondoo za maisha ya mbora wa mawasii

**Kiongozi wa waumini Ali bin Abu Talib**

Baada ya kifo cha nabii wa mwisho Muhammad (s.a.w.w.) uongozi wa Mwenyezi Mungu unaendelea kwa mawasii kumi na wawili toka kizazi chake. Kizazi ambacho Mwenyezi Mungu alikitakasa na kukiondolea uchafu nao ni Maimam wema waongozaji upande wa haki na makhalifa wema ambao Mtume (s.a.w.w.) aliwaacha pamoja na Qur'ani tukufu. Akauambia umma wake ushikamane navyo pamoja ili wapate mafanikio na wema hapa duniani na kesho Akhera. Imam Ali bin Abu Talib (a.s.) ndiye Imam wa kwanza kati ya Maimam viongozi wema na kati ya makhalifa wa Mwenyezi Mungu na watawala Wake katika ardhi Wake.

Mtume (s.a.w.w.) alitoa maelezo juu ya uimamu wake,[130] hiyo ni baada ya kumlea yeye mwenyewe na kumpandikiza elimu yake, sifa zake nzuri na maadili yake mazuri. Akafahamika kwa kufuata haki, jihadi yake, kujitolea kwake, kumwabudu Mwenyezi Mungu na kupenda kuhami ujumbe wa Mola Wake. Hivyo akamkabidhi jukumu baada ya kuubainishia umma jinsi yeye anavyostahiki na kufaa cheo hiki cha uwasii na uongozi. Alibainisha hayo tangu mwanzo wa utume wake uliobarikiwa.

Imam Ali aliwatangulia maswahaba wote katika kuukubali ujumbe wa Mwenyezi Mungu huku akiwatangulia ndugu wote wa karibu wa

130 *Al-Muraj'ati* cha Sayyid Abdul-Husayn Sharafudin, namba 20 na 68.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 69



Mtume (s.a.w.w.) katika kumsaidia Mtume (s.a.w.w.).[131] Akamhami katika kipindi chote cha zama za Makka.[132] Akalala kitandani kwa Mtume (s.a.w.w.) usiku wa kuhama[133] huku akifidia nafsi yake dhidi ya nafsi ya Mtume (s.a.w.w.). Aliendelea kuuhami Uislamu kipindi chote cha miaka yote ya matatizo[134] huku akitii amri za Mtume katika kila jambo na kila sehemu.

## Kukua kwa Imam Ali bin Abu Talib na hatua za maisha yake

### Nasaba yake ing'aayo:

Imam Ali (a.s.) ametokana na kuzaliwa na wazazi wawili watukufu watakasifu ambao hawajachafuliwa na shirki wala uchafu wa kijahiliya. Imam Ali (a.s.) amesema: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu baba yangu wala babu yangu Abdul Muttalib wala Hashim wala Abdul Manafi katu hawakuabudu sanamu……. Walikuwa wakiswali wakielekea Al-Kaaba kwa kufuata dini ya Ibrahim huku wakishikamana nayo.[135] Hivyo baba ni Abu Talib na jina lake ni Abdu Manafi. Babu ni Abdul Mutalib na jina lake ni Shaybatul-hamdi. Babu wa

131 *Taarikh Tabariy*, Juz. 2, Uk. 403. *Ihqaqul-Haqi*, Juz. 4 Uk. 58-70. *Shawahidut-Tanziil*, Juz. 1, Uk. 420.

132 *Al-Manaqib* cha Shahru Ashuub, Juz. 2, Uk. 65. *Aayanus-Shia*, Juz. 1, Uk. 372.

133 *Al-Mustadraku alas-Sahihayni*, Juz. 3, Uk. 4. *Biharul-An'war*, Juz. 19, Uk. 28.

134 Imam Ali alishiriki vita vyote kasoro vita vya Tabuk, kwa mfano tu rejea kitabu *Al-Manaqib*, Juz. 2, Uk. 81. *Qadatuna*, Juz. 2, Uk. 78-148.

135 Tazama *Imam Abu Talib* cha Fakhar bin Muidu Al-Musawiy. *Al-Ghadiri* ya Amini, Juz. 7, Uk. 330.

baba yake ni Hashim na jina lake ni Amru mtoto wa Abdu Manafi na jina lake ni Al-Mughira mtoto wa Quswayyi mtoto wa Kilabi mtoto wa Murrat mtoto wa Luayyi mtoto wa Ghalib mtoto wa Fahri mtoto wa Malik mtoto wa An-Nadhar mtoto wa Kinanat mtoto wa Khuzaymat mtoto wa Mudrikat, mtoto wa Iliyasa, mtoto wa Mudhar, mtoto wa Nazar, mtoto wa Maaddi, mtoto wa Adinan. Adinan anatokana na Ismail mtoto wa Ibrahim kipenzi cha Mwenyezi Mungu."

Abu Talib ni mdogo wa Abdullah mzazi wa Mtume (s.a.w.w.) kwa baba na mama. Alimlea Mtume (s.a.w.w.) utotoni mwake huku akimnusuru ukubwani, akamtetea na kumlinda huku akivumilia maudhi toka kwa mushrikina wa kiquraishi huku akimlinda dhidi yao. Hivyo kwa ajili yake akapatwa na matatizo makubwa huku akikumbana na misukosuko mikali lakini akavumilia katika kumnusuru na kusimamisha jambo lake mpaka maquraishi wakakata tamaa dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) kwani walikuwa wameshindwa mpaka alipofariki Abu Talib.

Hakuamrishwa kuhama isipokuwa baada ya kufariki Abu Talib. Abu Talib alikuwa muislamu asiyedhihirisha Uislamu wake, kwani laiti angekuwa akidhihirisha basi asingeweza kumnusuru Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kikamilifu kama alivyomnusuru. Zaidi ya hapo ni kuwa Abu Talib alikubali usahihi wa unabii wa Mtume (s.a.w.w.) mara nyingi katika mashairi yake mfano kauli yake: "Ukanilingania nami nikajua kuwa wewe ni mkweli. Umesema kweli na kabla ya hapo ulikuwa mwaminifu. Nilijua kuwa dini ya Muhammad ni dini bora kati ya dini zote za mwanadamu".[136]

Mama yake ni Fatima binti Asad bin Hashim bin Abdul Manafi bin Quswayyi.Yeye ndiye binti wa kwanza toka familia ya Hahim aliyezaa na kijana wa familia ya Hashim. Imam Ali (a.s.) alikuwa

136 *Aayanus-Shia*, Juz. 1, Uk. 324.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 71



ndiye mtoto wake mdogo kati ya watoto wake ambao ni Jafar, Aqil na Talib. Mama yake aliukubali Uislamu baada ya watu kumi wa mwanzo. Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akimkirimu na kumtukuza huku akimwita: Mama yangu. Na alipokaribiwa na umauti alimuusia Mtume (s.a.w.w.) na Mtume akakubali usia wake na hivyo akamsalia na kumshusha ndani ya mwanandani na kumlaza humo, hayo ni baada ya kumvisha kanzu yake (ya Mtume). Hapo maswahaba zake wakamwambia: "Hatujaona ukifanya kwa yeyote mfano wa uliyofanya kwake." Akajibu: "Hakuna mtu aliyekuwa mwema kwangu baada ya Abu Talib zaidi yake. Hakika nimemvisha kanzu yangu ili avishwe mapambo ya peponi, na nimemlaza na kanzu hiyo ili uzito wa kaburi uwe mwepesi kwake."[137]

Al-Mufid na At-Tabariy wameongeza kuwa: "Mtume (s.a.w.w.) alimtamkisha akiri utawala wa mwanae Ali (a.s.). Riwaya hiyo ni maarufu.[138] Na yeye ndiye mwanamke wa kwanza aliyetoa kiapo cha utii kwa Mtume wa Mwenyezi Mumgu (s.a.w.w.) kati ya wanawake wote.[139]

## Kuzaliwa kwake kulikobarikiwa:

Mashuhuri ni kuwa alizaliwa Makka ndani ya Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu (Al-Kaaba), siku ya Ijumaa, siku ya kumi na tatu ya mfungo kumi (Rajab) mwaka wa thelathini tangu kutokea kwa tukio la mwaka wa tembo.[140]

Al-Hakim An-Nisabury amesema: "Zimeenea habari kuwa Fatima binti Asad alimzaa kiongozi wa waumini Ali bin Abu Talib ndani ya

137 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz. 1, Uk. 13-14.
138 *Al-Ir'shadi*, Juz. 1, Uk. 5. *Iilamul-Waraa*, Juz. 1, Uk. 306.
139 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz. 1, Uk. 13-14.
140 *Al-Ir'shadi*, Juz. 1, Uk. 5.

Al-Kaaba."[141]

Al-Mufid na wenzake wamesema: "Hakuzaliwa yeyote yule ndani ya Al-Kaaba kabla yake wala baada yake. Mwenyezi Mungu alifanya hivyo kwa ajili ya kumpa heshima na kutukuza nafasi yake."[142]

Mama wa Ammarat binti Ubadat amesema: "Abu Talib alimshika mkono Fatima binti Asad akaenda naye Kaaba kisha akamwambia: "Kaa kwa jina la Mwenyezi Mungu," hapo akapatwa na uchungu kisha akajifungua kijana mwenye furaha msafi aliyesafika ambaye sijamwona mwingine kwa uzuri wa uso wake. Hapo akamwita jina, Ali, na Mtume (s.a.w.w.) akambeba mpaka nyumbani kwa Fatima."[143]

## Kupewa jina na lakabu zake:

Ibnu Abul-Hadid na wenzake wamesema: "Hakika jina lake la kwanza aliloitwa na mama yake ni Haydar (Simba) likiwa ni jina la babu yake, yaani baba wa mama yake Asad (Simba) bin Hashim. Ndipo baba yake akambadili jina na kumwita Ali."[144]

Mtume (s.a.w.w.) akampa kuniya ya Abu-Turab, hiyo ni baada ya kumuona yuko katika hali ya sijida huku uso wake umo ndani ya udongo. Jina hili ndilo alilolipenda sana yeye mwenyewe.[145]

141 *Al-Mustadrak alas-Sahihayn*, Juz. 3, Uk. 483.

142 *Al-Ir'shadi*, Juz. 1, Uk. 5. *Al-Fusulul-Muhimmah*, Uk. 30.

143 *Kashful-Ghummah*, Juz. 1, Uk. 59 na 60.

144 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz. 1, Uk. 12. *Kashful-Ghummah*, Juz. 1, Uk. 61.

145 *Iilamul-Waraa*, Juz. 1, Uk. 307. *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz. 1, Uk. 11.

Mwanawe Hasan (a.s.) wakati wa uhai wa Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akimwita baba Husain. Huku mwanae Husain akimwita baba Hasan. Pia aliitwa baba wa wajukuu wawili na baba wa manukato mawili. Mtume alimpa lakabu ya: Kiongozi wa waumini (*Amirul-Mu'minin*), huku muhajirina na ansari wakimwita kwa lakabu hiyo.[146]

Pia alipewa lakabu ya Mteule {*Al-Murtadha*}, walii wa Mwenyezi Mungu, kipenzi cha Mwenyezi Mungu, wasii wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Simba wa Mwenyezi Mungu, upanga wa Mwenyezi Mungu, ndugu wa Mtume, bwana wa waarabu, kijana wa kiquraishi, mgawa pepo na moto, Lango wa Jiji la Elimu, bwana wa waislam, jemedari wa waumini, kiongozi wa kundi mashuhuri, Imam wa wachamungu na mkweli mno.

Baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.) lakabu yake mashuhuri ilikuwa ni wasii.[147] Lakabu hii ilikuwa mashuhuri kwake tangu mwanzo, hivyo ikaenea sana mpaka ikachukua nafasi ndani ya vitabu vya lugha mfano: *Lisanul-Arab*, *Tajul-Urus* na vinginevyo. Wasomi (Baadhi) wa kisunni walijitahidi sana kutaka kuficha habari za uwasii wake na kutaka kuleta tafsiri nyingine kinyume na ile iliyoenea.[148]

## Malezi na makuzi yake:

Haraka sana Mtume (s.a.w.w.) alimtilia umuhimu maalumu Imam Ali bin Abu Talib (a.s.), alimpenda sana na kumwambia mama yake: "Weka kitanda chake karibu na kitanda changu." Mtume alikuwa

146 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz. 1, Uk. 12, 13, 143.
147 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz. 1, Uk. 12, 13, 143.
148 Tazama kitabu *Maalim Madrasatayn*, Juz. 1 Uk. 295 – 340, chapa ya tano.

akitawala sana malezi yake, hivyo alikuwa akimtoharisha Ali wakati wa kuogeshwa na akimuwekea maziwa mdomoni wakati wa kunywa maziwa. Alichezesha kitanda chake wakati wa kulala huku akimbembeleza awapo macho. Akimbeba kifuani kwake na shingoni huku akisema: "Huyu ni ndugu yangu, walii wangu, mwenye kuninusuru, mteule wangu, tegemeo langu, kinga yangu, mkwe wangu, wasii wangu, mme wa binti yangu, wasii wangu na khalifa wangu mwaminifu". Daima alikuwa akimbeba na kuzunguka nae katika milima na mabonde ya Makka.[149]

Imam Ali (a.s.) yeye mwenyewe amefafanua makuzi yake ya mfano ambayo yamejaa heshima kwa kiwango cha juu, akasema katika hotuba yake kuwa: "Mnajua nafasi yangu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ukaribu wa karibu na nafasi mahsusi niliyonayo kwake. Alinilea nikiwa mtoto akinikumbatia kifuani mwake na kitandani kwake. Akinigusisha mwili wake, akininusisha harufu yake. Alikuwa akitafuna kitu kisha akinilisha, hakupata uongo wa kauli yoyote toka kwangu, wala kosa lolote la kitendo.

Nilikuwa nikimfuata kama mtoto aliyeachishwa ziwa amfatavyo mama yake, huku kila siku akiniinua juu kwa kuniongezea sehemu ya maadili yake huku akiniamrisha kumfuata. Kila mwaka alikuwa akienda pango la Hira hakuna anayemuona isipokuwa mimi tu. Wala hakuna nyumba hata moja kipindi hicho iliyokuwa imekusanya waislam wasiyokuwa Mtume, Khadija na mimi nikiwa watatu wao, nikiona nuru ya wahyi na utume huku nikinusa harufu ya unabii.

Nilisikia mlio wa shetani pindi wahyi ulipomshukia Mtume, nikasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni sauti ya nini hii?" Akajibu: "Huyu ni shetani amekata tamaa dhidi ya kuabudiwa, haki-

149 *Kashful-Ghummah*, Juz.1, Uk. 60.

ka wewe unasikia ninayosikia na unaona nionayo isipokuwa wewe si nabii lakini wewe ni waziri na hakika wewe upo juu ya heri."[150]

### Hatua za maisha yake:

Kuanzia alipozaliwa mpaka Mtume (s.a.w.w.) alipopewa utume, nacho ni kipindi cha miaka kumi.

Kisha kipindi cha miaka kumi kuanzia alipopewa Mtume (s.a.w.w.) utume mpaka alipohama.

Kisha kipindi cha miaka kumi mpaka alipofariki Mtume (s.a.w.w.).

Kisha miaka ishirini na tano mpaka kumalizika utawala wa Uthmani.

Kisha miaka mitano ambayo ndio muda wa serikali yake.

## Muhtasari:

Ali bin Abu Talib (a.s.) alitokana na asili ile ile aliyotokana nayo Mtume (s.a.w.w.) hivyo nasaba yake na nasaba ya Mtume (s.a.w.w.) ni moja.

Ali (a.s.) alitofautiana na maswahaba wengine kwani hakuna shirki yoyote iliyomuingia. Kisha akawa ni mtu mahsusi kwa Mtume (s.a.w.w.) hivyo akawa akimfunza mafunzo yatokanayo na hekima za Mwenyezi Mungu na elimu ya Mola Wake, jambo ambalo hakulipata swahaba mwingine yeyote.

Ali (a.s.) alidhihirisha utiifu na ufuataji kamilifu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w.), akajipamba kwa

150 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 192.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 76



maadili mazuri, akajitolea nafsi na kila lenye thamani kwa ajili ya itikadi ya Uislamu.

Mwenyezi Mungu alimteua awe wasii wa Mtume Wake (s.a.w.w.) hivyo akasimamia jukumu la uwasii kwa ukamilifu mpaka adui akakiri hilo kabla ya rafiki.

Imam Ali (a.s.) alibeba majina na lakabu nzuri ambazo zinaonyesha jinsi alivyoshikamana sana na Mwenyezi Mungu na alivyokuwa na itikadi salama ya Mwenyezi Mungu na maadili bora mazuri.

## Maswali:

1. Ni jukumu gani ambalo Mtume (s.a.w.w.) alimpa Imam Ali (a.s.) baada yake?

2. Ni kitu gani kinachomtofautisha Imam Ali (a.s.) na maswahaba wengine wa Mtume (s.a.w.w.)?

3. Elezea jinsi gani Imam Ali (a.s.) alivyokuwa Khalifa wa Mtume (s.a.w.w.) na wala si mwingine?

4. Ni uhusiano gani wa kinasaba uliyopo kati ya Mtume Muhammad na Imamu Ali?

5. Ni karama zipi ambazo Mwenyezi Mungu alimfadhilisha kwazo Imam Ali (a.s.) wakati wa kuzaliwa kwake? Andika riwaya na yote unayoweza kuyapata ndani ya riwaya hiyo.

6. Kwa nini jina la Abu Turab ndilo alilolipenda sana Imam Ali?

7. Imam Ali (a.s.) aliishi na Mtume (s.a.w.w.) miaka mingapi?

# Somo la kumi

## Mwonekano wa utu wa Imam Ali bin Abu Talib (a.s.)

Sifa za ukamilifu zilikusanyika kwa Imam Ali bin Abu Talib. Alikuwa na sifa nzuri za kusifika, mahsusi za kupendeza, nasaba bora na sharafu tukufu, asili takatifu na nafasi yenye kuridhiwa. Sifa ambazo hakubahatika kuzipata mtu yeyote mwingine, kwani yeye ni jemedari wa waumini, mbora wa mawasii na khalifa wa kwanza wa Mtume (s.a.w.w.) kati ya makhalifa waongozao kwa amri ya Mwenyezi Mungu.

Maelezo ya Mtume (s.a.w.w.) na Qur'ani tukufu vimeeleza wazi kuhusu umaasumu wake dhidi ya kila uchafu.[151] Mtume (s.a.w.w.) akaapizana na wakristo wa Najran kupitia yeye, mkewe, na wanawe wawili.[152] Pia alimfanya ni kati ya ndugu zake wa karibu ambao tumewajibishwa kuwapenda[153] huku mara kwa mara Mtume (s.a.w.w.) akitueleza wazi kuwa wao ni sawa na Kitabu kitukufu,[154] hivyo huokoka yule atakayevishika viwili hivyo na huangamia yule atakayeviacha.

Imam Ali bin Abu Talib (a.s.) aliishi zama za Mtume (s.a.w.w.) na utume, kuanzia pale ufunuo ulipoanza kushuka mpaka ulipokatika kwa kufariki Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) huku akiwa na nafasi ya juu ambayo hutamaniwa. Nayo ni katika kumhami Mtume (s.a.w.w.) na utume muda wote wa miaka ishirini na tatu, ikiwa ni

151. Al-Ahzab: 33.

152. Al Imran: 61.

153. Shuraa: 23.

154 Tazama hadithi ya vizito viwili katika somo la nane.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 78



jihadi yenye kuendelea na mapambano endelevu ya kuhami Uislamu na tukufu zake. Hivyo misimamo yake, utendaji wake na sifa zake vimejiakisi katika Aya za Kitabu kitukufu na maelezo ya hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Ibnu Abbas amesema: "Ziliteremka Aya mia tatu kuhusu fadhila za Ali (a.s.),[155] hakuna Aya iliyoteremka na ibara ya: "Enyi mlioamini" isipokuwa Ali (a.s.) ndio kiongozi na mlengwa wa mwanzo katika Aya hiyo.[156] Hakika Mwenyezi Mungu amewalaumu wafuasi wa Muhammad katika baadhi ya Aya za Qur'ani lakini hakumtaja Ali (a.s.) isipokuwa kwa heri."[157]

Kutokana na kukithiri Aya zilizoteremka kuhusu fadhila za Ali (a.s.) baadhi ya wasomi wa zamani wameandika vitabu mahsusi ambavyo vimekusanya Aya zilizoteremshwa kwa ajili yake. Hivyo hapa tutaashiria baadhi ya Aya ambazo wanahadithi wameeleza wazi kuwa ziliteremshwa kwa ajili yake.

Imepokewa kutoka kwa Ibnu Abbas kuwa: "Ali (a.s.) alikuwa na dirhamu nne tu huku akiwa hana nyingine, hivyo usiku akatoa sadaka dirhamu moja, mchana dirhamu moja, na dirhamu nyingine akaitoa sadaka kwa siri na nyingine kwa dhahiri, hapo Mwenyezi Mungu akateremsha Aya isemayo: "Wale watoao mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, basi wana malipo yao kwa Mola wao, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika."[158]
Ibnu Abbas amesema: "Ali (a.s.) alitoa sadaka pete yake huku akiwa

155 *Al-Futuhatl-Islamiyyah*, Juz. 2, Uk. 516. *Tarikh Baghdad*, Juz. 6, Uk. 221. *Sawaiqul-Muhriqah*, Uk. 76. Pia tazama kitabu *Shawahidut-Tanzil na Nurul-Abswar*, Uk. 87 – 90.

156 *Kashful-Ghummah*, Uk. 93.

157 *Yanabiul-Mawadda*, Uk. 93.

158 Al-Baqarah: 274. Rejea kitabu *Yanabiul-Mawadda*, Uk. 93.

katika hali ya rukuu. Mtume (s.a.w.w.) akamuuliza mwombaji: "Ni nani aliyekupa pete hii?" Akajibu: "Ni yule aliye katika hali ya rukuu, hapo Mwenyezi Mungu akateremsha Aya isemayo: "Hakika kiongozi wenu khasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka na hali ya kuwa wamerukuu."[159]

Aya ya utakaso[160] imemfanya Ali (a.s.) kuwa kati ya Ahlul-Bayt wa Mtume (s.a.w.w.) ambao wametakaswa dhidi ya kila uchafu, huku Aya ya maapizano[161] ikimfanya kuwa nafsi ya Mtume (s.a.w.w.).

Ama Sura Insan imeashiria ukunjufu wa moyo aliyonao Ali (a.s.) na watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) na jinsi wanavyomwogopa Mwenyezi Mungu. Pia imebeba ushahidi wa Mwenyezi Mungu kuthibitisha kuwa wao ni watu wa peponi.[162] Waandishi wa vitabu Sahihi sita na wengineo miongoni mwa wanazuoni wa hadithi wametenga milango mahsusi ndani ya vitabu vyao inayoelezea fadhila za Imam Ali (a.s.) kupitia hadithi za Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Wanadamu ndani ya historia yao ya muda mrefu hawajamwona mtu bora kuliko Ali (a.s.) baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.). Wala hakuna mtu ambaye fadhila zake zimeandikwa kama zilivyoandikwa fadhila za Imam Ali (a.s.). Japokuwa muda wote wa utawala wa kizazi cha Umayya maadui na wanafiki walimwelekezea matusi na kashfa juu ya mimbari zao wakiwa na lengo la kumtia

159 Al-Maidah: 55. Rejea kitabu *Tafsir Tabari*, Juz. 6, Uk 156. Na *Tafsir Al-Baydhawiy*.

160 Al-Ahzab: 33. Rejea *Sahihi Muslim*, fadhila za maswahaba.

161 Al Imran: 61. *Sahihi Tirmidhiy*, Juz. 2, Uk. 300.

162 *Al-Kashafu* cha Az-Zamakhshar. *Ar-Riyadh an-Nadhrah* cha Tabariy, Juz. 2, Uk. 207.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 80



dosari, lakini hawakupata sehemu yoyote kwake yenye dosari na aibu.

Kati ya kauli za Umar bin Al-Khatab ni: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema: 'Hakuchuma mchumaji mfano wa fadhila za Ali, kwani yeye humwongoza mfuasi wake kwenye uongofu na humzuwia dhidi ya maangamio."[163]

Imam Ali (a.s.) aliulizwa: "Kwa nini wewe una Hadithi nyingi kuliko maswahaba wengine wa Mtume (s.a.w.w.)?" Akajibu: Hakika mimi nilikuwa nimuulizapo ananijibu, na ninyamazapo hunianza".[164]

Imepokewa kutoka kwa Ibnu Umar kuwa: Siku Mtume (s.a.w.w.) alipounga undugu kati ya maswahaba zake, Ali alikuja huku macho yake yakidondoka machozi, hapo Mtume (s.a.w.w.) akamwambia Ali (a.s.): "Wewe ni ndugu yangu hapa duniani na kesho Akhera."[165]

Imepokewa kutoka kwa Abu Layla Al-Ghaffariy kuwa alisema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akisema: "Baada yangu itatokea fitina, basi ikitokea hali hiyo shikamaneni na Ali bin Abu Talib, hakika yeye ndiye wa kwanza kuniamini, na ndiye wa kwanza atakayenipa mkono siku ya Kiyama, yeye ni mkweli mno, na yeye ndiye atakayefarakisha kati ya haki na batili ya umma huu, yeye ndiye jemedari wa waumini na mali ndio jemedali wa wanafiki."[166]
Makhalifa wote wamekiri kuwa Ali (a.s.) ndiye mjuzi zaidi kuliko

163 *Ar-Riyadh an-Nadhrah* cha Tabariy, Juz. 1, Uk. 166.

164 *Tabaqat* cha Ibnu Saad, Juz. 2 Uk. 338. *Hilyatul-Awliyai*, Juz. 1, Uk. 68.

165 *Sunan Tirmidhiy*, Juz. 5 Uk 595, hadithi ya 3720.

166 *Al-Isabat* cha Ibnu Hajar, Juz. 4, Uk. 171, namba 994. *Majmauz-Zawaid*, Juz. 1, Uk 102.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 81



maswahaba wote na ndiye anayefahamu sheria zaidi kuliko maswahaba wote, na kuwa laiti si Ali (a.s.) basi wangeangamia, mpaka ikafikia kauli ya Umar kuwa mfano halisi, nayo ni: "Laiti kama si Ali Umar angeangamia."[167] Imepokewa kutoka kwa Jabir bin Abdullah Al-Answar kuwa alisema: "Tulikuwa hatuwatambui wanafiki isipokuwa kwa kumchukia Ali bin Abu Talib (a.s.)."

Zilipomfikia Muawiya habari za kuuwawa Ali (a.s.) alisema: "Sheria na elimu yote imeondoka kwa kifo cha mwana wa Abu Talib."[168]

As-Shaabiy amesema: "Ali bin Abu Talib ndani ya umma huu ni sawa na Masihi mwana wa Mariam kwa wana wa Israel: Kuna kundi lililompenda mpaka likakufuru ndani ya mapenzi yake, na kundi lingine likamchukia hivyo likakufuru kwa kumchukia."[169] Alikuwa mkarimu sana. Alikuwa na maadili ayapendayo Mwenyezi Mungu katika ukarimu, katu hakuwahi kumjibu mwombaji hapana sina.[170]

Swaa'swaa' bin Swawhan alimwambia Ali bin Abu Talib siku aliyopewa kiapo cha utii kuwa: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu ewe kiongozi wa waumini! Hakika umeupamba ukhalifa lakini wenyewe haujakupamba, umeuinua lakini wenyewe haujakuinua, na wenyewe unakuhitajia sana kuliko wewe unavyouhitajia."

Ibnu Shabramat amesema: "Hakuna mtu yeyote asiyekuwa Ali bin Abu Talib mwenye uwezo wa kusema juu ya mimbari: 'Niulizeni.'"[171]
Qaaqaa bin Zararat alisimama kaburini kwa Imam Ali (a.s.) kisha

167 *Sharhu Nahjul-Balagha*, Juz. 1, Uk. 6. *Tadhkiratul-Khuwas*, Uk. 87.
168 *Al-Istiab* pambizoni mwa *Al-Isabat*, Juz. 3, Uk. 45.
169 *Al-Aqdu Al-Farid*, Juz. 2, Uk. 216.
170 *Sharhu Nahjul-Balaghah*, Juz. 1, Uk. 7.
171 - Aayanus-Shia, Juz. 3, kifungu cha 1 Uk. 103

akasema: "Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako ewe kiongozi wa waumini, naapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa hakika uhai wako ulikuwa ni ufunguo wa kheri, na laiti watu wangekukubali basi wangekula toka juu yao na toka chini ya miguu yao, lakini wao wameidharau neema na wakaijali sana dunia."[172]

## **Muhtasari**:

Imam Ali (a.s.) alijitenga kwa kuwa na sifa mahsusi ambazo zilimtofautisha na maswahaba wengine, zikamwajibisha awashinde wote waliotaka kulingana nae miongoni mwa maswahaba na wasiokuwa maswahaba. Aya za Qur'ani zimejaa fadhila hizi za pekee huku maelezo ya Mtume (s.a.w.w.) yakiashiria sifa hizi zilizomtofautisha Ali (a.s.) na wengine.

Ushahidi wa maswahaba na waliokuja baada ya maswahaba unaashiria undani wa fadhila za Ali (a.s.) ndani ya umma huu japokuwa watu wengi hawakufuata uimamu wa mtu huyu mtukufu.

## Maswali:

1. Taja alama za utu wa Imam Ali (a.s.) katika nyanja za: Elimu, sheria, imani, ushujaa, ujasiri, ukaribu wake na Mtume (s.a.w.w.), haiba, unyenyekevu na kutoipenda dunia kama alivyoonekana na wenzake?

2. Je unaweza kutoa sura halisi kuhusu jinsi utu wa Imam Ali (a.s.) ulivyoathiri katika safari ya tablighi ya Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa mtazamo wa wenzake?

3. Ikiwa fikira na rai zote zinamsifu Imam Ali (a.s.), basi ni kwa nini

172 *Tarikh Yaaqubiy*, Juz. 2, Uk. 213.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 83



hakupewa haki yake?

4. Taja Aya tatu za Qur'ani zinazoashiria muhtasari wa fadhila na sifa mahsusi za Imam Ali (a.s.)?

5: Taja hadithi tatu mashuhuri za Mtume (s.a.w.w.) zinazomwinua Ali bin Abu Talib (a.s.)?

# Somo la kumi na moja

## Sifa za Imam Ali (a.s.) na mwonekano wake

### Kuifuata haki:

Shakhsia ya Imam Ali (a.s.) ilikuwa na alama dhahiri ambayo ndio makusanyikio ya sifa zake zote na mazalisho ya ukamilifu wake wote, nayo ni kuifuata haki vyovyote itakavyokuwa na popote itakapokuwepo. Kufuata kwake haki kulipatikana tangu kipindi cha mwanzo cha uhai wake kwa kutii amri za Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w.) bila mipaka. Pia kujitokeza kwake daima katika kupambana kwa ajili ya malengo ya utume na uongozi uliotakasika, kumfuata nabii kiongozi kwa ukamilifu na kujijenga kiukamilifu kwa ajili ya amri zote za uongozi huu uliyonyooka.

Hivyo kwa ajili hii akastahiki kuwa khalifa wa Mtume (s.a.w.w.), naibu mtekelezaji, na mwaminifu mwenye moyo mkunjufu katika kutimiza malengo ya Mtume (s.a.w.w.) na makusudio ya utume, kwani sifa zote nzuri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zilipatikana vizuri kwa Imam Ali (a.s.).

## Ibada yake:

Imam Ali (a.s.) amesema: “Hakika kuna watu wanamwabudu Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kutamani, hakika hiyo ni ibada ya wafanya biashara. Na hakika kuna watu wanamwabudu Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuogopa, hakika hiyo ni ibada ya mtumwa. Na kuna watu wanamwabudu Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kumshukuru, hakika hiyo ni ibada ya watu huru.”[173]

Ibnu Abul-Hadid Al-Muutaziliy amesifia ibada ya Imam Ali (a.s.) kwa kusema: “Alikuwa ni mfanya ibada sana, mwenye kuswali na kufunga kuliko watu wote. Watu wamejifunza Swala za usiku, kushikamana na nyuradi na swala za Sunna kutoka kwake. Unasemaje kuhusu mtu ambaye kutokana na kuhifadhi uradi wake amefikia kutandikiwa busati la ngozi usiku katikati ya vita siku ya usiku wa Hariri, akavuta uradi wake huku mishale ikidondoka mikononi mwake na mingine ikipita juu ya masikio yake kulia na kushoto lakini hatetemeshwi na hayo, wala hasimami mpaka amalize jukumu lake. Unasemaje kuhusu mtu ambaye kutokana na kurefusha sijida yake bapa lake la uso lilikuwa na sugu kama sugu za ngamia.?”

Ukifuatilia dua zake na minong’ono yake ukaelewa yaliyomo ndani, kuanzia jinsi anavyomtukuza Mwenyezi Mungu na kumtakasa, mpaka anavyonyenyekea kwa ajili ya haiba na utukufu wa Mwenyezi Mungu huku akimfuata kwa unyenyekevu, utajua ni jinsi gani alivyozungukwa na ikhlasi na utafahamu ni ndani ya moyo upi zimetoka dua hizo na ni kupitia ulimi gani imepatikana minong’ono hiyo.

173 *Nahjul-Balaghah*, semi fupi 237.

## Utawa wake:

Harun bin Antranti amepokea kutoka kwa baba yake kuwa alisema: "Niliingia kwa Imam Ali (a.s.) huko Al-Khawranaqi, yalikuwa majira ya masika nikamkuta kajifunika kitambaa chakavu. Nikamuuliza: Ewe kiongozi wa waumini, hakika Mwenyezi Mungu amekuwekea wewe na familia yako fungu katika mali hii, kisha wewe unajifanyia hivyo? Akajibu: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu, sikupata chochote toka kwenu, wala sina chochote isipokuwa kipande hiki cha kitambaa ambacho nilikuwa nacho toka Madina."[174]

Imam Ali (a.s.) alisikika akisema juu ya mimbari: "Ni nani atakayenunua upanga wangu huu? Laiti ningekuwa na thamani ya kununulia shuka basi nisingeuuza." Hapo akasimama mtu na kusema: "Nakupa thamani ya shuka hivi sasa."[175]

Mmoja wao akamletea Ali (a.s.) chakula kitamu kizuri lakini Ali (a.s.) hakukila, akakitazama na kusema: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu ewe chakula una harufu nzuri, rangi ya kupendeza na ladha nzuri, lakini sipendi kuizoweza nafsi yangu mambo ambayo haijayazowea."[176]

Mashuhuri ni kuwa Ali (a.s.) hakupandanisha tofali juu ya tofali wala nguzo juu ya nguzo. Alikataa kuishi ndani ya kasri la utawala ambalo lilikuwa limeandaliwa kwa ajili yake huko mji wa Kufa. Ibnu Abul-Hadid ameelezea utawa wa Imam Ali (a.s.) akasema: "Katu hakushiba chakula, na alikuwa mgumu wa kula na kuvaa, alikuwa akisema:

174 *Hilyatul-Awliyai*, Uk. 82. *Al-Kamil fi Tarikh*, Juz. 2, Uk. 442.

175 *Al-Manaqib* cha Al-Khawarazmi, Uk. 69. *Kashful-Ghummah*, Juz. 1, Uk. 232.

176 *Tadhkiratul-Khuwas*, Uk. 115.

"Msiyafanye matumbo yenu kuwa makaburi ya wanyama."[177]

## Msamaha na upole wake:

Ibnu Abul-Hadid amesema: "Ama kuhusu upole na msamaha, alikuwa mpole sana anapokosewa na msamehevu sana dhidi ya mwenye kosa. Lilidhihirika hilo siku ya vita vya ngamia (Jamal), kwani alimshinda Mar'wan bin Al-Hakam ambaye alikuwa ndiye adui yake mkubwa na mwenye chuki sana dhidi ya Ali lakini Ali alisamehe.[178]

Watu wa Basra walimpiga vita wakaupiga uso wake na nyuso za wanawe kwa mapanga huku wakimkashifu, lakini alipowashinda hakuwauwa, bali akanadi msemaji wake katikati ya vikosi vya jeshi lake: "Sikilizeni, anayekimbia hafuatwi, aliye majeruhi hashambuliwi, aliyetekwa hauwawi, na yeyote atakayetupa silaha chini basi amesalimika. Pia atakayejiunga na askari wa Imam naye kasalimika". Hakuchukua mizigo yao wala hakuteka watoto wao, wala hakuchukua chochote katika mali yao huku laiti angetaka kufanya hivyo angefanya lakini yeye aliacha kufanya hivyo ili atoe msamaha.

Pindi jeshi la Muawiya lilipomiliki na kuzingira pande zote za mto Furati, viongozi wa Sham waliamrisha jeshi kwa kusema: "Wauweni kwa kiu kama walivyomuuwa Uthman bin Affan kwa kiu." Hapo Ali (a.s.) na maswahaba zake waliliomba jeshi liwaachie wanywe maji. Askari wakajibu: "Tunaapa kwa Mwenyezi Mungu hapana, hatuwezi kuwapa hata tone moja la maji mpaka mfe kwa kiu kama alivyokufa mwana wa Affan."

177 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz.1 Uk. 26.
178 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz.1, Uk. 22.

Imam Ali (a.s.) alipoona hakuna njia isipokuwa kifo aliwaongoza maswahaba zake na kuwashambulia askari wa Muawiya mashambulizi mazito mpaka akawaondoa toka kwenye vituo vyao, hivyo baada ya mauaji mazito ambayo yalidondosha vichwa na mikono mingi, Imam Ali (a.s.) alimiliki maji dhidi yao, na hapo askari wa Muawiya wakawa jangwani hawana maji.

Maswahaba na wafuasi wake wakamwambia: "Ewe kiongozi wa waumini wanyime maji kama walivyokunyima, wala usiwanyweshe hata tone moja, waue kwa upanga wa kiu na uwashike kwa mikono wala hauna haja ya kuendelea na vita." Akajibu: "Hapana, naapa kwa Mwenyezi Mungu siwalipi mfano wa kitendo chao, waachieni baadha ya sehemu za kunywea maji, kwani ukali wa upanga unatosha."

Hakika kitendo hiki ukikilinganisha na upole na usamehevu ni uzuri wa hali ya juu, na ukikilinganisha na dini na uchamungu basi hakuna budi mfano wa hili lifanywe na mtu kama yeye (a.s.)."[179]

## Ushujaa na ushupavu wa Imam (a.s.):

Ibnu Abul-Hadid amezungumzia ushujaa wa Imam Ali (a.s.) akasema: "Hakika yeye aliwasahulisha watu kumbukumbu ya ushujaa wa wale waliyokuwa kabla yake. Msimamo wake vitani ni mashuhuri, hutolewa mfano mpaka siku ya Kiyama. Yeye ni shujaa ambaye katu hakukimbia wala hakutetereka dhidi ya maadui. Wala hakuna aliyechomoza kupambana naye isipokuwa alimuuwa. Katu hakupiga pigo la kwanza kisha akahitajia la pili. Imepokewa ndani ya hadithi kuwa: Mapigo yake yalikuwa ni moja.[180]

179 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz.1, Uk. 23.

180 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz.1 Uk. 20, uhakiki wa Muhammad Abul Fadhli Ibrahim.

Pindi Ali (a.s.) alipomwomba Muawiya achomoze kwenye mpambano ili watu wapumzike na vita kwa kuuawa mmoja wao, Amru alimwambia Muawiya: "Hakika kakufanyia uadilifu." Hapo Muawiya akasema: "Hujawahi kunidanganya tangu uanze kuninasihi isipokuwa leo, yaani unaniamrisha niende kupambana na Abul Hasan ilihali wewe unajua fika kuwa ni shujaa asiyezuilika, naona unatamani utawala wa Sham baada yangu."[181]

Waarabu walikuwa wakijifaharisha wasimamapo kupambana naye vitani, hivyo dada wa Amru bin Abdul Waddi alipokuwa akimlilia kaka yake alisema: "Laiti aliyemuuwa Amru angekuwa si huyu aliyemuuwa, basi ningelia milele maadamu bado nipo duniani. Lakini aliyemuuwa ni mtu asiyekuwa na mfano, na baba yake alikuwa akimwita: 'Wa pekee asiye na mfano.'"[182]

Ibnu Qutayba amesema: "Katu hakupambana na mtu isipokuwa alimshinda,[183] na yeye ndiye aliyeng'oa mlango wa Khaybari kisha likakusanyika kundi la watu ili waweze kuugeuza mlango huo hawakuweza kuugeuza. Na yeye ndiye aliyeng'oa sanamu la Hubal toka juu ya Al-Kaaba, sanamu ambalo lilikuwa kubwa sana lakini akaling'oa na kulitupa aridhini. Na yeye ndiye aliyeng'oa jabali kubwa kwa mkono wake zama za utawala wake yakatoka maji chini yake, hiyo ilikuwa ni baada ya jeshi zima kushindwa kung'oa jabali hilo."[184]

181 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz.1 Uk. 20, uhakiki wa Muhammad Abul Fadhli Ibrahim.

182 Ni miongoni mwa beti ambazo kazitaja mwandishi wa kamusi *Lisanul-Arab*, Juz. 8, Uk 395.

183 *Al-Maarif*, Uk. 210.

184 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz.1, Uk. 21.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 89



## Kujizuwia dhidi ya dhulma na ujeuri:

Imam Ali (a.s.) pamoja na nguvu zake zote zisizo na mfano na ushujaa wake wa pekee lakini alikuwa akijizuia kutokufanya dhulma na ujeuri vyovyote vile itakavyokuwa. Wanahistoria wote wamesema kuwa Ali (a.s.) alikuwa haanzi vita isipokuwa pale atakaposhambuliwa. Alikuwa akiharakisha kusawazisha mambo kati yake na adui kupitia njia za amani ambazo zitazuwia umwagaji damu, hali hii ni hata kama mtu ataharakisha kumfanyia uadui. Hivyo mara nyingi alikuwa akikariri masikioni mwa mwanae Hasan kuwa: "Msiombe kupambana."[185]

Kwa kuwa kauli ya Imam haitoki isipokuwa kutoka kwenye madini safi basi mara zote alikuwa akitekeleza huu usia wake, hivyo alijizuwia kupigana isipokuwa pale alipolazimishwa. Kwa ajili hiyo pindi majeshi ya waasi (Khawariji) yalipoanza kujiandaa ili kumpiga na akatokea mtu mmoja kumnasihi Imam kuwa aanze kuwashambulia kabla hawajamshambulia, Imam alimjibu kwa kusema: "Siwapigi mpaka watakaponipiga."[186]

## Muhtasari:

Pindi tunaposoma kurasa za utu wa Imam Ali (a.s.) hakika tunakuwa tumeashiria kiasi tu kidogo kinachofikiriwa na akili zetu katika kufahamu nafasi ya Imam huyu maasumu. Kwani akili imeshindwa kujua utukufu wa mwanadamu huyu, hivyo baadhi zikavuka mipaka na kujikuta zimemshirikisha Mwenyezi Mungu, na nyingine zikapunguza hivyo zikamchukia na kujikuta zimeritadi.

185 *Nahjul-Balaghah*, hekima ya 233.

186 Tazama kitabu *Abqariyatul-Imam Ali* cha Abbas Mahmud Al-Aqqad, Uk. 18.

Imam Ali (a.s.) alikuwa mchamungu sana wala hakuna yeyote aliyemshinda kwa ibada, lakini yeye aliweka mfano bora wa uhusiano wa mja na muumba wake hivyo akatekeleza ibada kwa kiwango bora zaidi. Akatekeleza ibada ndani ya mwenendo wake wa kila siku, na mfumo wake wa malezi ambao unamjenga mwanadamu mchamungu na kumtengenezea ustaarabu wa kipekee wa kiislamu.

Imam Ali (a.s.) aliishi huku akiwa kajitenga mbali na ladha zote za dunia hii ya mpito, hilo ni kwa sababu aliijua vizuri dunia na akajua vizuri namna ya kujitenga nayo, hivyo akazidiriki neema za Mwenyezi Mungu ambazo hazilingani na neema nyingine yoyote ile.

Imam Ali (a.s.) alimtendea kila adui yake kwa heshima na adabu, kwa akili na imani, akitarajia kutengeneza umma na kuondoa uharibifu, huku akitaka kuamsha dhamira zilizo ndani ya nafsi zenye maradhi, hivyo akasamehe na kuwa mpole huku akijisahaulisha mabaya aliyotendewa, akasahau kulipiza kisasi japokuwa kulipiza huko ni haki yake.

Historia haijamfahamu mtu shujaa mwenye kuitetea imani ya Mwenyezi Mungu kama Imam Ali (a.s.). Hakika alikuwa jasiri shujaa mwenye yakini asiyetetereka, shupavu asiyelainika, mwenye moyo usiojua khofu, hivyo akaupa ulimwengu wote sura dhahiri ya ukomandoo na ushujaa katika medani za kivita na katika kutekeleza jukumu gumu.

Kajizuia kufanya uadui ilikuwa ni msingi kati ya misingi ya mfumo wa Imam Ali (a.s.) katika maisha yake.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 91



## Maswali:

1. Ni sifa zipi muhimu zilizompamba Imam Ali (a.s.)?

2. Elezea jinsi utu wa Imam Ali (a.s.) ulivyopatikana kutokana na kuishi kwake na Mtume (s.a.w.w.)? Na ni athari zipi zilizopatikana katika mahusiano hayo?

3. Elezea jinsi zilivyokuwa ibada kwa Imam Ali (a.s.)?

4. Kwa nini Imam Ali (a.s.) alikuwa akijiepusha na dunia japokuwa ana haki ya kuitumia?

5. Ni kitu gani kilichomtofautisha Imam Ali (a.s.) na wengine wenye kujitenga na dunia?

6. Toa mifano halisi miwili inayoonyesha msamaha na upole wa Imam Ali (a.s.)?

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 92



# Somo la kumi na mbili

## Sifa za Imam Ali (a.s.) na mwonekano wake

### Urafiki:

Laiti kama si mafuriko makubwa ya urafiki wa kweli na huruma iliyojaa na kumwagika ndani ya nafsi yake basi Ali (a.s.) asingechagua urafiki penye uadui. Kwa ajili hiyo wanahabari waaminifu kuanzia wafuasi wake hadi adui zake wamepokea kuwa: Pindi Zubayri na Talha walipong'ang'ania kumpiga vita, wakakataa kumtii huku wakimtuhumu katika tukio mashuhuri la vita vya ngamia (Jamal) Ali (a.s.) aliwaendea akiwa hajajiandaa kwa vita, hana ngao wala silaha huku akiwaonyesha amani aliyodhamiria, kisha akanadi: "Ewe Zubayri! Njoo kwangu". Zubayri akatoka akiwa amejiandaa kwa vita akiwa na silaha. Aisha alipomsikia Ali (a.s.) akapiga kelele akisema: "Eee vita."

Alipiga ukulele huo kwa kuwa kwa uchache alikuwa hana shaka kuwa hakuna kipingamizi isipokuwa ni Zubayri kuuawa, kwani anayepambana na Ali (a.s.) bila kizuizi huuawa hata kama atakuwa ni shujaa mkubwa wa namna yoyote ile au akawa na ujuzi wa juu wa kivita wa kiwango chochote kile.

Lililomshangaza sana Aisha na waliomzunguka ni wao kumwona Ali bin Abu Talib (a.s.) akimkumbatia Zubayri kwa muda mrefu, kwa kuwa sababu za mapenzi ya kweli haziishi ndani ya moyo mkubwa kama huu. Imam Ali (a.s.) akaanza kumuuliza Zubayri kwa lugha ya

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 93



urafiki wao wa zamani akisema: “Jihurumie ewe Zubayri, hivi ni kitu gani kilichokutoa uje kunipiga vita?” Akajibu: “Damu ya Uthman.” Imam akasema: “Mwenyezi Mungu amuuwe aliyetuchonganisha kwa damu ya Uthman.”

Hapo Imam akaanza kumkumbusha ahadi zao, urafiki wao na siku za undugu wao wa zamani. Na huenda Ali (a.s.) alilia sehemu kama hii, lakini Zubayri aliendelea kumpiga vita Imam Ali (a.s.) mpaka Zubayri alipouawa huku kifo chake kikimkarahisha yule aliyemuuwa mwenye kujali upendo Ali bin Abu Talib (a.s.).[187]

## Huruma ya Ali (a.s.):

Imam Ali (a.s.) alisema: “Naapa kwa Mwenyezi Mungu laiti nikipewa mbingu saba na vyote vilivyo chini yake eti ili tu nimwasi Mwenyezi Mungu kwa kumnyang’anya mdudu chungu punje ya shairi, sitofanya, na hakika dunia yenu hii ni dhalili kwangu kuliko jani lililomo mdomoni mwa nzige.”[188]

Ali (a.s.) ndiye mwenye maagizo mazuri aliyoyatuma kwa Al-Ashtar An-Nakhaiy gavana wake wa Misri na watu wake. Ndani ya maagizo hayo amesema: “Usiwe mnyama mkali mwenye kushambulia unayetumia fursa kwa ajili ya kuwala wao. Kwani hakika wao wako katika makundi mawili: Ima ni ndugu yako katika dini au ni kiumbe mwenzako, hivyo wape msamaha wako kama unavyopenda upewe msamaha na Mwenyezi Mungu. Wala usijute kwa msamaha wowote utakaotoa, wala usijivune kwa adhabu yoyote utakayotoa.” Kisha akamwambia: “Jizuie kujilimbikizia.”[189]

187 *Murujud-Dhahab*, Juz. 2, Uk. 370. *Qadatuna*, Juz. 2 Uk 176.
188 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 224.
189 *Nahjul-Balaghah*, barua ya 53.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 94



Hakika ukali wa Ali (a.s.) katika kuzuwia kujilimbikizia ulikuwa ni sababu kubwa ambayo ilipelekea kutokea yaliyotokea kati yake na Muawiya na jamaa zake, kwani hakika hawa walitaka ufalme, mali na utajiri kwa ajili ya nafsi zao huku Ali (a.s.) akitaka hayo yote yawe kwa ajili ya raia wote.

Huruma iliwafikia watu wote akawasamehe dhidi ya yale wanayoyatenda, hivyo watu wa Basra walimpiga vita, wakaupiga kwa mapanga uso wake na nyuso za wanae, wakamtukana na kumlaani, lakini alipowashinda hakuwauwa na akawa kawaingiza katika amani yake. Na aliusia kutendewa wema yule mwovu muuaji wa nafsi yake Ibnu Muljim.

## Uadilifu wa Ali (a.s.):

Si ajabu Ali (a.s.) kuwa mwadilifu kuliko watu wote bali ajabu ni kama hatokuwa hivyo. Kati ya mambo yanayoelezea uadilifu wake ni kuwa alikuta ngao yake kwa mkiristo mmoja wa kawaida, hivyo akampeleka kwa Kadhi ambaye jina lake ni Sharihu ili aweze kumhukumu na kumtolea maamuzi, hivyo waliposimama wote wawili mbele ya Kadhi, Imam Ali (a.s.) alisema: “Hakika ni ngao yangu sijaiuza wala sijaitoa zawadi.” Hapo Kadhi akamuuliza yule mkiristo: “Unasemaje kuhusu aliyoyasema kiongozi wa waumini?” Akajibu: “Hakuna ngao isipokuwa ni ngao yangu, na kiongozi wa waumini kwangu si mwongo”. Hapa Kadhi Sharihu akamuelekea Ali (a.s.) na kumuuliza: “Je una mashahidi watakaothibitisha kuwa hii ni ngao yako?” Ali (a.s.) akatabasamu na kusema: “Sharihu umepatia, sina mashahidi.”

Hivyo Sharihu akahukumu kuwa ngao ni ya yule mkiristo na hapo akaichukua yule mkiristo na kuondoka huku kiongozi wa waumini akimtazama.

Isipokuwa baada ya hatua chache yule mkiristo akarudi huku akisema: "Hakika mimi nakiri kuwa haya ni maadili ya manabii, yaani kiongozi wa waumini ananipeleka kwa Kadhi ili ahukumiwe yeye!" Kisha akasema: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika ngao hii ni ngao yako ewe kiongozi wa waumini, na mimi nilisema uongo katika madai yangu."

Baada ya muda watu walimwona mtu huyu akiwa pembeni mwa Imam Ali (a.s.) akiwa ni askari wake mwaminifu na komandoo wake mkubwa akipambana vikali katika vita vya Nahruwani dhidi ya waasi (Khawariji).[190] **(200)**

Usia wa Imam Ali (a.s.) na barua zake kwa magavana wake, zote zinakaribia kulenga lengo moja nalo ni uadilifu, hivyo watu wote wa mbali na karibu hawakumkubali isipokuwa ni kwa sababu alikuwa ni kipimo cha uadilifu, kipimo ambacho hakikuelemea kwa mtu wa karibu wala hakikumpendelea mtawala, hakikuhukumu isipokuwa haki tupu.

Ama Uthman bin Affan ambaye alitawala dola kabla yake hakika aliachia huru mikono ya ndugu zake wa karibu, wasaidizi wake na swahiba zake wafanye watakavyo katika kila sekta ya vyeo na mali huku akiongozwa na mawazo mabaya ya siri, na hasa Mar'wan ndiye aliyemuathiri sana katika mawazo. Hivyo ilipofika dola mikononi mwa Imam Ali (a.s.) hakutaka chochote isipokuwa ni kuwafanyia uadilifu, akawavua utawala baadhi yao akawaondoa kwenye vyeo na kuwatenga dhidi ya ujilimbikiziaji wa mali huku akipambana na kila aliyetaka kugeuza dini kwa lengo la kujimiminia mali, vyeo na mamlaka nyumbani kwake kwa kuitoa dini kwenye msitari wake.

190 *Tarikhul-Khulafai*, Uk. 184. *Al-Kamil fi Tarikh*, Juz. 3 Uk. 401.

Mara kwa mara alikariri kauli yake nzuri masikioni mwa watu hawa akisema: "Mimi ninajua litakalowafaa na kunyoosha mapindo yenu, lakini haifai niwatengenezee hali zenu kwa kuiharibu nafsi yangu."[191]

## Ukarimu wa Imam Ali (a.s.):

Imam Ali (a.s.) alikuwa mkarimu sana na mwenye mkono mkunjufu kuliko watu wote, kwani alikuwa akifunga na inapofika wakati wa kuftari anachukua chakula chake na kumpa mtu huku akibaki na njaa, hivyo Aya hizi zikamshukia yeye na familia yake: **"Na huwalisha chakula masikini na yatima na mfungwa hali ya kuwa wanakipenda.* Tunakulisheni kwa ajili ya radhi ya Mwenyezi Mungu tu, hatutaki kwenu malipo wala shukurani."**[192]

Wafasiri wamepokea kuwa alikuwa hamiliki isipokuwa dirhamu nne, hivyo akatoa sadaka dirhamu moja usiku na nyingine mchana, na dirhamu nyingine kwa siri na ya nne kwa dhahiri hapo ikateremshwa Aya: **"Wale watoao mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, basi wana malipo yao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika."**[193]

Imepokewa kuwa alikuwa akimwagilia maji mitende ya mayahudi huko Madina mpaka mkono wake unatoa uvimbe lakini apatapo malipo huyatoa sadaka huku akibakia na njaa akifunga jiwe juu ya tumbo lake.

191 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 69,
192 Al-Insan: 8-9.
193 Al-Baqarah: 274.

## Ukweli na nia njema ya Imam Ali (a.s.):

Alifikia kiwango cha juu cha nia njema, kiasi kwamba kutokana na nia hiyo njema akapoteza utawala wa dola, na laiti kama katika hali fulani angebadili nia yake njema basi asingepata adui, wala rafiki zake wasingegeuka adui dhidi yake. Kuna kipindi maswahaba wakubwa muhajirina walijikusanya kwake kwa lengo la kutaka kumkinaisha kwa kumpa njia ya kumwondoa Muawiya, amuundie jambo la ghafla litakalommaliza, lakini aliwakatalia wote akijiepusha dhidi ya njama hiyo.

Baada ya Imam Ali (a.s.) kupewa kiapo cha utii cha kuongoza dola alikuja Al-Mughira bin Shu'bah ambaye alijulikana kwa ujanja, njama na mitego, akamwambia Ali (a.s.): "Hakika wewe una haki ya kutiiwa na kunasihiwa, na mawazo ya leo huzaa yatakayokuja kesho, na upotovu wa leo hupoteza yaliyotakiwa kesho, hivyo mwache Ibnu Amir katika kazi yake, na Muawiya katika kazi yake na watumishi wengine katika kazi zao ili watakapokutii na askari wao wakakupa kiapo cha utii basi ndipo ubadili utakayembadili na umwache unayemtaka." Imam akanyamaza kwa muda kisha akatangaza kuikataa njama hiyo akisema:

"Sidanganyi katika dini yangu wala sifanyi la udhalili katika jambo langu."[194]

Pindi njama na ujanja wa Muawiya ulipodhihiri Imam alitoa ibara ifuatayo ambayo inafaa kuwa mfano bora wa maadili mema ya hali ya juu, alisema: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu, hakika Muawiya si mjanja kuliko mimi, lakini yeye anadanganya na kutenda maovu, hivyo laiti kama si kuchukia udanganyifu basi mimi ningekuwa mjan-

194 - Murujud-Dhahab, Juz. 2 Uk. 364-365.

ja kuliko wote."[195]

Amehimiza kukazania nia njema katika hali yoyote ile akasema: "Alama ya imani ni kutanguliza ukweli japo unakudhuru, na kuuacha uwongo japo unakunufaisha."[196]

## Kujiamini kwa Imam Ali (a.s.):

Sifa zote hizi nzuri ziliungana na sifa nyingine ya kupendeza ya kujiamini, ambayo Imam alifahamika kwayo. Bali kujiamini ni kitu kinachoshikamana na sifa hizi, hivyo Imam anatenda huku akiwa na matumaini na uzuri wa matendo yake, huku akidhihirisha haki wazi wazi, kiasi kwamba hata shujaa wa Bara la Uarabu Amru bin Abdul Wuddi hakumzuia kudhihirisha haki huku Mtume (s.a.w.w.) na maswahaba wakimtahadharisha dhidi ya Amru. Hiyo ni dalili inayoonyesha kujiamini kwake na ushujaa wake mbele ya haki, vitu ambavyo vilijaa ndani ya nafsi yake.

Mara nyingi amekuwa akitoka kuelekea kwenye swala bila ya kusindikizwa na mtu atakayezuia hatari za maadui mpaka Ibnu Muljimu alipomkuta na kumpiga kwa upanga wenye sumu. Je, huu si ushahidi juu ya kujiamini kwake mbele ya haki, kujiamini ambako kunaendesha viungo vyake vyote na mwenendo wake wote.

Kutokana na kujiamini huku kuzuri ndio maana anamwambia swahaba wake na gavana wake huko Madina Sahlu bin Hunayfa Al-Answariy kuwa: "Ama baada, zimenifikia habari kuwa watu kati ya wale waliokuwa kabla yako wanakwenda kwa Muawiya kwa siri, hivyo usihuzunike kwa idadi yao itakayokupita wala kwa mchango

195 *Nahjul-Balaghah*, hotuba ya 200.
196 *Nahjul-Balaghah*, hekima ya 458.

wao utakaokutoka, kwani naapa kwa Mwenyezi Mungu wao hawajakimbia toka kwenye ujeuri wala hawajajiunga na uadilifu."[197]

**Muhtasari**:

Huruma ya kutekeleza ahadi ni huruma ya kina kwa Imam Ali (a.s.), huruma ambayo ilikuwa imejenga moyo wake huku ikidhihirika katika matendo na mienendo yake, hiyo ni hata mbele ya adui yake. Akitarajia kuwaongoza waliopotea na kuwarudisha katika njia sahihi wale waliokengeuka.

Ama kuhusu uadilifu ni kuwa laiti kama ungejitokeza kwa mtu basi angekuwa ni Ali bin Abu Talib (a.s.) na wala si mwingine, kwani alikuwa ni nguvu kali ya kutekeleza uadilifu kwa watu wote. Alikuwa ni mjuzi anayemjua mwanadamu, jamii na kanuni za Mwenyezi Mungu, hivyo kidole chake hakikuacha haki na uadilifu kwa maana yote ya uadilifu na vipengele vyake vyote katika maisha.

Kila kitu katika utu wa Imam Ali (a.s.) kimekamilika na chenye muundo mmoja, kwani hatupati tofauti yoyote katika sifa zake na mwonekano halisi wa utu wake, hivyo akastahiki kuwa alama kati ya alama za utukufu wa Mwenyezi Mungu na mfano bora kwa wanadamu wote katika kumtii Mwenyezi Mungu, na kujenga imani ya Mwenyezi Mungu, kifikira, kimwenendo na kihuruma, hivyo yeye ni mfano mwema wa mtawala shupavu na mtawaliwa mwaminifu mtiifu, na yeye ni sura halisi ya nia njema, utiifu, ibada na nguvu ya haki.

---

197 *Nahjul-Balaghah*, barua ya 70.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 100



Imam Ali (a.s.) alikuwa mkarimu sana kuliko watu wote huku akiwa na mkono mkunjufu. Alikuwa na ukarimu wa hali ya juu huku akijitofautisha kwa kuwa na moyo salama usiokuwa na chuki hata kwa maadui zake, hivyo hakuridhia jambo mbadala lichukue nafasi ya ukweli, kikauli au kivitendo. Sifa zote hizi ziliungana na sifa ya kujiamini mbele ya haki kwa kiwango cha juu.

Mwana wa Abu Talib alijitofautisha na wengine kwa jihadi iliyoendelea katika vipindi vyote vya maisha yake yote huku akiwa na maadili bora na mtazamo wa ndani wa makini uliyonyooka, akiwa na ubainifu safi na utambuzi wa haraka na nguvu za kupambana, hivyo akawa ni kiongozi bora na mfano wa juu baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) katika kila sifa bora.

## Maswali:

1. Toa taswira halisi ya urafiki wa Imam Ali (a.s.)?

2. Toa maneno matatu yanayothibitisha na kutoa sura halisi ya huruma ya Imam Ali (a.s.)?

3. Ni mahusiano yapi yaliyopo kati ya uadilifu na Imam Ali (a.s.)?

4. Japokuwa Imam Ali (a.s.) alikuwa hana kitu lakini kwa nini alikuwa mkarimu kuliko watu wote?

5. Ni uhusiano upi uliyopo kati ya ukweli wa Imam Ali (a.s.) na ukunjufu wa nia yake?

6. Toa taswira mbili zinazoonyesha jinsi Imam Ali (a.s.) alivyojiamini kwa kiwango cha hali ya juu?

# Somo la kumi na tatu

## Urithi wa Imam Ali (a.s.)

Baada ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) hatupati hazina kubwa yenye rutuba iliyokamilika na iliyo maarufu kama hazina aliyoiacha Imam Ali bin Abu Talib (a.s.). Na ya kwanza ni hazina inayojulikana kwa jina la kilele cha fasaha, yaani *Nahjul-balaghah*. Ya pili ni ijulikanayo kwa jina la hekima bora na makusudio ya maneno, yaani *Ghurarul-Hikam wa Durarul-Kalim.*

Kamusi za maudhui ya vitabu hivi viwili vya thamani zimetupa sura ya wazi na halisi kuhusu ukubwa na upana wa hazina hii. Kuanzia ujazo wake, kina chake hadi mjumuisho wake uliojumuisha sekta mbalimbali za maisha ya mwanadamu, kuanzia kijamii hadi mtu mmoja mmoja.

Sisi hapa tumechagua toka kwenye hazina hii kubwa maudhui mbili muhimu zenye uhusiano wa karibu na mtu mmoja mmoja hadi jamii nzima.

### Hali halisi ya wema na uovu:

Akhera ndio kufaulu kwa watu wema.

Tutakaposimama mbele ya Mwenyezi Mungu ndipo wema na uovu utabainika.

Utamu wa Akhera huondoa makali ya uchungu wa mateso ya dunia.

## Mtu mwema:

Mwema ni yule anapoogopa adhabu hujisalimisha, na anapotarajia thawabu hutenda mema. Inatosha mtu kuwa mwema kwa kuaminiwa katika mambo ya dini na dunia. Ni mwema wa hali ya juu sana yule ambaye moyo wake umekutanishwa na ubaridi wa yakini.
Hawi mwema ambaye ndugu zake ni waovu.
Mwema ni yule anayedharau asichokipata.

### Vinavyopelekea mtu kuwa mwema:

#### Akili na maarifa:

Atakayeuwa ujinga wake kwa kutumia elimu yake basi amefaulu kwa kupata hadhi ya juu ya wema. Atakayemfahamu vizuri Mwenyezi Mungu basi daima hatokuwa muovu.

#### Ikhlasi na utiifu kwa Mwenyezi Mungu:

Atakayemtii Mwenyezi Mungu milele hatokuwa muovu.
Mtu huwa hawi mwema isipokuwa kwa kumtii Mwenyezi Mungu.
Mwema ni yule ambaye utiifu wake una ikhlasi.
Harakisha kutii utakuwa mwema.
Mtu yeyote hawi mwema isipokuwa kwa kusimamisha sheria za Mmwenyezi Mungu.
Kukesha usiku katika hali ya kumtii Mwenyezi Mungu ni mavuno ya mawalii na ni bustani ya watu wema. Mkesho wa macho kwa kumtaja Mwenyezi Mungu ni fursa ya watu wema na utakaso wa mawalii.

#### Bidii katika kuitengeneza nafsi:

Atakayepiga vita nafsi yake katika kutafuta wema wake basi atakuwa

mwema.
Hakika nafsi ambayo inajitahidi kung'oa mabaki ya matakwa itapata inalolitafuta na itapata wema katika marejeo yake.

**Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu:**

Jihadi ni nguzo ya dini na njia ya watu wema.

**Utawa dhidi ya dunia isiyodumu:**

Hakika dunia hutolewa na hukataliwa, hivyo watu wema huachana nayo, huku waovu huitamani. Jiepushe na dunia utapata wema katika marejeo yako na yatakuwa mema mafikio yako.

Watakaopata wema wa dunia kesho ni wale wanaoikimbia leo.
Ikiwa kweli mnatafuta neema basi ziacheni huru nafsi zenu toka nyumba ya uovu.

**Uzuri wa kujiandaa na kifo:**

Jitahadhari na mauti, yaandalie maandalizi mazuri utapata wema katika marejeo yako.

Kifo kina raha kwa watu wema.

**Kuitathmini nafsi:**

Atakayeitathmini nafsi yake atakuwa mwema.

**Kukitafuta kilichokupotea:**
Kutafuta mwishoni mwa umri wako kile ulichokipoteza mwanzoni mwa umri wako hukufanya uwe mwema katika marejeo yako.

**Kukaa na wanavyuoni:**

Kaa na wanavyuoni uwe mwema.

**Kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu:**

Mkarimu husifiwa hapa duniani na hupata mema huko Akhera.
Ukitoa mali yako kwa ajili ya Akhera yako kisha ukamwachia Mwenyezi Mungu yule aliyekuja baada yako, utakuwa umepata wema kwa yale uliyotoa na umeutendea wema urithi wako kwa yule uliyemwachia.

**Aliye mwema kuliko wengine:**

Ukitamani kuwa mwema kuliko wengine basi yafanyie kazi yale uliyoyajua.
Mwema zaidi kwenye kheri ni yule anayetenda kheri.
Mwema zaidi kuliko watu wengine ni yule muumini mwenye akili.
Mwema kuliko watu wengine ni yule mwenye kujihukumu mwenyewe kwa kumtii Mwenyezi Mungu.
Mwema zaidi kuliko watu wote duniani ni yule mwenye kuiacha dunia, na mwema zaidi huko Akhera ni mwenye kutenda kwa ajili ya Akhera.
Mwema zaidi kuliko watu wote ni yule atakayejua fadhila zetu na akajikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kupitia sisi. Akawa na mapenzi ya dhati kwetu, akatenda yale tuliyohimiza na kuamrisha, akaacha yale tuliyokataza, basi mtu kama huyo ni katika sisi na yeye atakuwa pamoja nasi katika nyumba ya kudumu.

**Mtu mwovu:**

Atakayetegemea dunia ndio mwovu asiye na kitu.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 105



**Alama za mwovu:**

Miongoni mwa uovu ni mtu kuzuia dini yake kupitia dunia yake.
Miongoni mwa alama za uovu ni kuwatendea ubaya watu wema.
Miongoni mwa alama za uovu ni kumlaghai rafiki.

**Vinavyosababisha uovu:**

Upumbavu ni uovu.
Nia mbaya ni uovu.
Kulimbikiza haramu ni uovu.
Mtu hawi mwovu isipokuwa kwa kumwasi Mwenyezi Mungu.
Miongoni mwa uovu wa mtu ni shaka kuharibu yakini yake.
Sababu ya uovu ni kuipenda mno dunia.
Yule ambaye lengo lake ni dunia basi Siku ya Kiyama uovu wake utarefuka.
Matokeo ya husda ni uovu wa dunia na Akhera.
Kupenda mali na shari husababisha uovu na udhalili.
Kitendo cha mtu kudhulumu hapa duniani ni anwani ya uovu wake huko Akhera.[198]
Muhtsari:

Qur'ani imetilia umuhimu mambo yote yanayohusu maisha na mustakabali wa mwanadamu, hivyo Mtume (s.a.w.w.) na kizazi chake nao wakafuata njia hiyo ya Qur'ani, wakisimama imara kutafsiri makusudio ya Qur'ani na kubainisha ishara na alama zake.

Suala la wema na uovu ni suala la mwanzo kabisa walilotilia umuhimu na kuliashiria, hivyo wakafafanua kipimo cha wema na uovu huku wakifafanua alama na mwonekano wa mtu mwema na mtu

198 Tazama *Ghurarul-Hikam Wadurarul-Kalim* cha Al-Amidiy.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 106



mwovu.

Waligusia vinavyosababisha wema na uovu, hivyo kwa maelezo hayo wakatoa mfumo kamili wa ukamilifu wa mwanadamu katika maisha.

## Maswali:

1. Kutokana na maneno ya Imam Ali (a.s.) ni kipi kipimo cha wema?

2. Kwa mtazamo wa Imam Ali (a.s.) ni yupi aliye mwema?

3. Elezea jinsi wema unavyopatikana?

4. Ni nani aliye mwema kuliko watu wote?

5. Ni vitu gani vinavyompelekea mtu kuwa mwovu, na ni zipi alama za uovu?

# Somo la kumi na nne:

## Urithi wa Imam Ali (a.s.)

Falsafa ya utawala na nidhamu yake

**Kwanza: Utawala ni dharura ya kijamii:**

Uimamu ni mpangilio wa umma.
Lazima watu wawe na kiongozi, awe mwema au mwovu.

**Pili: Falsafa ya utawala:**

**Utawala ni jambo linalokuja na kutoweka:**

Dola kama inavyokuja ndivyo inavyorudi.
Utawala wenye kuhama wenye kuondoka ni jambo dhalili jepesi.

**Utawala ni njia si lengo:**

Ewe Mwenyezi Mungu, hakika wewe unafahamu kuwa yale yaliyotoka kwetu hayakuwa kwa ajili ya kugombania utawala wala kupata chochote kati ya mabaki ya kinachosagika. Lakini yalitoka kwa ajili ya kuhami mafunzo ya dini Yako na kudhihirisha wema katika nchi yako, ili wasalimike wale waliyodhulumiwa miongoni mwa waja Wako na zifanyiwe kazi hukumu Zako zilizoachwa.

**Utawala ni sehemu ya kutahinia maisha:**

Akili za watu hutahiniwa kwa mambo sita: Urafiki, mahusiano, utawala, kuvuliwa cheo, utajiri na ufakiri.

Uwezo hudhihirisha sifa njema na mbaya.

**Tatu: Majukumu ya dola ya kiislamu:**

**Kuuelimisha umma:**

i. Ni wajibu wa Imam kuwaelimisha anaowatawala sheria ya Uislamu na imani yake.

**Kusimamia uadilifu:**

Uadilifu ni nguzo ya raia.
Uadilifu ni nidhamu ya utawala.
Hakuna kinachowapa hali nzuri raia isipokuwa ni uadilifu tu.
Kwa uadilifu hufuatwa sunna za Mwenyezi Mungu na dola huimarika.

**Kuihami dini:**

Kila dola inayozungukwa na dini huwa haishindwi.
Watawala ni watetezi wa dini.
Atakayefanya utawala wake ni kutoa huduma kwa ajili ya dini yake basi kila kitu kitamnyookea.

**Kutekeleza sheria:**

i. Kuwalazimisha waja wa Mwenyezi Mungu kutekeleza hukumu za Mwenyezi Mungu ni kutekeleza haki na kila chenye manufaa.

ii. Kati ya majukumu aliyobebeshwa Imamu na Mwenyezi Mungu
] ni kutekeleza adhabu kwa yule anayestahiki.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 109



**Kujitahidi kutoa nasaha:**

Imam hana jukumu lolote isipokuwa lile alilobebeshwa toka kwenye amri ya Mola Wake nalo ni kuzidisha mawaidha na kujitahidi kutoa nasaha.

**Kuhakikisha kipato na kuboresha maisha:**

Ama haki yenu iliyopo kwangu ni kuwanasihi na kuwahakikishieni kipato chenu.
Watawala wenye hali nzuri sana ni wale ambao maisha ya watu yanaboreka wanapoishi nao**.**

**Kulea umma:**

i. Ama haki yenu iliyopo kwangu ni kuwanasihi…..kuwafunza ili msiwe wajinga na kuwaadabisha kama mlivyojifunza.

**Kutetea uhuru wa nchi na heshima ya taifa**

i. Katika mafunzo ya Imamu kwa magavana wake ni kauli hii: “Hifadhini mipaka yao na pembe za nchi zao.” Pia akasema: “Lazima watu wawe na kiongozi…..watakayemtumia kumpiga adui.”

**Kuleta usalama wa ndani:**

i. Lazima watu wawe na kiongozi…….ambaye kupitia yeye njia zote zitakuwa na amani.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 110



**Kuwasaidia wasiyojiweza:**

Zaka ya mtawala ni kumsaidia asiyejiweza.

**Kujali ujenzi wa nchi:**

i. Ubora wa mtawala ni kujenga nchi.

**Kuwatetea madhaifu:**

i. Dhaifu huendelea kutetewa dhidi ya mwenye nguvu mpaka mwema atakapostarehe na dhaifu akastarehe dhidi ya muovu.

**Nne: Sababu za kudumu dola na sifa ya mtawala wa kuigwa:**

**Kufahamu mambo:**

Imam anahitaji moyo wenye akili.

Akili iliyojiepusha na machafu huamrisha mema.

**Kuifuata haki na kuidhihirisha vitendoni:**

Atakayeifanya haki kuwa ndio dira basi watu watamfanya mtawala.
Atakayeitawala nafsi yake atapata utawala.
Utawala wako ukipenya hadi ndani ya nafsi yako basi nafsi za watu zitajikusanya kuelekea kwenye uadilifu wako.
Kiongozi bora ni yule ambaye matamanio yake hayamwongozi.
Kiongozi mwenye akili sana ni yule anayeitawala nafsi yake kwa ajili ya raia kupitia yale yanayoangusha hoja za raia dhidi yake, na akawatawala raia kupitia yale yanayothibitisha hoja yake dhidi yao.

**Ushujaa katika kutekeleza haki na kusimamisha uadilifu:**

i. Imam anahitaji moyo wenye akili na ulimi wenye kauli na moyo mpana ili asimamishe haki nzito.

**Nia njema:**

Mtawala bora ni yule mwenye vitendo na nia njema, mwadilifu kwa askari wake na raia wake.

**Ufasaha wa maneno:**

Imam anahitaji….ulimi wenye kauli.

**Ihsani kwa raia:**

Atakayewafanyia ihsani raia wake Mwenyezi Mungu humtandazia mbawa za rehema zake na humwingiza katika msamaha wake.
Atakayewafanyia ihsani watu wake anastahiki utawala.

**Kueneza uadilifu kwa watu wote:**

Nguzo ya utawala ni uadilifu.
Atakayefanya uadilifu utawala wake hupenya.
Aliye mwadilifu katika utawala wake hatohitajia wasaidizi wake.
Atakayetenda kwa uadilifu Mwenyezi Mungu atalinda utawala wake.
Mwenye kuzidi uadilifu wake siku zake husifika.
Mtawala mwenye maadili bora ni yule anayewajumuisha watu kwa uadilifu wake.

**Utawa wa nafsi:**

Mtawala bora ni yule mwenye kuizuia sana nafsi yake.

Mbora ni yule asiyebabaishwa wala kudanganywa huku tamaa hazimlaghai.

**Uchumi na kuratibu maisha:**

Hatoangamia yule mwenye kufanya iktiswadi.
Siasa nzuri hudumisha utawala.
Uratibu mzuri na kujiepusha na ubadhirifu ni utawala bora.

**Uadilifu wa nafsi:**

Uadilifu dhidi ya nafsi ni pambo la utawala.
Zaka ya nguvu ni uadilifu dhidi ya nafsi.

**Upole:**

Msingi wa utawala ni kutumia upole.
Siasa nzuri ni upole**.**

**Uvumilivu:**

Uvumilivu ni msingi wa utawala.
Nguzo ya utawala ni kifua kipana (uvumilivu).
Msamaha ni Zaka ya uwezo.
Muadhibu mtumwa wako amwasipo Mwenyezi Mungu lakini msamehe akuasipo wewe.
Utawala wa uadilifu hupatikana katika mambo matatu: Kulainika katika jambo ulilo na uhakika nalo, kulipiza kisasi katika jambo la

uadilifu na kumpendelea mwenzio katika jambo ulilokusudia.

**Kutetea dini:**

Ifanye dini kinga ya dola yako, na shukurani kinga ya neema yako, hivyo kila dola inayozungukwa na dini haishindwi, na kila neema inayokingwa na shukurani hainyang'anywi.

**Kujizuia kwa bidii:**

Omba msaada wa uadilifu kwa kuwa na nia njema kwa raia, kupunguza tamaa na kuzidi kujizuia dhidi ya maasi.

**Kuhisi kuwa mamlaka ni amana ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yako:**

Hakika mtawala ni muhazini wa Mwenyezi Mungu hapa ardhini.
Hakika mamlaka yako si wito wa chakula kwa ajili yako.

**Kuwa macho:**

Ambaye hayajamdhihirikia akiwa macho hawatomnufaisha chochote walinzi wake.

Miongoni mwa alama za dola ni kuwa macho (kuwa chonjo) ili kulinda mambo.

**Kutojivunia nguvu:**

Mwenye hadhi hajivunii cheo alichopata hata kama ni kikubwa namna gani, na dhalili hujivunia cheo chake.

**Kuamrisha yanayowezekana:**

Ukitaka utiiwe omba yanayowezekana.

**Mgao sahihi wa kazi na kuainisha majukumu ya kila mmoja:**

Kila mwanadamu kati ya watumishi wako mpe kazi yake ambayo utamwajibisha kwayo, kufanya hivyo ni bora ili wasitegeane.

**Kugawa wema:**

Atakayetoa wema wake atastahiki uraisi.
Ukarimu ni utawala.
Anayetoa cheo chake husifika.
Pambo la utawala ni kuwapendelea watu (kabla ya nafsi yako).[199]

## Muhtasari:

Uislamu ulikuja kuanzisha dola ya Mwenyezi Mungu yenye mpangilio wa Mwenyezi Mungu na utawala wa kuigwa ambao utamhakikishia mwanadamu wema wa sasa na wa baadaye. Mtume (s.a.w.w.) kiongozi aliasisi dola na kusimamisha nguzo zake. Ama wasii wake mlinzi wa ujumbe wake alibainisha mafunzo ya dola ya kuigwa baada ya kufukuza uovu baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.). Akabainisha sababu za kudumu dola, kukamilika na kuendelea. Akabainisha sababu za kuporomoka dola, ustaarabu wake na utamaduni wake. Ujumbe wake wa kuigwa aliyoutuma kwa gavana wake wa Misri Malik Al-Ashtar unatoa taswira halisi timilifu ya utaratibu wa utawala wa kiislamu.

199 Tazama *Ghurarul-Hikam Wa Durarul-Kalim* cha Al-Amidiy, sehemu ya nne, Uk. 327 – 348.

## Maswali:

1. Elezea kwa ufupi njia za kuthibiti na kuboreka kwa utawala?

2. Kutokana na kauli za Imam Ali (a.s.) je, tunaweza kupata maelekezo ya kumpa baba wa familia kwa kuzingatia yeye ni mtawala wa familia?

3. Kutokana na maelezo ya Imam Ali (a.s.) mtawala ana wajibu gani juu ya umma?

4. Kutokana na kauli za Imam Ali (a.s.) je, unaweza kuainisha mambo yanayowatoa watawala kwenye msitari sahihi?

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 116



# Somo la kumi na tano

## Fatima Az-Zahrau mama wa Maimam watakasifu

### Nasaba yake tukufu:

Hakika kiungo kati ya uimamu na utume ni Fatima binti Muhammad, mama wa Maimam maasumina na mbora wa wanawake wote wa ulimwenguni. Mama yake ni mbora wa wanawake wa kikuraishi, Khadija binti Khuwaylid bin Asad bin Abdul-Uzza bin Quswayy, na yeye ndiye mke wa kwanza wa Mtume (s.a.w.w.) na yeye alitokana na nyumba yenye elimu na sharafu. Hakika kumzaa mtu kama Fatima Az-Zahrah mkweli, mtakasifu na maasumu kunatosha kabisa kuwa utukufu mkubwa kwake.

### Mazazi yake matukufu:

Tabarasiy ndani ya kitabu *Iilamul-Waraa* amesema: "Linalodhihiri katika riwaya za wapokezi wetu ni kuwa alizaliwa Makka siku ya ishirini ya mfungo tisa mwaka wa tano tangu Mtume (s.a.w.w.) kukabidhiwa utume, na Mtume (s.a.w.w.) alifariki Fatima akiwa na umri wa miaka kumi na nane na miezi saba."[200]

Imepokewa kutoka kwa Jabir bin Yazid kuwa alisema: "Imam Al-Baqir (a.s.) aliulizwa: Fatima aliishi muda gani tangu kufariki kwa Mtume (s.a.w.w.)? Akajibu: "Miezi minne na akafariki akiwa na umri wa miaka ishirini na tatu."[201]

200 *Iilamul-Waraa*, Juz. 1, Uk. 290.

201 Mfano wa hiyo inapatikana ndani ya kitabu *Manaqib* cha Ibnu Shah'ri Ashuub, Juz. 1, Uk. 357.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 117



Hakika hili linakaribiana sana na yale waliyoyapokea wasiokuwa Imamiya kuwa alizaliwa mwaka wa arubaini na moja tangu kuzaliwa Mtume (s.a.w.w.), hivyo atakuwa kazaliwa mwaka mmoja tangu Mtume (s.a.w.w.) kukabidhiwa utume.[202]

Mwalimu wetu Abu Said Al-Waidhiy ndani ya kitabu *Sharafun-Nabii* amesema: "Watoto wote wa Mtume (s.a.w.w.) walizaliwa kabla ya Uislamu isipokuwa Fatima na Ibrahim hakika wao wawili walizaliwa ndani ya Uislamu."[203]

## Majina yake na lakabu zake:

Imepokewa kutoka kwa Imam Jafar As-Sadiq (a.s.) kuwa alisema: "Fatima ana majina tisa mbele ya Mwenyezi Mungu: Fatima, As-Siddiqah, Al-Mubarakah, At-Tahirah, Az-Zakiyyah, Ar-Radhiyah, Al-Mardhiyyah, Al-Muhaddathah na Az-Zahrau."[204]

Imepokewa kutoka kwa Imam Ridha (a.s.) kuwa Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Hakika binti yangu amepewa jina la Fatima kwa sababu Mwenyezi Mungu amemtenga mbali na moto yeye na yule atakayempenda."[205]

Mtume (s.a.w.w.) alimpa jina la Batul[206] kisha akamwambia Aisha:

202 *Mustadrakul-Hakim*, Juz. 3, Uk. 161 na 163. *Al-Istiab*, Juz. 4 Uk. 374. *Maqtal* cha Al-Khawarazimiy, Uk. 83. *Al-Iswabah*, Juz. 4 Uk. 377.

203 *Iilamul-Waraa*, Juz. 1, Uk. 290.

204 *Amalis-Suduq*, Uk. 484. *Al-Khiswal*, Juz. 2, Uk. 414. *Dalailul-Imamah*, Uk. 10. *Tajul-Mawalid*, Uk. 20.

205 *Uyunu Akhbar-Ridha*, Juz. 2 Uk. 46. *Maanil-Akhbar*, Uk. 64. *Ilalus-Sharaiu*, Uk. 178.

206 *Ilalus-Sharaiu*, Uk. 181. *Manaqib* cha Ibnu Shah'ri Ashuub, Juz. 3, Uk. 330.

"Ewe mwenye macho mekundu, hakika Fatima si kama wanawake wa kibinadamu yeye hapatwi na siku kama mnavyopatwa na siku."[207]

Alikuwa akichuruzika maji ya Peponi kwa sababu pindi Mtume (s.a.w.w.) alipopelekwa miraji aliingia Peponi akala na kunywa chakula na maji ya Peponi kisha usiku huo huo akarudi na kumwingilia mkewe Khadija na akawa kashika mimba ya Fatima, hivyo mimba ya Fatima ikatokana na maji ya Peponi.[208]

## Makuzi yake:

Fatima amezaliwa na kutokana na wazazi wawili watukufu, kwani hakuna mtu yeyote ambaye ana baba mwenye athari kama za baba yake, athari ambazo zilibadili sura nzima ya historia, huku ndani ya muda mfupi zikimpeleka mwanadamu hatua za mbali kuelekea mbele. Wala historia haijatusimulia kuhusu mama kama mama yake ambaye alimpa mume wake na dini yake tukufu kila alicho nacho kwa malipo ya kupata uongofu na nuru.

Chini ya kivuli cha wazazi hawa wawili watukufu ndipo alipokulia Fatima Al-Batul, akakulia ndani ya nyumba ambayo imezungukwa na mapenzi ya baba yake ambaye alibeba joho la utume na akavumilia yale ambayo majabali yalishindwa kuvumilia.

207 *Manaqib* cha Ibnu Shah'ri Ashuub, Juz. 3 Uk. 330. *Al-Muujam Al-Kabir*, Juz. 22, Uk. 400.

208 Rejea aliyoyapokea Ibnu Abbas kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) ndani ya kitabu *Manaqib* cha Ibnu Al-Mughazaliy, Uk. 357 na 406. *Manaqib* cha Al-Khuwarazamiy, Uk. 64. *Dhakhairul-Uqba,* Uk. 36.

## Vipindi vya maisha yake:

Fatima Az-Zahrau (a.s.) aliishi ndani ya misukosuko ya kufikisha ujumbe tangu utotoni mwake, akawekewa vikwazo yeye, baba yake, mama yake na Bani Hashim wengine katika bonde maarufu ilihali wakati vikwazo vinaanza alikuwa hana umri isipokuwa miaka miwili tu.

Vilipoondolewa tu vikwazo baada ya miaka mitatu migumu akakumbana na msukosuko mwingine nao ni kufiwa na mama yake kisha kufariki ami yake huku akiwa mwanzoni mwa mwaka wake wa sita, hivyo akabakia kama kifuta machozi cha baba yake akimliwaza wakati wa upweke huku akimsaidia dhidi ya majeuri na mabeberu ya kikurayshi.

Mtume akahama kuelekea Madina yeye na Fatima mwingine akiwa ni mtoto wa ami yake Ali (a.s.) huku akiwa na umri wa miaka minane, hivyo akabakia na baba yake mpaka alipokutanishwa na mtoto wa ami yake, Ali bin Abu Twalib, hapo ikaanzishwa nyumba tukufu ndani ya Uislamu kwani Fatima aligeuka chombo safi cha kuendeleza kizazi kitakatifu cha Mtume (s.a.w.w.) na kheri nyingi waliyopewa kizazi kitakasifu cha Mtume (s.a.w.w.).

Az-Zahrau alitoa mfano bora wa mke na mama ndani ya kipindi kigumu cha historia ya Uislamu, kipindi ambacho Uislamu ulikuwa unataka kuweka njia ya kudumu ya utukufu wa juu lakini ndani ya mazingira ya kijahiliya na mila za kikabila zinazokataa uwanadamu wa mwanamke huku zikimhesabu mwanamke kuwa ni aibu. Hivyo ikawajibika kwa Az-Zahrau kutumia mwenendo wake binafsi na wa kijamii ili kuwa mfano halisi wa kivitendo unaojenga mjengo halisi wa mafunzo na hadhi ya ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Az-Zahrau ameuthibitishia ulimwengu wa wanadamu kuwa yeye ni mwanadamu

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 120



timilifu ambaye ameweza kuwa alama ya uwezo wa juu wa Mwenyezi Mungu na muujiza wake wa ajabu, hiyo ni kutokana na hadhi, heshima na utukufu aliokuwa nao. Az-Zahrau Al-Batul alimzalia Ali (a.s.) watoto wawili watukufu wa kiume nao ni mabwana wa vijana wa Peponi na watoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu: Hasan na Husein Maimam watakasifu, pia alimzalia mabinti wawili watukufu: Zaynabu mkubwa na Ummu Kulthum wapiganaji wawili wenye subira.

Az-Zahrau alimporomosha mwanae wa tano Muhsin baada ya kifo cha baba yake kutokana na matukio ya uadui dhidi ya nyumba yake, nyumba ya utume na uimamu, hapo zikatimia habari za Qur'ani iliposema: **"Hakika sisi tumekupa kheri nyingi.* Basi swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje.* Hakika adui yako atakuwa mkiwa."**

Hivyo yeye Zahrau ndio kheri nyingi ya utume ambayo Mwenyezi Mungu alimpa Mtume wake (s.a.w.w.), isipokuwa Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anahitaji wenye kujitolea atakaowatoa kwa ajili ya mti wake wenye kustawi ili kuwazima maadui zake ambao tangu mwanzo walisimama kidete kuuwa Uislamu na alama zake.

## Kifo chake na kuoshwa kwake:

Az-Zahrau (a.s.) alifariki Madina siku ya tatu ya mfunguo tisa mwaka wa kumi na moja. Aliishi siku tisini na tano tangu kufariki kwa Mtume (s.a.w.w.).[209] Wengine wamepokea kuwa aliishi miezi minne. Wengine wakasema siku arubaini. Pia imepokewa kuwa aliishi siku sabini na tano huku wengine wakidai aliishi miezi sita au minane.[210]

209 *Adh-Dhuriyat-Tahirah* cha Ad-Duulabiy, Uk. 151 na 199. *Kashful-Ghummah*, Juz. 1, Uk. 503.

210 *Manaqib* cha Ibnu Shah'ri Ashuub, Juz. 3 Uk. 357. *Al-Iswabah*, Juz. 4, Uk. 379. *Jalaul-Uyun*, Juz. 1, Uk. 216.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 121



Imam Ali (a.s.) ndiye aliyemwosha.[211] Imepokewa kuwa Asmaa binti Umays ndiye aliyemsaidia Imam Ali (a.s.) kumwosha. Az-Zahrau alikuwa kaacha usia kuwa atakapofariki asioshwe na yeyote yule isipokuwa Ali (a.s.) na Asmaa.[212]

## Mazishi yake na eneo la kaburi lake:

Aliswaliwa usiku, na waliomswalia ni Ali (a.s.), Hasan, Husein, Ammar, Mikdad, Aqil, Zubeyr, Salman, Baridah na kundi dogo la Bani Hashim. Kisha kiongozi wa waumini Ali (a.s.) akaenda kumzika kwa siri ikiwa ni kutekeleza usia wake kuhusu hilo.[213]

Watu wametofautiana kuhusu eneo la kaburi lake, yupo anayesema kuwa alizikwa Baqii.[214] Yupo anayesema alizikwa nyumbani kwake. Bani Umaiyya walipozidi msikitini ikawa ni msikitini.[215] Yupo anayesema kuwa alizikwa kati ya kaburi la Mtume (s.a.w.w.) na mim-

211 *Al-Kafiy*, Juz. 1, Uk. 382. *Ilalus-Sharaiu*, Uk. 184. *Dalailul-Imamah*, Uk. 46. *Tajul-Mawalid*, Uk. 98. *Al-Istiaab*, Juz. 4, Uk. 379.

212 *Kashful-Ghummah*, Juz. 1, Uk. 500. *Mustadrakul-Hakim*, Juz. 3, Uk.163. *Al-Istiaab*, Juz. 4, Uk. 379.

213 *Rawdhatul-Waidhina,* Uk 152. *Tajul-Mawalid*, Uk. 98. *Manaqib* cha Ibnu Shah'ri Ashuub, Juz. 3, Uk. 363. Sahih *Bukhari*, Juz. 5, Uk. 177. *Sahih Muslim*, Juz. 3, Uk. 1380. *Tabaqat* cha Ibnu Saad, Juz. 8 Uk. 229 *Muswannaf* cha Abdur-Razzaq, Juz. 5 Uk. 427. *Sunan Al-Bayhaqiy*, Juz. 6, Uk. 300. *Tarikh At-Tabariy,* Juz. 3, Uk. 208. *Mustadrakul-Hakim*, Juz. 3 Uk. 162. *Al-Istiaab*, Juz. 4, Uk. 379. *Usudul-Ghaba*, Juz. 5, Uk. 524.

214 *Tajul-Mawalid*, Uk. 99. *Manaqib* cha Ibnu Shah'ri Ashuub, Juz. 3, Uk. 357. *Kashful-Ghummah*, Juz. 1, Uk. 501.

215 *Al-Kafiy,* Juz. 1, Uk. 383. *Al-Faqihi*, Juz. 1, Uk. 148. *Uyunul-Akhbar-Ridha*, Juz. 1, Uk. 311. *Maanil-Akhbar,* Juz. 1, Uk. 268. *Dhakhairul-Uqba* Uk. 504.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 122



bari yake.[216] Huenda hili ndilo lililoashiriwa na Mtume (s.a.w.w.) aliposema: "Kati ya kaburi langu na mimbari yangu kuna kiunga kati ya viunga vya peponi."[217] Isipokuwa Tabarasiy amesema: "Kauli ya kwanza iko mbali na usahihi, na kauli mbili za mwisho zinakaribia usahihi, hivyo anayechukua tahadhari katika kumzuru humzuru maeneo yote matatu."[218]

## Muhtasari:

Fatima Az-Zahrau (a.s.) mbora wa wanawake wote na binti wa mbora wa viumbe amekulia chini ya kivuli cha nabii wa rehema na mlezi wa wanadamu, hivyo Mwenyezi Mungu akampenda kutokana na sifa zake bora. Mama yake alifariki huku akipambana na misukosuko kwa ajili ya ujumbe wa Mwenyezi Mungu, hivyo Fatima (a.s.) akawa kifuta machozi na liwazo la baba yake.

Alihama kutoka Makka akiwa na mtoto wa ami yake ili aungane na baba yake ambaye alikuwa ameanza kujenga misingi ya dola ya kiislamu iliyobarikiwa.

Mwenyezi Mungu alimteua awe mke wa Ali bin Abu Twalib, hivyo akatoa mfano bora wa mwanamke wa kiislamu, huku akiwa ni chombo safi cha kuendeleza kizazi cha Mtume (s.a.w.w.) ambacho kilien-

216 *Maanil-Akhbar*, Juz. 1, Uk. 268. *Rawdhatul-Waidhina*, Uk. 152.

217 *Al-Kafiy*, Juz. 4, Uk. 553-555. *Al-Faqihi*, Juz. 2 Uk. 339. *At-Tahdhib* cha Tus, Juz. 6, Uk. 7. *Al-Muwatta*, Juz. 1, Uk. 97. *Sahih Bukhar*, Juz. 2, Uk. 77. *Sahih Muslim*, Juz 2, Uk. 1010. *Musnad Ahmad*, Juz. 2, Uk. 236 na 376 na 438 na 466 na 533. Pia Juz. 3, Uk. 4, na Juz. 4, Uk. 39 na 40. *Sahih Tirmidhiy*, Juz. 5, Uk. 718 na 719. *Sunan An-Nasaiy*, Juz. 2, Uk. 35

218 *Iilamul-Waraa*, Juz. 1, Uk. 293.

delea kupitia wanae wa kiume mabwana wa vijana wa Peponi, hivyo yeye akawa ni makutano ya utume na uimamu.

Aliishi na baba yake na mumewe ndani ya matatizo yote ya ulinganio wa Uislamu akashirikiana nao katika jukumu la kujenga Uislamu.

Baada ya baba yake alikumbana na dhulma toka kundi lililoacha njia, hivyo akaporomosha (kuharibika mimba) mwanae wa tano kutokana na tukio la uadui alilofanyiwa yeye pamoja na mumewe. Baada ya tukio hilo hakuishi muda mrefu akawa ameungana na baba yake huku akiwa mwenye subira mvumilivu wa maudhi yote yaliyomfika kwa ajili ya ujumbe wa milele wa Muhammad (s.a.w.w.).

## Maswali:

1. Fatima Az-Zahrau amezaliwa wapi?

2. Pindi Mtume (s.a.w.w.) alipokabidhiwa utume Fatima (a.s.) alikuwa na umri wa miaka mingapi?

3. Fatima Az-Zahrau aliolewa lini?

4. Ni watoto gani wa kiume na wa kike waliozaliwa na Fatima?

5. Ni vipi vipindi vya maisha yake?

6. Kwa nini nyumba ya Fatima Az-Zahrau ndio nyumba tukufu ndani ya Uislamu?

7. Lini, wapi na vipi alizikwa Az-Zahrau (a.s.)?

# Somo la kumi na sita

## Mwonekano wa utu wa Fatima Az-Zahrau

Fatima Az-Zahrau (a.s.) ni binti wa nabii mtukufu na ni mke wa Imam mtukufu na ni mama wa wajukuu wawili Hasan na Husein mabwana wa vijana wa Peponi. Hakika yeye ni uso wenye kung'ara kwa ajili ya utume wa mwisho, na ni chombo safi kwa ajili ya kuendeleza kizazi kitakasifu, na ni chimbuko safi la kizazi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) huku akiwa ni mbora wa wanawake wote ulimwenguni.

Historia yake ni sawa na historia ya utume kwani alizaliwa kabla ya Mtume (s.a.w.w.) kuhama, na akafariki miezi michache baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.). Aya za Qur'ani tukufu ndani ya miongo hii miwili ya historia ya Uislamu zimebeba karama na fadhila za Az-Zahrau, baba yake, mumewe na wanawe ambao walitoa mfano bora wa jihadi, subira, moyo mkunjufu na kujitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Ama upande wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yeye alionyesha utukufu wa nafasi yake na daraja la kutamaniwa alilofikia katika njia ya ujumbe wa Mwenyezi Mungu huku Mtume (s.a.w.w.) akienda sawia na njia ya Qur'ani katika kueleza karama na fadhila za Ahlul-Bayt wote kwa ujumla na kueleza karama na fadhila za moyo wa Mtume (s.a.w.w.) kwa upekee.[219]

219 Rejea yaliyopokewa kuhusu tafsiri ya Sura Al-Kawthar, Aya ya utakaso, Aya ya mapenzi kwa watu wa karibu, Aya ya maapizano, Sura Dahri na maelezo ya Mtume (s.a.w.w.) kuhusu Az-Zahrau na Ahlul-Bayt ndani ya kitabu *Aalamul-Hidayah*, Juz. 3.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 125



## Az-Zahrau mbele ya mbora wa Mitume (s.a.w.w.):

Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu hughadhibika kwa kughadhibika Fatima na huridhia kwa kuridhia Fatima."[220]

Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Fatima ni pande la nyama yangu atakayemuudhi kaniudhi, na atakayempenda kanipenda."[221]

Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Fatima ni moyo na roho yangu inayonizunguka."[222]

Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Fatima ni mbora wa wanawake wote wa ulimwenguni."[223]

Ushahidi kama huu ni mwingi ndani ya vitabu vya hadithi na sira[224] ukipokewa toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ambaye

---

220 *Kanzul-Ummal*, Juz. 6 Uk. 219. Al-*Mustadraku alas-Sahihayni*, Juz. 3, Uk. 153. *Mizanul-Iitidal*, Juz. 3, Uk. 72.

221 *As-Swawaiqul-Muhriqah* Uk. 107 na 138. *Sahih Bukhar* kitabu cha mwanzo wa uumbaji. *Kanzul-Ummal*, Juz. 6, Uk. 22. *Sahih Muslim* kitabu cha fadhila za sahaba. *Khasais* cha An-Nasaiy, Uk. 35. *Sahih Tirmidhiy*, Juz. 2, Uk. 319.

222 *Faraidus-Samtwayn*, Juz. 2, Uk 66.

223 *Musnad Abi Dawdi*, Juz. 6 hadithi za wanawake. *Hilyatul-Awliyai* cha Abu Naim, Juz. 2, Uk. 29. *Mushkilul-Athar*, Juz. 1 Uk. 48. *Shar'hu Nahjul-Balaghah* cha Abul Hadid, Juz. 9, Uk. 193. *Al-Awalim*, Juz. 11, Uk. 46 na 49.

224 *Kanzul-Ummal*, Juz. 7, Uk. 92. *Musnad Ahmad*, Juz. 6, Uk. 296 na 323. *Mustadrakus-Sahihayni*, Juz. 3 Uk. 148 na 151. *Sahih Bukhar* kitabu cha kuomba idhini. *Sahih Tirmidhiy*, Juz. 2, Uk. 306. *Hilyatul-Awliyai* cha Abu Naim, Juz. 2, Uk. 42. *Al-Istiaab*, Juz. 2, Uk. 720 na 750.

hatamki la matamanio yake[225] wala hapendelei kwa sababu au nasaba, wala katika jambo la Mwenyezi Mungu haogopi lawama ya mwenye kulaumu.

Kwa kuwa Mtume mtukufu (s.a.w.w.) amezama ndani ya Uislamu na kwa sababu hiyo akawa ni kiigizo chema kwa watu wote ndio maana mapigo ya moyo wake, mtazamo wa macho yake, mpapaso wa mikono yake, hatua za utembeaji wake na mawazo ya fikira zake vyote vimekuwa ni mafunzo kati ya mafunzo ya dini, chanzo cha sheria, taa ya uongofu na njia ya uokovu.

Hakika ushahidi huu kutoka kwa hitimisho la mitume ni medali kwa Az-Zahrau, medali ambazo zinazidi kung'aa kila muda unavyokwenda, hasa pale tunapoangalia chanzo cha msingi ndani ya Uislamu kupitia maneno ya Mtume (s.a.w.w.) aliyomwambia Az-Zahrau kuwa: "Ewe Fatima, tenda kwa ajili ya nafsi yako, hakika mimi sitokufaa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu."[226]

Na kauli ya Mtume (s.a.w.w.): "Katika wanaume wamekamilika wengi lakini kwa wanawake hawajakamilika isipokuwa Mariam binti Imran, Asia binti Muzahim mwanamke wa Firaun, Khadija binti Khuwaylid na Fatima binti Muhammad (s.a.w.w.)."[227]

Na kauli ya Mtume (s.a.w.w.): "Hakika Fatima ni tawi la moyo wangu hunichukiza yanayomchukiza na hunifurahisha yanayomfu-

225 Ameashiria hilo ndani ya Sura An-Najmi: 3.

226 *Fatumatuz-Zahrau witri fi Ghamdi,* Utangulizi wa Sayyidi Musa As-Sadri

227 Ameipokea mwandishi wa kitabu *Al-Fusulul-Muhimmah* kutoka kwenye *Sahih Tirmidhiy,* Uk. 123. Na rejea *Tafsirul-Wusuul,* Juz. 2, Uk.159. *Musnad Ahmad,* Juz. 2, Uk. 511.

rahisha,**[228]** na hakika nasaba zote siku ya Kiyama zitakatika ila nasaba yangu, sababu yangu na ukwe wangu."**[229]**

Imepokewa kuwa siku moja Mtume (s.a.w.w.) alitoka huku akiwa kamshika mkono Fatima akasema: "Anayemtambua huyu basi kishamtambua na asiyemtambua basi huyu ni Fatima binti Muhammad, na yeye ni kipande cha nyama yangu, na ni moyo wangu unaonizunguka, hivyo atakayemuudhi atakuwa kaniudhi na atakayeniudhi atakuwa kamuudhi Mwenyezi Mungu".**[230]** Mara nyingine akasema: "Fatima ndiye nimpendaye sana kuliko watu wote.**"[231]**

Maelezo haya ni ushahidi bora juu ya umaasumu wake baada ya Aya ya utakaso, bali yanatuchorea njia ya utambuzi dhidi ya matukio yatakayoukumba Uislamu kiasi kwamba haghadhibiki isipokuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

### Az-Zahrau mbele ya Ahlul-Bayt, maswahaba na tabiina:

Kutoka kwa Imam Ali bin Husein Zaynul-Abidin amesema: "Khadija hakumzalia Mtume (s.a.w.w.) mtoto yeyote ndani ya maumbile ya kiislamu isipokuwa Fatima."**[232]**

---

228 *Mustadrakul-Hakim*, Juz. 3, Uk. 154. *Kanzul-Ummal*, Juz. 12, Uk. 111, hadithi ya 3424.

2229 *Musnad Ahmad*, Juz. 4, Uk. 323 na 322. *Al-Mustadrak*, Juz. 3, Uk. 58.

230 *Al-Fusulul-Muhimmah*, Uk. 128. Na ameipokea ndani ya kitabu *Al-Mukhtaswar* kutoka kwenye *Tafsir At-Thaalabiy*, Uk. 133.

231 *Aamal* cha Tus, Juz. 1 Uk. 24. *Al-Mukhtaswar,* Uk. 136.

232 *Rawdhatul-Kafiy*, Uk. 536.

Kutoka kwa Imam Muhammad Al-Baqir amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu alimwachanisha kwa elimu."[233]

Kutoka kwa Imam Jafar As-Sadiq amesema: "Hakika aliitwa Fatima kwa sababu viumbe wameachanishwa na maarifa yake."[234]

Ibnu Abbas amesema: "Siku moja Mtume (s.a.w.w.) alikuwa amekaa huku akiwa na Ali, Fatima, Hasan na Husein akasema: Ewe Mwenyezi Mungu hakika wewe unajua kuwa hawa ni kizazi changu na niwapendao sana kuliko watu wote, hivyo mpende atakayewapenda na umchukie atakayewachukia, mtawalishe atakayewatawalisha na umfanyie uadui atakayewafanyia uadui, msaidie atakayewasaidia, wafanye watakasifu dhidi ya kila uchafu, watakasifu dhidi ya kila dhambi na uwasaidie kwa roho mtakatifu toka kwako."

Imepokewa toka kwa mama wa waumini Ummu Salamah kuwa alisema: "Fatima binti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ndiye aliyeshabihiana sana na Mtume (s.a.w.w.) kisura na kimaumbile."

Imepokewa toka kwa mama wa waumini Aisha kuwa alisema: "Sikumwona mtu aliyekuwa mkweli kuliko Fatima isipokuwa yule aliyemzaa.[235] Alikuwa aingiapo kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) basi Mtume husimama humkaribisha na kumbusu kisha humshika mkono na kumkalisha alipokaa yeye. Na Mtume (s.a.w.w.) aingiapo kwa Fatima basi husimama toka alipokuwa ameketi kisha hubusu mikono yake na humkalisha alipokaa yeye. Alikuwa msiri wa Mtume (s.a.w.w.) na marejeo yake katika jambo lake."[236]

233 *Kashful-Ghummah*, Juz. 2, Uk. 99.
234 *Biharul-An'war*, Juz. 43, Uk. 65.
235 *Kashful-Ghummah*, Juz. 2, Uk.97 na 99.
236 *Ahlul-Bayt* cha Tawfiqi Abu Ilmi, Uk. 144.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 129



Ibnu Swabbagh Al-Malikiy amesema: "Na yeye ni binti wa yule aliyeteremshiwa: "Utukufu ni wa ambaye alimpeleka mja wake".[237] Watatu baada ya jua na mwezi, binti wa mbora wa wanadamu, mzawa mtakasifu aliye mbora kwa kongamano la wema wote."[238]

Al-Hafidh Abu Nuaim Al-Isfihaniy amesema: "Kati ya vitakaswa vya watakasifu na visafi vya wachamungu ni Fatima mbora, mtawa, pande la nyama ya Mtume na shabihi wake….. Alikuwa kajitenga mbali na dunia na starehe zake, huku akijua vizuri machungu ya aibu za dunia na maangamizo yake."[239]

Abdul-Hamid bin Abul-Hadid Al-Muutazaliy amesema: "Mtume (s.a.w.w.) alimtukuza sana Fatima kinyume na watu walivyokuwa wakifikiria….. mpaka akavuka kiwango cha mapenzi ya wazazi kwa wana wao, hivyo akatamka mara kwa mara na sehemu mbalimbali, mbele ya watu maalumu na mbele ya watu wote kuwa: "Yeye ni mbora wa wanawake wote wa ulimwenguni, na hakika yeye ni pacha wa Mariam binti Imran, na kuwa atakapotaka kupita kwenye kisimamo cha siku ya Kiyama atanadi mwenye kunadi toka upande wa Arshi kuwa: Enyi watu mliopo kwenye kisimamo, fumbeni macho yenu ili apite Fatima binti Muhammad."

Hii ni kati ya hadithi sahihi wala si dhaifu, kwani si mara moja Mtume (s.a.w.w.) amekuwa akisema: "Huniudhi linalomuudhi na hunighadhibisha linalomghadhibisha, na hakika yeye ni pande la nyama yangu, hunichukiza yanayomchukiza."[240]

---

237 Al-Israi:1.

238 *Al-Fusulul-Muhimmah*, Uk.143 chapa ya Beirut.

239 *Hilyatul-Awliyai* cha Abu Naim, Juz. 2, Uk. 39, chapa ya Beirut.

240 *Shar'hu Nahjul-Balaghah*, Juz. 9, Uk. 193.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 130



## Muhtasari:

Fatima ni nyota ing'aayo katika mbingu ya akida ya kiislamu na ni bendera ya uongofu kwa wanadamu. Mwenyezi Mungu amemsifia ndani ya Qur'ani huku akidhihirisha fadhila zake. Ama Mtume (s.a.w.w.) yeye amemsifia huku akivichorea vizazi vijavyo alama za hadhi yake, nafasi yake na mchango wake na akiwahimiza waislam wampende na kumridhisha. Kisha Maimam maasumina nao wakamsifu na kueneza nuru yake mpaka ikabainika kwa kila mwenye macho kuwa ni wajibu kueneza fadhila zake.

Maswahaba na wanafunzi wa maswahaba, waandishi, watu wa hadithi na wanahistoria wote wamemtukuza na kuinua nafasi yake huku wakitamka fadhila zake na sifa zake.

## Maswali:

1. Taja Aya za Qur'ani zinazozungumzia fadhila za Az-Zahrau?

2. Mtume wa Mwenyezi Mungu amekutanisha ridhaa na ghadhabu ya Az-Zahrau na ridhaa na ghadhabu yake. Nini maana ya kauli hiyo?

3. Toa hadithi tatu toka kwenye maelezo ya Maimam maasumina kuhusu fadhila za Az-Zahrau?

4. Ni ipi nafasi ya Az-Zahrau mbele ya waandishi na wanahistoria?

# Somo la kumi na saba

## Fadhila na mwonekano wa Az-Zahrau (a.s.)

Hakika yeye ni binti wa nabii aliyezikomboa na kuziongoza akili zama zote. Pia yeye ni mke wa Imam ambaye alikuwa nguzo miongoni mwa nguzo za haki na mwendelezo wa nabii mtukufu katika historia ya mwanadamu. Hakika Fatima (a.s.) alipata akili kamilifu, roho nzuri, na dhamira safi, hivyo kwa msimamo wake na urithi wake akatuchorea sifa za njia bora ambayo dini imepita. Hivyo yeye Fatima (a.s.) akawa nguzo kati ya nguzo za dini, kwa ajili hiyo huwezi kujua historia ya Uislamu vizuri bila kujua historia yake.

Hakika Az-Zahra (a.s.) alikuwa mfano bora wa mwanamke katika ubinadamu, utawa, heshima na utukufu, ukiongeza uelevu wa juu na elimu pana aliyokuwa nayo. Fahari hii inatosha, nayo ni kulelewa ndani ya shule ya unabii na kuhitimu masomo yake toka chuo cha utume. Akanywa toka kwa baba yake Mtume mwaminifu yale aliyokunywa baba yake toka kwa Mola wa ulimwengu.[241]

Hakika Fatima (a.s.) alisikia Qur'ani toka mdomoni mwa nabii mtukufu na toka kwenye sauti ya Ali (a.s.), hivyo akamwabudu Mola wake baada ya kuzitambua sheria zake, faradhi zake na sunna zake, utambuzi ambao haukufikiwa na yeyote mwingine mwenye sharafu na karama. Na hapa ndipo tunapojua siri ya maneno aliyotamka Aisha kuwa: "Hajampata mwanamke aliyependwa sana na Mtume (s.a.w.w.) kuliko Fatima." Japokuwa yeye Aisha alibadili hilo akase-

241 *Ahlul-Bayt* cha Tawfiq Abu Ilmi, Uk.116.

ma: “Sikumwona mtu mkweli mno kuliko Fatima isipokuwa tu yule aliyemzaa.”[242]

Hivyo ndivyo alivyogeuka Az-Zahrau sura halisi ya mwanadamu mkamilifu ambaye waumini wananyenyekea kwa kumtakasa.

## Elimu yake na maarifa yake:

Fatima (a.s.) hakukomea tu kwenye maarifa aliyoandaliwa na nyumba ya ufunuo, wala hakuishia kujing’arisha kielimu kutokana na mionzi ya elimu na maarifa yaliyomzunguka pande zote, bali alikuwa akijaribu kumywa elimu nyingine vyovyote iwezekanavyo, hiyo ni kila anapokutana na baba yake na mume wake ambaye ni mlango wa jiji la elimu ya Mtume (s.a.w.w.).

Alikuwa na utaratibu wa kudumu wa kuwatuma watoto wake Hasan na Husein kwenda kwenye darasa la Mtume (s.a.w.w.) kisha huwahoji pindi wanaporejea, hivyo ndivyo alivyokuwa akijali utafutaji wa elimu huku akijali kuwalea wanawe malezi bora. Japokuwa majukumu yake yalikuwa mengi lakini alikuwa akitoa elimu yake kuwapa wanawake wengi wa kiislamu. Hakika juhudi hizi endelevu za kutafuta elimu na kuisambaza zimemfanya awe miongoni mwa wapokezi wakubwa wa kike wa hadithi. Pia awe miongoni mwa wabebaji wa sunna takatifu kiasi kwamba kitabu chake kikubwa ambacho alikuwa akikijali sana kikajulikana kwa jina la msahafu wa Fatima.

Tusisahau kuwa kati ya majina yake ni Muhaddathah, yaani msemeshwa. Kwa ajili hiyo anakuwa pacha wa Mariam katika kuzungumzishwa na malaika, na hili ni chimbuko jingine la elimu yake ambayo ilihamia kwa wanawe maasumina wakirithishana wao

242 *Ahlul-Bayt* cha Tawfiq Abu Ilmi, Uk.116.

kwa wao.

Hotuba mbili muhimu alizotoa baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.) zinatosha kuwa dalili juu ya hilo na juu ya ubora wa fikira zake na ukamilifu wa elimu yake.[243] Hotuba moja alitoa mbele ya maswahaba wakubwa ndani ya msikiti mtumufu wa Mtume (s.a.w.w.) na nyingine nyumbani kwake. Hakika zimekusanya madhumuni ya kupendeza yanayoonyesha undani wa fikira zake, upana wa maarifa yake, uwezo wa lugha yake, ukweli wa habari zake kuhusu mwelekeo wa umma baada ya umma kuacha njia sahihi baada tu ya kifo cha baba yake. Zaidi ya hapo ni maadili yake ya juu na jihadi yake kubwa kwa Mwenyezi Mungu na katika njia ya haki.

Az-Zahrau alikuwa miongoni mwa Ahlul-Bayt, wao walimcha Mwenyezi Mungu na Yeye akawafunza,[244] na hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu alivyomwachanisha kwa elimu na hivyo akaitwa Fatima, kama alivyoelekea kwa Mwenyezi Mungu hivyo akaitwa Al-Batul.

## Maadili yake bora:

Fatima (a.s.) alikuwa mwenye maadili bora, dhamira safi, nafsi safi, mwepesi wa kufahamu, mwenye matendo bora, jasiri shujaa, jasiri wa nafsi, asiyejivuna, asiyedhibitiwa na dunia danganyifu, asiyejikweza na asiye na kiburi.[245]

---

243 Tazama hotuba hizo mbili ndani ya kitabu *Al-Ihtijaj* cha At-Tabarasiy

244 Anaashiria kauli ya Mwenyezi Mungu: “Mcheni Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atawafunza” Sura Al-Baqarah: 282.

245 *Ahlul-Bayt* cha Tawfiq Abu Ilmi, Uk.132 - 134.

Alikuwa mvumilivu, mwingi wa subira, mnyenyekevu mtulivu, mpole mwenye huruma, mtawa mwenye kujihifadhi. Ulimi wake ulikuwa haupiti isipokuwa penye haki. Hatamki isipokuwa ukweli, hamtaji mtu kwa ubaya, hateti wala hasengenyi. Huhifadhi siri, hutekeleza ahadi, huwa mkweli wa nasaha, anakubali udhuru, hujiepusha kumkosea mtu, na mara nyingi husamehe akosewapo, hivyo hupokea kosa kwa kulipa msamaha.

Alikuwa mbali na shari mwenye kuelemea heri, mwaminifu, mkweli katika kauli yake, mkweli wa dhati na ahadi, alikuwa katika kiwango cha juu cha utawa. Hasukumwi na matamanio yake, kwa sababu yeye ni miongoni mwa Ahlul-Bayt wa Mtume (s.a.w.w.) ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na kuwatakasa moja kwa moja.

Alikuwa aongeapo na mtu au kuhutubia wanaume basi ni lazima kuwa na pazia kati yake na wao, pazia ambayo huzuwia kati yao kwa ajili ya utawa na kujihifadhi. Alikuwa amekinaika na hali yake akiamini kuwa tamaa hufarakisha moyo na huharibu mambo. Akishikamana na kauli aliyoambiwa na baba yake: "Ewe Fatima vumilia dhidi ya machungu ya dunia ili ufaulu kwa kupata neema za milele."[246]

Hivyo alikuwa ameridhika na maisha mepesi mvumilivu dhidi ya ugumu wa maisha, mwenye kutosheka na kidogo cha halali, mwenye kuridhia, mwenye kuridhiwa, hatamani ya mtu mwingine wala hakodolei macho yasiyokuwa haki yake, wala hakujishusha kwenda kumwomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Hakika yeye alijitosheleza kama alivyosema baba yake: "Hakika utajiri bora ni utajiri wa nafsi."[247]

---

246 *Ad-Durrul-Manthur*, Juz. 6, Uk. 261.

247 *Nahjul-Fasaha*, neno la 2382.

Hakika yeye ni mbora ambaye alijielekeza kwa Mwenyezi Mungu na kuiacha dunia yake, akajiepusha na kujitenga na mapambo na udanganyifu wake, akafahamu maangamizi yake, akavumilia kutekeleza majukumu yake, huku akipambana na ugumu wa maisha na ulimi wake ukilowana kwa kumtaja Mola Wake.

Hakika lengo la Az-Zahrau lilikuwa ni Akhera, hivyo hakukusanya furaha za dunia huku akimwona baba yake ameipa mgongo dunia na yote yaliyomo duniani kuanzia ladha, starehe na matamanio ya dunia. Subira yake juu ya matatizo ni maarufu, ukubwa wa shukurani yake wakati wa raha inajulikana, ni maarufu kwa kuridhika na matokeo ya majaliwa ya Mwenyezi Mungu mpaka akasimulia toka kwa baba yake kuwa: “Mwenyezi Mungu ampendapo mja wake humjaribu kwa matatizo, hivyo iwapo atasubiri humkweza na akiridhia humteua.”[248]

## Muhtasari:

Kama maadili ya Mtume (s.a.w.w.) ni Qur’ani basi maadili ya Az-Zahra ndio maadili ya baba yake. Yametudhihirikia maadili bora ya Az-Zahra na utu wake wa juu unaomfanya awe kiigizo kwa waislam wote.

Mwenyezi Mungu alimfanya bora kuliko wanawake wote wa ulimwenguni kwa sababu yeye amekunywa elimu ya Mwenyezi Mungu, akaamini ujumbe wa Uislamu, akamtii Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa moyo mmoja zaidi ya maelezo.

Aliweza kutoa nguvu zake zote katika njia ya Mwenyezi Mungu, kujenga Uislamu na kuhudumia umma wa waislam kwa ajili ya mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu. Alikuwa na moyo mkunjufu

248 Tazama *Ahlul-Bayt* cha Tawfiq Abu Ilmi, Uk.137.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 136



katika imani yake na ibada yake, akakamilika katika kila linalohusu maisha yake mpaka mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu na Mtume yakadhihirika katika kila hatua ya maisha yake.

## Maswali:

1. Elezea mazingira ya tauhidi aliyokulia Az-Zahrau (a.s.)?

2. Elezea jinsi Az-Zahrau (a.s.) alivyojali elimu na maarifa?

3. Bainisha maadili yake bora ya muhimu?

4. Taja sifa mahsusi za elimu na maarifa ya Az-Zahrau (a.s.)?

5. Elezea ni upi msahafu wa Fatima (a.s.)?

6. Hotuba mbili za Az-Zahrau (a.s.) zina hadhi gani kihistoria?

### Kwa ajili ya kujisomea

Az-Zahrau (a.s.) alikuwa ni mbora wa kuwapendelea wengine kuliko nafsi yake huku akimuiga baba yake katika hilo mpaka imekuwa maarufu kuwa alitoa sadaka gauni lake la harusi usiku wa kupelekwa kwa mumewe.

Maelezo yaliyomo ndani ya Sura Ad-Dahri yanatosha kuthibitisha upendeleo wake na ukarimu wake. Jabir bin Abdullah Al-Answariy amepokea kuwa: Mtume alitusalisha Swala ya alasiri na baada ya kumaliza alikaa huku kazungukwa na maswahaba zake, ghafla akatokeza mzee wa kiarabu akiwa kijifunga nguo chakavu akiwa dhaifu mwenye uchovu. Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akamfuata na kumuuliza habari zake. Mzee akasema: "Ewe Mtume

wa Mwenyezi Mungu, mimi nina njaa nilishe, sina nguo nivishe na fakiri nipe masurufu."

Mtume akajibu: "Mimi sina kitu sasa hivi lakini mwonyesha kheri ni sawa na mtenda kheri, hivyo nenda nyumbani kwa yule ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanampenda na yeye anawapenda, humtanguliza Mwenyezi Mungu kuliko nafsi yake, nenda nyumbani kwa Fatima."

Nyumba ya Fatima ilikuwa imeungana na nyumba ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ambayo alikuwa akiitumia kujitenga na wakeze, akamwambia Bilal: "Ewe Bilal simama umpeleke kwa Fatima." Akaondoka bedui akiwa na Bilal na alipofika mlangoni kwa Fatima aliita kwa sauti ya juu: "Amani iwe juu yenu enyi kizazi cha Mtume, mapishano ya malaika, mashukio ya Jibril roho mwaminifu akiwa na ufunuo toka kwa Mola wa ulimwengu."

Fatima akasema: "Waa'leykum salam, ni nani wewe?"
Akasema: "Mimi ni mzee wa kiarabu ninahisi njaa, sina nguo, na masikini. Nisaidie Mwenyezi Mungu atakurehemu."

Fatuma na Ali na wao walikuwa katika hali kama hiyo kwani walikuwa na siku tatu hawajakula chochote, huku tangu mwanzo Mtume (s.a.w.w.) akiwa anajua hali hiyo. Hivyo Fatima (a.s.) akaenda kuchukua tandiko la ngozi ya kondoo ambalo Hasan na Husein walikuwa wakilalia. Kisha akamwambia: "Chukua ewe mbisha hodi hakika Mwenyezi Mungu atakubadilishia kwa kukupa kilicho bora zaidi ya hiki."

Bedui akasema: "Ewe binti wa Muhammad, nimelalamika kwako kuwa nina njaa kisha wewe unanipa tandiko la ngozi ya kondoo nitalifanyia nini huku nikiwa na njaa kama hii?" Fatima (a.s.) aliposikia

maneno haya alichukua mkufu uliokuwa shingoni mwake ambao alipewa zawadi na Fatima binti wa ami yake Hamza bin Abdul Muttalib, hivyo akauvua na kumpa bedui kisha akamwambia: “Chukua ukauuze, hakika Mwenyezi Mungu atakubadilishia kwa kukupa kilicho bora zaidi.”

Bedui akachukua mkufu na kwenda nao msikiti wa Mtume (s.a.w.w.) huku Mtume akiwa kaketi na maswahaba zake. Bedui akasema: “Ewe Mtume, Fatima amenipa mkufu huu.”

Mtume akamwambia: “Uza mkufu huo.”
Jabir anasema: Mtume akalia na kusema: “Itakuwaje Mwenyezi Mungu asikubadilishie kwa kukupa kilicho bora zaidi ilihali mkufu huo kakupa Fatima binti wa Muhammad mbora wa wanawake wote wa ulimwengu!”

Ammar bin Yasir akasimama na kusema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! je unaniruhusu kununua mkufu huu?” Mtume akajibu: “Ununue ewe Ammar kwani laiti makundi mawili (binadamu na majini) yangeshirikiana kuununua basi Mwenyezi Mungu asingeyaadhibu kwa moto.” Ammar akasema: “Ewe bedui! unauza mkufu kiasi gani?” Akajibu: “Kwa kipande cha mkate na nyama, kwa nguo ya kiyemeni ambayo itanitosha kujisitiri na kumwabudia Mola Wangu na dinari itakayotosha kunifikisha nyumbani kwangu.”

Ammar alikuwa amekwishauza fungu lake alilopewa na Mtume (s.a.w.w.) kutoka kwenye vita vya Khaybar, hivyo alikuwa hajabakiwa na kitu, ndipo alipomwambia: “Nakupa dinari ishirini, dirhamu mia mbili za fedha, nguo ya kiyemeni na usafiri wangu utakufikisha nyumbani kwako na nitakushibisha kwa kukupa mkate na nyama.” Bedui akasema: “Ewe ndugu! hakika wewe ni mkarimu mno.” Hapo Ammar akaenda naye na kumpa yote aliyomdhamini. Bedui akarudi

kwa Mtume (s.a.w.w.) na hapo Mtume akamuuliza: "Je, umeshiba na umevaa?" Bedui akajibu: "Hakika nimetosheka."

Mtume (s.a.w.w.) akamwambia: "Mlipe Fatima kwa wema wake." Bedui akasema: **"**Ewe Mwenyezi Mungu, hakika wewe ni Mola wa tuliyokuzushia na hatuna Mola tunayepasa kumwabudu isipokuwa wewe, na wewe ndiye mtoa riziki kwetu katika kila hali, hivyo ewe Mola, mbariki binti wa Mtume Fatima kwa kumpa neema ambayo hakuwahi mtu yeyote kuiona wala kuisikia."

Hapo Mtume (s.a.w.w.) akaitikia dua yake na kisha akawageukia maswahaba na kuwaambia: "Hakika Mwenyezi Mungu ameshampa Fatima hayo hapa duniani kwani: Mimi ndiye baba yake wala hakuna yeyote ulimwenguni mfano wangu, na Ali (a.s.) ndiye mumewe na laiti asingeumbwa Ali (a.s.) basi milele Fatima asingepata wa kumstahili, na akampa Hasan na Husein wala hakuna yeyote ulimwenguni aliyeruzukiwa watoto mfano wao, wao ni mabwana wa vijana wa wajukuu wa manabii na mabwana wa vijana wa Peponi."

Mbele yake alikuwepo Mikdad, Ammar na Salman, Mtume (s.a.w.w.) akawaambia: "Je, niwaongezee?" Wakajibu: "Ndiyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu." Akasema: "Jibril amenijia akaniambia kuwa: Atakapozikwa Fatima malaika wawili watamuuliza: Ni nani Mola wako? Atawajibu: "Allah ndio Mola wangu." Watamuuliza: "Ni nani nabii wako?" Atasema: "Baba yangu." "Na ni nani walii wako?" Atajibu: "Ni huyu aliyesimama mdomoni mwa kaburi langu."

Mtume akasema: "Je, niwaongeze fadhila zake? Hakika Mwenyezi Mungu amemuwekea walinzi kati ya malaika wanamlinda mbele na nyuma, kushoto na kulia, wako naye katika uhai wake, kifo chake na ndani ya kaburi lake. Wanazidisha kumwombea rehema na amani yeye na baba yake, mume wake na wanae, hivyo atakayenizuru mimi

baada ya kifo changu atakuwa kanizuru wakati wa uhai wangu, na atakayemzuru Fatima atakuwa kanizuru mimi, na atakayemzuru Ali bin Abu Twalib atakuwa kamzuru Fatima, na atakayewazuru Hasan na Husein atakuwa kamzuru Ali, na atakayevizuru vizazi vyao wawili hawa atakuwa kawazuru wao wenyewe."

Hapo Ammar akaenda kuupaka mkufu manukato na kuuweka ndani ya kitambaa cha kiyemeni. Alikuwa na mtumwa aliyemnunua kutokana na fungu lake alilopata toka Khaybari, hivyo akampa mtumwa wake ule mkufu na kumwambia: "Chukua mkufu huu umpelekee Mtume na wewe uwe miliki yake." Mtumwa akauchukua mkufu ule na kumpelekea Mtume (s.a.w.w.) na kumwambia aliyoambiwa na Ammar. Mtume akamwambia: "Chukua mkufu huu umpelekee Fatima na wewe uwe miliki yake."

Mtumwa akauchukua mkufu ule na kumpelekea Fatima na kumwambia aliyoambiwa na Mtume (s.a.w.w.). Hapo Fatima akapokea mkufu kisha akamwacha huru mtumwa huku kijana yule akicheka. Fatuma akamuuliza: "Ewe kijana! ni kitu gani kinachokuchekesha?" Akajibu: "Unanichekesha ukubwa wa baraka za mkufu huu, kwani umemshibisha mwenye njaa, ukamvisha asiye na nguo, ukamtajirisha fakiri, ukampa uhuru mtumwa na mwisho ukarejea kwa mwenyewe."[249]

249 *Ahlul-Bait*, Uk. 138.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 141



# Somo la kumi na nane:

## Fadhila na mwonekano wa Az-Zahrau (a.s.)

### Imani na ibada zake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu:

Kumwamini Mwenyezi Mungu ndio alama ya mwanadamu mkamilifu, na ibada kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ndio ngazi ya kufikia kilele cha ukamilifu. Na hakika manabii wamepata makazi bora katika nyumba ya heshima kutokana na daraja lao la imani na juhudi zao za kuchuma mema hapa duniani na moyo mkunjufu katika ibada kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Qur'ani ndani ya Sura Ad-Dahri imethibitisha ukamilifu wa moyo mkunjufu wa Az-Zahrau na unyenyekevu wake kwa Mwenyezi Mungu, ukubwa wa imani yake Kwake na siku ya mwisho, imani ambayo imetengeneza mfano bora wa kuigwa kama alivyothibitisha hilo Mtume (s.a.w.w.) kwa kusema: "Hakika binti yangu Fatima moyo wake na viungo vyake vimejazwa imani na Mwenyezi Mungu mpaka kwenye mfupa wa ubongo, hivyo akatetemeka kwa ajili ya kumtii Mwenyezi Mungu."[250]

Akasema tena: "Hakika anaposimama mihrabuni mbele ya Mola wake nuru yake huwang'aria malaika wa mbinguni kama nuru ya sayari inavyowang'aria watu wa aridhini, hapo Mwenyezi Mungu huwaambia malaika wake: Enyi malaika Wangu, hebu mtazameni mja wangu wa kike Fatima, mbora wa waja wangu wote wa kike, amesimama mbele yangu huku viungo vyake vikitetemeka kwa

250 *Biharul-An'war*, Juz. 43 Uk. 46 na 56-58

kuninyenyekea, amenielekea kwa moyo wake akiniabudu, nawathibitishieni kuwa nimewasalimisha wafuasi wake dhidi ya moto."[251]

Hasan bin Ali (a.s.) amesema: "Nilimwona mama yangu Fatima amesimama mihrabuni kwake usiku wa Ijumaa, aliendelea kurukuu na kusujudu mpaka ikachomoza asubuhi huku nikimsikia akiwaombea heri waumini wa kiume na wa kike, akiwataja kwa majina yao, huku akizidisha kuwaombea ilihali yeye mwenyewe hajajiombea chochote. Nikamwambia: Ewe mama yangu mpendwa! Kwa nini hujiombei kama unavyowaombea wengine? Akajibu: "Ewe mwanangu mpendwa! Kwanza jirani kisha wa ndani."[252]

Saa za mwisho za mchana wa Ijumaa alikuwa akizifanya ni maalumu kwa ajili ya dua. Pia alikuwa halali lifikapo kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani. Alikuwa akiwahimiza wote waliyomo nyumbani kwake kuuhuisha usiku huo kwa ibada na dua. Hasan Al-Basri amesema: "Hakutokea mtu mfanya ibada sana ndani ya umma huu kama Fatima, alikuwa akisimama kufanya ibada mpaka nyayo zake zinavimba.[253] Alikuwa akihema ndani ya Swala yake kwa ajili ya kumwogopa Mwenyezi Mungu."[254]

Je ndani ya maisha yake Fatima aliwahi kutoka kwenye mihrabu yake? Hapana. Hakika humwabudu Mwenyezi Mungu nyumbani kwake kwa kuwa mke bora na kuwalea wanawe malezi bora huku akimtii na kumwabudu Mwenyezi Mungu kwa kutekeleza huduma zote za jamii, aliwasaidia mafakiri na kuwapendelea kuliko nafsi yake hata kama hana cha kujitosheleza.

251 *Biharul-An'war*, Juz. 43 Uk. 46 na 56-58.
252 *Amaali As-Suduq, Al-Majlis* 24, Uk. 100.
253 *Iddatud-Dai*, Uk.139.
254 *Iddatud-Dai*, Uk.139.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 143



## Mapenzi na huruma yake:

Az-Zahrau (a.s.) alichukua mapenzi, upendo na huruma toka kwa baba yake, hivyo alikuwa mwana mwema kwa Mtume (s.a.w.w.). Alimpenda Mtume (s.a.w.w.) kwa dhati, hivyo akampendelea kuliko nafsi yake. Alikuwa akihudumia nyumba ya baba yake huku akitekeleza ayatakayo Mtume (s.a.w.w.), hivyo anatekeleza yanayomfaa Mtume (s.a.w.w.), yanayompa raha na utulivu huku akiharakisha kutenda kila linalomridhisha baba yake, Mtume wa Mwenyezi Mungu. Anamwandalia maji ya kuoga, chakula, anafua nguo zake, zaidi ya hapo anashirikiana na wanawake wengine kubeba chakula na vinywaji kwa ajili ya kuhudumia na kuwatibu majeruhi.

Hakika katika vita vya Uhud alitibu majeraha ya baba yake, hivyo alipoona damu hazikatiki akachukua kipande cha mkeka kisha akakiunguza mpaka kikawa jivu kisha akamwagia jivu hilo kwenye jeraha na hapo damu ikasimama. Akamletea kipande cha mkate wakati wa kuchimba handaki, Mtume (s.a.w.w.) akamuuliza: “Ni kitu gani hiki ewe Fatima?” Akajibu: “Ni kipande cha mkate nilioutengeneza kwa ajili ya wanangu wapendwa hivyo nimekuletea kipande chake.” Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Hakika hiki ndio chakula cha kwanza kinachoingia mdomoni mwa baba yako tangu siku tatu.”[255]

Hakika Az-Zahra (a.s.) aliweza kuziba pengo la mapenzi, pengo ambalo Mtume (s.a.w.w.) alilipata baada ya kufiwa na wazazi wake wawili na mkewe mtukufu Khadija (r.a.) huku akiwa katika mazingira magumu ya ulinganio wa jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Na hapa tunafahamu kiini cha lile alilolikariri Mtume (s.a.w.w.) ulimini mwake kwa kusema: “Fatima ni mama wa baba yake.”[256]

255 *Awalimul-Uluum*, Juz. 1 Uk. 244 amenukuu toka kwenye kitabu *Majmauz-Zawaid*, Juz. 1 Uk. 312.

256 Rejea *Usudul-Ghaba*, Juz. 5 Uk. 520. *Al-Istiaab*, Juz. 4 Uk. 380.

Alikuwa akihusiana naye uhusiano wa mama, anaubusu mkono wake, anakuwa wa kwanza kumzuru aingiapo Madina na wa mwisho kumuaga atokapo Madina. Safari na misafara yake ya kivita huanzia nyumbani kwa Fatima (a.s.), hivyo alikuwa akijiongezea baraka na upendo katika safari na misafara yake toka katika chemchemu hii safi. Pia alikuwa akirudi mara kwa mara nyumbani kwa Fatima, hivyo Fatima (a.s.) humpokea kama mama ampokeavyo mwanae, humlea, humkumbatia na humpunguzia machungu huku akimuhudumia na kumtii.

## Mapambano yake endelevu:

Fatima (a.s.) alizaliwa kipindi cha mapambano kati ya Uislamu na Ujahiliya. Akafumbua macho yake huku waislamu wakiwa katika jihadi kali dhidi ya ushirikina wenye kiburi. Maquraishi waliweka vikwazo dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) na Bani Hashim wote, hivyo Mtume (s.a.w.w.), mkewe mpiganaji, na binti yake mtakasifu wote wakaingia bonde la Abu Twalib, humo wakawekewa vikwazo muda wa miaka mitatu, wakaonjeshwa aina za ukata na ugumu wa maisha. Pamoja na hayo yote lakini walipambana katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kutetea haki na kujitolea kwa ajili ya imani tukufu.

Miaka ya vikwazo vizito na vigumu ikapita na Mtume (s.a.w.w.) akatoka huku akiwa ameshinda. Ndani ya mwaka huo huo Mwenyezi Mungu akapenda kumchagua Khadija, pia ndani ya mwaka huo akafariki Abu Twalib ami wa Mtume (s.a.w.w.) na mtetezi wa Uislamu, hivyo huzuni na uchungu vikachukua moyo wa Mtume (s.a.w.w.) baada ya kuwa amemkosa kipenzi cha moyo wake.

Hivyo ndivyo Fatima (a.s.) alivyopatwa na msiba huku akiwa bado hajashiba mapenzi ya mama yake, na hapo akaungana na baba yake

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 145



katika machungu. Japokuwa alimkosa mama yake, chanzo cha mapenzi, lakini Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akijaribu kumpa mapenzi mbadala toka kwake badala ya mapenzi makubwa ya mama yake.

Baada tu ya kufariki ami yake na mtetezi wake Abu Twalib maquraishi walimwagia kila chuki yao na maudhi yao juu ya Mtume (s.a.w.w.) huku Az-Zahrau (a.s.) akiona kwa macho yake maudhi yote yanayofanywa na wajinga na waovu wa kiquraishi, ilihali Mtume (s.a.w.w.) akitaka kuwatoa gizani na kuwapeleka kwenye nuru.

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akijaribu kumpunguzia machungu huku akimhimiza kuwa na subira kwa kumwambia: “Ewe mwanangu mpendwa usilie, hakika Mwenyezi Mungu anamlinda na kumnusuru baba yako dhidi ya maadui wa dini Yake na ujumbe wake”.[257] Hivyo ndivyo alivyokuwa Mtume (s.a.w.w.) akipandikiza roho ya mapambano ya juu ndani ya nafsi ya binti yake huku akiujaza moyo wake subira na imani ya ushindi.

Az-Zahra (a.s.) alihamia Madina baada ya baba yake kuhama toka anga la Makka la kutisha. Alihama na mtoto wa ami yake Ali bin Abu Twalib (a.s.) ambaye alidharau kiburi cha ujeuri wa maquraishi hivyo Az-Zahrau (a.s.) akaungana na Mtume (s.a.w.w.) huko Kuba baada ya miguu yake kuvimba kutokana na kutembea.

Kwa unyeyekevu Az-Zahrau (a.s.) akahamia kwa mumewe huko Madina baada ya baba yake kusimamisha misingi ya dola, akashirikiana na baba yake katika mapambano kwa subira dhidi ya matatizo ya maisha na misukosuko ya jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu huku Fatima akijaribu kutoa sura halisi ya mfano wa kuigwa katika maisha mapya ya ndoa.

257 *Siratul-Mustafa*, Uk. 295

Az-Zahrau (a.s.) alichangia sehemu kubwa na ya kuonekana katika kuinusuru haki na kutetea usia wa Mtume (s.a.w.w.) pale aliposimama kidete dhidi ya uendaji kinyume, akapiga kelele kwa namna isiyo na mfano huku akiwa pembeni ya kipenzi chake Ali bin Abu Twalib (a.s.) ndani ya siku ngumu za maisha yake ili ahakikishe kuwa uwanja wa ndani wa Ali (a.s.) ni imara haudhoofiki. Pamoja na hayo yote anaacha uamuzi na msimamo wa mwisho utolewe na kuchukuliwa na kiongozi wake, mume wake na Imam wake Ali (a.s.) ili aamue linalonasibiana sana na mazingira.

Az-Zahrau (a.s.) alikuwa akienda kila Jumamosi asubuhi kwenye makaburi ya mashahidi katika viwanja vya Uhud kisha akiwaombea rehema na msamaha. Hakika vitendo hivi vinaonyesha ni kwa kiwango gani Fatima (a.s.) alithamini jihadi na shahada huku vikiweka wazi thamani ya maisha yake kivitendo, maisha ambayo yalianza kwa jihadi, yakategemea jihadi, yakakomea kwa jihadi, hiyo ni ili apate cheo cha shahidi.[258]

## Muhtasari:

Az-Zahrau (a.s.) alifuata nyayo za baba yake katika kila jambo, hivyo Mtume (s.a.w.w.) anathibitisha kuwa Mwenyezi Mungu ameujaza moyo wake na viungo vyake vyote imani kwa ajili yake. Pia walioishi naye wamethibitisha kuwa alikuwa mtu wa ibada sana kuliko watu wote.

Pia amefahamika kwa huruma kwa baba yake mpaka akampendelea kuliko nafsi yake, wanawe, hivyo baba yake akampa jina la: Mama wa baba yake.

258 Tazama *Fatimatuz-Zahrai Witri fi Ghumdi*, utangulizi wa Sayyid Musa As-Sadri.

Alibeba jukumu la jihadi katika njia ya Mola Wake kabla na baada ya kuolewa. Akasimama imara mbele ya matatizo baada ya kufariki baba yake ili aing'arishe njia ya haki kwa wapitaji.

**Maswali:**

1. Toa wasifu wa ibada ya Az-Zahrau (a.s.)?

2. Az-Zahrau (a.s.) alishiriki na baba yake katika vita gani?

3. Elezea jinsi Az-Zahrau (a.s.) alivyompunguzia machungu baba yake?

4. Elezea sifa za Az-Zahrau (a.s.) kama mama?

5. Ni upi mchango na nafasi ya Az-Zahrau (a.s.) katika kuimarisha ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.)?

# Somo la kumi na tisa

## Urithi wa Az-Zahrau (a.s.)

i. Imepokewa toka kwa Fatima binti wa Mtume (s.a.w.w.) kuwa yeye Fatima aliingia nyumbani kwa Mtume (s.a.w.w.), hapo Mtume (s.a.w.w.) akatandika nguo kisha akamwambia akae juu yake, kisha akaingia Hasan, Mtume (s.a.w.w.) akamwambia kaa pamoja na mama yako. Akaingia Husein, Mtume (s.a.w.w.) akamwambia kaa nao. Kisha akaingia Ali (a.s.) akaambiwa na Mtume (s.a.w.w.) kaa nao. Kisha Mtume (s.a.w.w.) akashika pembe za nguo na kuwafunika na kusema: "Ewe Mwenyezi Mungu; wao wanatokana na mimi na mimi natokana na wao, ewe Mwenyezi Mungu waridhie kama nilivyowaridhia."[259]

ii. Kutoka kwa Muhammad bin Umar Al-Kannasiy kutoka kwa Jafar bin Muhammad kutoka kwa baba yake kutoka kwa Ali bin Husein kutoka kwa Fatima mdogo kutoka kwa Husein bin Ali kutoka kwa Fatimah binti Muhammad alisema: "Alitujia Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu amejifaharisha kwenu, hivyo akawasamehe nyinyi wote kwa ujumla na akamsamehe Ali mahsusi, na hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, si mwenye kuogopwa kwa ajili ya watu wangu na ni mwenye kupendwa kwa sababu ya kizazi changu. Huyu hapa Jibril ananipa habari kuwa: Mwema wa kweli ni yule atakayempenda Ali wakati wa uhai wangu na baada ya kifo changu."[260]

259 *Dalailul-Imamah*, hadithi ya 2 na 3 na ya 34.

260 *Asnal-Matwalib* cha Shamsud-Din Al-Jazriyyu, 70.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 149



iii. Kutoka kwa Ali (a.s.) kutoka kwa Fatima (a.s.) alisema: "Mtume aliniambia: Ewe Fatima, atakayekuombea rehema wewe basi Mwenyezi Mungu atamsamehe na atamkutanisha na mimi peponi sehemu yoyote nitakayokuwepo."[261]

iv. Kutoka kwa Zaynab binti Ali kutoka kwa Fatima binti wa Mtume (s.a.w.w.) alisema: Mtume alisema kumwambia Ali: "Ewe Ali! Wewe na wafuasi wako ni watu wa Peponi."[262]

v. Fatima (a.s.) alisema: "Mtume aliniambia: Hivi huridhii kuwa mimi nimekuoza kwa mwislamu wa kwanza kuamini, mwenye elimu nyingi kuliko wao. Hakika wewe ni mbora wa wanawake wote wa ulimwenguni kama Mariam alivyokuwa mbora kuliko wanawake wote wa kaumu yake."[263]

vi. Kutoka kwa Sahl bin Saad Al-Answariy amesema: "Fatima binti wa Mtume (a.s.) aliulizwa kuhusu Maimam. Akajibu: Mtume alikuwa akimwambia Ali: "Ewe Ali! wewe ni Imam na khalifa baada yangu, na wewe una haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao, hivyo akipita Hasan ni mwanao Husein ndiye mwenye haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao. Akipita Husein ni mwanae Ali bin Husein ndiye mwenye haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao. Akipita Ali ni mwanae Muhammad ndiye mwenye haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao. Akipita Muhammad ni mwanae Ja'far ndiye mwenye haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao. Akipita Jafar ni mwanae Musa ndiye mwenye haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao. Akipita Musa ni mwanae Ali ndiye mwenye haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao. Akipita Ali ni mwanae Muhammad ndiye mwenye haki

261 *Kashful-Ghummah*, Juz. 1. Uk. 472.

262 *Dalailul-Imamah*, hadithi ya 2 na 3. Ihqaqul-Haq, Juz.7 Uk. 307. *Yanabiul-Mawadda* 257.

263 *Asnal-Matwalib* cha Allamah Al-Wasswaniy Al-Yammaniy.

zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao. Akipita Muhammad ni mwanae Ali ndiye mwenye haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao. Akipita Ali ni mwanae Hasan ndiye mwenye haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao. Akipita Hasan ni mwanae Mahdi ndiye mwenye haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao. Mwenyezi Mungu atafungua Mashariki ya ardhi na Magharibi yake kupitia yeye. Wao ndio Maimam wa haki na ndimi za kweli, atanusurika atakayewanusuru, atatelekezwa atakayewatelekeza."[264]

v. Aliashiria makusudio ya sheria ya kiislamu kwa kusema: "Mwenyezi Mungu ameweka imani kwa ajili ya kuwatakasa dhidi ya shirki. Swala kwa ajili ya kuwaepusha na kiburi. Zaka kwa ajili ya kuitakasa nafsi na kuongeza riziki. Funga kwa ajili ya kuimarisha ikhlasi. Hija kwa ajili ya kuimarisha dini. Uadilifu kwa ajili ya kuziunganisha nyoyo. Utiifu wenu kwa ajili ya nidhamu ya sheria. Uimamu wetu kwa ajili ya kusalimika na mfarakano. Jihadi kwa ajili ya kuupa heshima Uislamu. Subira ni msaada ili muwajibike kupata malipo. Kuamrisha mema ni masilahi ya wote. Kuwatendea wema wazazi wawili ni kinga dhidi ya adhabu ya Mwenyezi Mungu. Kuunga undugu ni kuongeza umri na kuongeza idadi. Kisasi ni kwa ajili ya kuhifadhi damu. Kutekeleza nadhiri ni kwa ajili ya kuomba msamaha. Kutimiza vipimo na mizani ni kwa ajili ya kuondoa ulaghai. Kukataza kunywa pombe ni kwa ajili ya kuwatakasa dhidi ya uchafu. Kujiepusha kutuhumu ugoni ni kwa ajili ya kuzuia laana. Kuacha wizi ni kwa ajili ya kupelekea nafsi kujimiliki. Mwenyezi Mungu akaharamisha ushirikina kwa ajili ya kumnyookea Yeye tu kwa Umola wake."

viii. Az-Zahrau (a.s.) alimuuliza baba yake: "Ewe baba yangu mpendwa, ni mambo gani yanayompata mwanaume na mwanamke anayed-

264 *Kifayatul-Athar* 193-200.

harau Swala?" Akajibu: "Ewe Fatima, mwanaume yeyote au mwanamke akipuuzia Swala Mwenyezi Mungu humtahini kwa kumpa mambo kumi na tano, sita hapa duniani, matatu wakati wa kifo chake, matatu kaburini, na matatu Siku ya Kiyama atakapotoka kaburini.

xi. Fatima (a.s.) alisema: Mtume aliniambia: "Jiepushe na ubahili hakika ni aibu isiyompata mkarimu. Jiepushe na ubahili hakika ni mti uliomo motoni na matawi yake yamo duniani, hivyo atakayeshika tawi moja kati ya matawi yake litamwingiza motoni. Kuwa mkarimu, hakika ukarimu ni mti kati ya miti ya peponi matawi yake yamening'inia hapa aridhini, hivyo atakayechukua tawi moja kati ya matawi yake litamwingiza Peponi."[265]

x. Fatima (a.s.) alisema: "Kufurahi mbele ya uso wa muumini kunawajibisha mwenye kufurahi kupata pepo, na kutabasamu mbele ya uso wa adui mpingaji kunamkinga mwenye kufurahi dhidi ya adhabu ya moto."[266]

xi. Fatima (a.s.) alisema: "Atakayepandisha ibada safi kwa Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu atamteremshia masilahi yake bora."[267]

xii. Mtume (s.a.w.w.) aliwauliza maswahaba zake kuhusu mwanamke, akasema: "Mwanamke ni nini?" Wakajibu: "Ni utupu." Akasema: "Ni wakati gani anakuwa karibu sana na Mola wake?"

265 *Ahlul-Bayt* cha Tawfiq bin Abu Ilmi, Uk. 130-131.

266 *Tafsirul-Imam* 354. Na makusudio ya kipengele cha pili ni kufanya taqiyya mbele ya maadui wa Ahlul-Bayt (An-Nawaswib).

267 *Biharul-An'war*, Juz. 71, Uk. 184.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 152



Hawakujua jibu. Ndipo Fatima (a.s.) aliposikia akasema: "Huwa karibu sana na Mola wake pindi anapotawa nyumbani kwake." Hapo Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Hakika Fatima ni kipande cha nyama yangu."[268]

xiii. Alimsifia mwanamke bora kwa kusema: "Mbora wao ni yule asiyetazamwa na wanaume wala asiyetazama wanaume."[269]

xiv. Kutoka kwa Ali bin Husein bin Ali (a.s.) amesema: "Hakika Fatima binti wa Mtume (s.a.w.w.) alimruhusu kipofu aingie kisha akamwekea pazia, hapo Mtume (s.a.w.w.) akamwambi: "Fatima kwa nini umemwekea pazia ilihali yeye hakuoni?" Akajibu: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! ikiwa yeye hanioni mimi namwona, na yeye ananusa harufu." Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Nakiri kweli wewe ni pande la nyama yangu."[270]

## Muhtasari:

Riwaya zilizopokewa kutoka kwa Az-Zahrau (a.s.) ni ushahidi tosha juu ya upana wa maarifa yake aliyokunywa kutoka kwenye chemchemu ya utume. Az-Zahra (a.s.) ana hotuba mbili mashuhuri ambazo zinawakilisha kina cha maarifa yake na upana wa elimu zake mbalimbali. Kupitia hizi hotuba mbili fasaha; historia imesajili nafasi yake adimu katika kugundua njama hatari zilizoukumba Uislamu, dola ya kiislamu na umma wa kiislamu baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.).
Az-Zahrau (a.s.) alimjali mwanamke wa kiislamu na familia ya kiislamu kupitia msimamo wake, semi zake na maagizo yake, hivyo akawa ni mfano mzuri wa mwanamke msomi wa kiislamu na

268 *Biharul-An'war,* Juz.43 Uk. 92.
269 *Hilyatul-Awliyai*, Juz. 2 Uk. 40.
270 *Mulhaqat Ihqaqul-Haq*, Juz. 10 Uk.258.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 153



mwanadamu kiongozi na kiigizo chema kwa kila mwanamke, na kuanzia hapa akapata medali ya mbora wa wanawake wote wa ulimwenguni.

## Maswali:

1. Taja mifano ya filosofia ya sheria ya Mwenyezi Mungu ndani ya urithi wa Az-Zahrau (a.s.)?

2. Elezea msimamo wa Az-Zahrau (a.s.) kuhusu uimamu baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)?

3. Toa dalili inayothibitisha jinsi Az-Zahrau (a.s.) alivyojali na kutilia umuhimu hadithi za Mtume (s.a.w.w.)?

4. Elezea mwenendo wa Az-Zahrau (a.s.) katika mahusiano yake na wanaume?

5. Muumini inampasa aweje?

6. Kutokana na maneno ya Az-Zahrau (a.s.) ni nani aliye mwema wa kweli?

**Mwisho wa dua zetu ni kumshukuru Mwenyezi Mungu**.

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 154



## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 155



27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n’amavuko by’ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur’ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur’an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake

59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju’l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju’l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja’a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 157



89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Wanawake katika Uislamu na mtazamo mpya
106. Idil Ghadiri
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Nne
112. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
113. Shiya N'abasahaba
114. Iduwa ya Kumayili
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Vikao vya Furaha

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 158



117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Historia na sera ya vijana wema
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaa ya kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Mas-ala ya Kifiqhi
139. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
141. Azadari

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 160



# Back Cover

Hakuna shaka kuwa historia ya mwanadamu ndio chemchemu na chanzo cha maarifa, chanzo ambacho mataifa yanakihitaji katika safari yake yenye kuendelea. Na ndio chanzo pekee chenye uwezo wa kuhuisha na kulisukuma taifa mbele na kulipa sifa na hadhi maalumu huku kikilifunganisha taifa hilo na mizizi yake ya ustaarabu ambayo hulizuwia taifa dhidi ya mmomonyoko.

Qur'ani inamhimiza kila mwanadamu ikimtaka azame ndani ya historia ya mwanadamu na azingatie yaliyomo ili awaidhike na kuongoka, hivyo Mwenyezi Mungu anasema: *"Je, hawatembei katika ardhi ili wapate nyoyo za kufahamia au masikio ya kusikilizia…?"* (22:46) Baada ya Mwenyezi Mungu kutoa historia ya Adi, Thamudi, Firauni, watu wa miji iliyopinduliwa na watu wa Nuh, akasema: *"Ili tuifanye ukumbusho kwenu na sikio lisikialo lisikie."* (69:12)

Historia ya ujumbe mbalimbali wa Mwenyezi Mungu imejaa masomo na mazingatio, masomo ambayo yameonyesha jinsi Manabii watukufu walivyojali mataifa yao ili kuyaokoa kutoka kwenye matatizo mbalimbali. Haya na mengine utayakuta ndani ya kitabu hiki.

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
**Al-Itrah Foundation**
S.L.P - 19701,
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info

Historia na sera ya viongozi wema D.Kanju.qxd 2/22/2010 8:12 AM Page 161